# Nipashe

Ijumaa Januari 25, 2019 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0579823

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper LIKE & FOLLOW US



Je, wajua? Magwiji 62 wamiliki nusu ya utajiri uliopo duniani

Ukurasa 14

Aliyetuhumiwa 'kuiba gari lake' anufaika fidia Sh. trilioni 2.7

Ukurasa 19

BUFE

Ijumaa Januari 25, 2019 Nipashe

BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA

Mambo 3 ya UNESCO kuelekea maendeleo 2030

Uchumi wa madini Mahenge, Ulanga ulivyoangukia mtihani na mwekezaji

Na Salome Samweli, TUDARCO, aliyekuwa Mahenge

UWAZI wa mikataba ya kampuni za wachimbaji wadogo na wakubwa wa madini katika kata ya Nawenge, kijiji cha Epanko, wilaya ya Ulanga mkoani Morogoro, sasa ni vita vya muda mrefu.

Hadi sasa serikali imesimamisha uchimbaji madini ya vito aina ya Rubi, yaliyopatikana kupitia wachimbaji we-...

...ya Morogoro.

Hapo pamegundulika kuwapo madini aina ya graphite au kinywe au grafiti, yanayotarajiwa kuchimbwa na kampuni zilizokwishapata leseni kutoka Wizara ya Nishati, ambazo ni: Tans Graphite, Mahenge Resource na Graphite Advancement, zilizoko katika hatua za utafiti, ulipaji fidia na tathimini za mazingira.

INAENDELEA UK.16

UCHUMI

Habari katika picha

Ukurasa 17

UKURASA 13



# Radi ilivyoua mama, mwanawe shambani

UKURASA 4

## MATOKEO KIDATO IV

# Udanganyifu watikisa



• **Wabomoa** madirisha kupitisha 'nondo' • **Wasichana** vinara kitaifa • **Hakuna** shule ya serikali 10 bora • **Walimu** shule ya Dar iliyoshika mkia kutimuliwa • **Matokeo** watahiniwa 381 yazuiwa kupisha uchunguzi... *Endelea ukurasa 2*

| SHULE 10 BORA 2018 | |
|---|---|
| 1. ST. FRANCIS GIRLS | (MBEYA) |
| 2. KEMEBOS | (KAGERA) |
| 3. MARIAN BOYS | (PWANI) |
| 4. AHMES | (PWANI) |
| 5. CANOSSA | (DAR) |
| 6. MAUA SEMINARY | (K'NJARO) |
| 7. PRECIOUS BLOOD | (ARUSHA) |
| 8. MARIAN GIRLS | (PWANI) |
| 9. BRIGHT FUTURE GIRLS | (DAR) |
| 10. BETHEL SABS GIRLS | (IRINGA) |

| SHULE 10 BORA 2017 | |
|---|---|
| 1. ST. FRANCIS GIRLS | (MBEYA) |
| 2. FEZA BOYS | (DAR) |
| 3. KEMEBOS | (KAGERA) |
| 4. BETHEL SABS GIRLS | (IRINGA) |
| 5. ANWARITE GIRLS | (K'NJARO) |
| 6. MARIAN GIRLS | (PWANI) |
| 7. CANOSSA | (DAR) |
| 8. FEZA GIRLS | (DAR) |
| 9. MARIAN BOYS | (PWANI) |
| 10. SHAMSIYE BOYS | (DAR) |

| SHULE 10 ZA MWISHO 2018 | |
|---|---|
| 1. PWANI MCHANGANI | (KAS. UNGUJA) |
| 2. UKUTINI | (KUS. PEMBA) |
| 3. KWEDIBOMA | (TANGA) |
| 4. RWEMONDO | (KAGERA) |
| 5. NAMATULA | (LINDI) |
| 6. KIJINI | (KAS. UNGUJA) |
| 7. KOMKALAKALA | (TANGA) |
| 8. KWIZU | (K'NJARO) |
| 9. SEUTA | (TANGA) |
| 10. MASJID QUBAH MUSLIM | (DAR) |

# Ajali ya basi yaua wanne, kujeruhi 42

UKURASA 3



# ...Mwanafunzi bora atoboa siri ushindi

UK. 2

MICHEZO SIMBA YAJIPANGA KUITESA BANDARI UK.32 MAONI, KATUNI UK.6

# Kinara kidato cha IV atoboa siri ya ushindi



**Na Romana Mallya**

MWANAFUNZI Hope Mwaibanje (18) (pichani), aliyeibuka kinara katika Mtihani wa Kidato cha Nne (CSEE) uliofanyika mwaka jana, ameeleza siri ya ufaulu wake.

Matokeo ya mtihani huo yalitangazwa jana, jijini Dodoma na Katibu Mkuu wa Baraza la Mitihani (Necta), Dk. Charles Msonde, huku Mwaibanje akitangazwa kuwabwaga watahiniwa wenzake 322,964.

Akizungumza na Nipashe jana akiwa jijini Mbeya muda mfupi baada ya kutangazwa kwa matokeo hayo, Mwaibanje alieleza jinsi ilivyokuwa ngumu kwake kuwa miongoni mwa wanafunzi 10 walioongoza kitaifa.

Alisema mara kwa mara walimu wao walikuwa wakiwaeleza kuwa, wakiweka juhudi katika masomo, watafanya vizuri katika, ikizingatiwa shule yao (Ilboru) inasifika kwa kufanya vizuri na kutoa wanafunzi bora kitaifa mara kwa mara.

"Maneno haya ya walimu ndiyo yaliyonifikisha hapa nilipo, ingawa matarajio yangu hayakuwa haya, nilikuwa napambana niwe miongoni mwa wanafunzi 10 bora kitaifa, lakini Mungu ameamua kuniinua zaidi, namshukuru sana," alisema.

Mwanafunzi huyo alisema ndoto yake ni kuwa daktari wa magonjwa ya moyo, anayoona ni changamoto kubwa nchini kwa sasa.

"Niseme ukweli, sikutegemea kama ningeongoza kitaifa, nilichokuwa napambana kusoma sana ni kuhakikisha kwenye wanafunzi 10 bora kitaifa sikosi, namshukuru Mungu, yeye ameamua kuniinua zaidi na kunifanya niongoze kitaifa," alisema.

"Ratiba ya kuingia darasani ilikuwa inaanzia saa moja asubuhi hadi saa nane mchana, baada ya kutoka darasani kuanzia saa tisa alasiri hadi saa 12 jioni, nilikuwa najisomea mwenyewe. Baada ya hapo dini, tukimaliza kuanzia saa mbili usiku hadi saa sita nilikuwa najisomea.

"Niseme ukweli kutoka moyoni, walimu wetu pia walikuwa karibu na wanafunzi, walikuwa wanatufuatilia hatua kwa hatua za ufaulu wetu. Pia

INAENDELEA UK. 8

## MATOKEO KIDATO IV

# Udanganyifu watikisa

**Na Augusta Njoji,**
DODOMA

BARAZA la Mitihani (Necta), limetangaza matokeo ya Mtihani wa Kidato cha Nne (CSEE) uliofanyika Novemba mwaka jana, huku likiwafutia matokeo watahiniwa 254 kutokana na udanganyifu na kuandika matusi.

Waliokumbwa na baa la kufutiwa matokeo ni pamoja na watahiniwa 57 wa Shule ya Sekondari Tumaini Lutheran Seminary iliyoko mkoani Morogoro.

Imeelezwa kuwa baraza limewafutia matokeo watahiniwa hao na kukifunga kituo hicho kutokana na kubainika kufanya udanganyifu kwenye mtihani huo.

Akitangaza matokeo hayo jijini Dodoma jana, Katibu Mtendaji wa Necta, Dk. Charles Msonde, alisema watahiniwa 252 walibainika kufanya udanganyifu kwa kuingia kwenye chumba cha mtihani wakiwa na notisi, maarufu nondo.

"Kati ya wanafunzi hao, 180 ni wa shule, 71 ni wa kujitegemea na mmoja ni wa mtihani wa maarifa (QT). Pia kuna wawili waliandika matusi kwenye karatasi zao za majibu," alisema.

Dk. Msonde pia alisema baraza limezuia matokeo ya watahiniwa 37 ambao walipata matatizo ya kiafya na kushindwa kufanya mtihani kwa baadhi ya masomo, huku likiwapa fursa ya kufanya mtihani huo mwaka huu.

"Baraza pia limezuia matokeo ya watahiniwa 136, hawa walipata matatizo ya kiafya na kushindwa kufanya mtihani kwa masomo yote, wamepewa fursa ya kufanya mtihani huo kama watahiniwa wa shule mwaka huu," alisema.

Alibainisha kuwa, matokeo ya watahiniwa 381, katika shule za St. Mathew's (228) na St. Mark's (153) yamezuiwa ili kufanyike kwanza uchunguzi wa tuhuma za kufanya udanganyifu.

**UDANGANYIFU TUMAINI**

DK. Msonde alisema hali ya ufanyaji wa mtihani huo ilikuwa salama maeneo yote nchini, isipokuwa kwenye Kituo cha Shule ya Sekondari Tumaini Lutheran Seminary iliyoko wilayani Malinyi, Morogoro.

Alisema baraza lilipokea taarifa kutoka kwa raia mwema kuwa kituo hicho kuna udanganyifu ulikuwa unafanyika kwenye mtihani huo.

"Baraza kwa kushirikiana na Kamati ya Mtihani ya Wilaya na Mkoa, walifika mara moja kwenye shule hiyo na kubaini mambo mbalimbali ukiwamo uharibifu wa miundombinu ya madirisha ili kupitisha majibu ya mitihani," alisema.

Dk. Msonde alisema uongozi wa shule kwa kushirikiana na walimu sita wa shule hiyo, watahiniwa wa kidato cha nne, baadhi ya wanafunzi wa kidato cha pili na tatu, wasimamizi wawili, askari polisi mmoja aliyekuwa na kazi ya kulinda mtihani, walipanga njama na kutekeleza

INAENDELEA UK. 8



Katibu Mtendaji wa Baraza la Mitihani la Taifa (NECTA), Dk. Charles Msonde (kulia), akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dodoma jana, wakati akitangaza matokeo ya mitihani ya kidato cha nne, iliyofanyika Novemba 2018, nchini kote. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Walimu wote shule iliyoshika mkia kidato cha IV kufukuzwa

**Na Romana Mallya**

WALIMU 12 waliokuwa wanafundisha katika Shule ya Sekondari Masjid Qubah Muslim Seminary jijini Dar es Salaam wanatarajia kufukuzwa na kuajiriwa wapya kutokana na shule hiyo kuwa ya mwisho kwenye matokeo ya mtihani wa kidato cha nne uliofanyika mwaka jana.

Katika matokeo ya mtihani huo yaliyotangazwa jana jijini Dodoma na Katibu Mtendaji wa Baraza la Taifa la Mitihani (Necta), Dk. Charles Msonde, shule hiyo iliyoko Kijitonyama jijini imefunga orodha ya shule 10 zilizofanya vibaya zaidi.

Shule hiyo ilikuwa na wanafunzi 43 waliandikishwa kufanya mtihani huo, lakini wawili (mvulana na msichana) hawakuufanya.

Kati ya wanafunzi 41 (wavulana 27) wa shule hiyo waliofanya mtihani huo na kuipa matokeo hayo mabaya, 15 wamepata daraja la IV na 26 wamepata daraja 0, hivyo shule yao haina ufaulu wa daraja I-III.

Mkurugenzi wa shule hiyo, Abubakar Musa, aliliambia Nipashe jijini Dar es Salaam jana, kuwa matokeo hayo yamesababishwa na uongozi mbaya uliopita. Alidai kupewa uongozi Desemba 28, mwaka jana, baada ya wanafunzi hao kufanya mtihani huo.

Musa alisema kuwa, baada ya kuchukua uongozi huo, hatua ya kwanza waliyofanya mwezi uliopita ni kumwondoa mkuu wa shule.

Kutokana na matokeo mabaya yaliyotangazwa jana, wameamua kuwaondoa walimu wote 12 waliokuwa wakifundisha shuleni hapo.

"Tulianza kuisafisha shule kwa kumwondoa mkuu wa shule kwa sababu hali haikuwa nzuri na matokeo ndio kama yanavyoonekana, watoto wamefeli wote. Walimu hawa 12 tuliwaambia tutawapima kutokana na ufaulu wa wanafunzi, kwa matokeo haya wote tunawafukuza," alisema.

Mkurugenzi huyo alisema walikaa kikao jana na kingine cha menejimenti kitakaa tena ili kuwaondoa walimu hao.

"Hatuwezi kuendelea na walimu hawa, kama ulivyoona ma

INAENDELEA UK. 8

## Serikali kutoa bil. 5/- kukamilisha hospitali

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

SERIKALI kupitia Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, inatarajia kutoa zaidi ya Shilingi bilioni tano kukamilisha ujenzi wa Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Shinyanga, ili ianze kufanya kazi ya kutoa huduma ya matibabu kwa wananchi, na kuwaepushia gharama kubwa za kwenda kutibiwa kwenye hospitali ya Bugando, jijini Mwanza.

Hospitali hiyo ilianza kujengwa rasmi mwaka 2014, ikiwa imeshakamilika jengo la utawala pekee kwa gharama ya Sh. bilioni 1.6.

Waziri wa wizara hiyo, Ummy Mwalimu, alisema hayo wakati alipofanya ziara ya siku moja mjini hapa kukagua ujenzi huo, Kituo cha Afya Kambarage na huduma za matibabu katika hospitali ya mkoa huo.

Alisema ukamilishwaji wa ujenzi wa hospitali hiyo ni muhimu, hivyo serikali itatoa Shilingi bilioni tano, ili kukamilisha majengo muhimu ya kutolea tiba, na ifikapo Julai Mosi, mwaka huu ianze kufanya kazi ya kutoa matibabu kwa wananchi.

"Mpaka sasa tumeshatenga Sh. bilioni 2.5 ambazo zitajenga majengo mawili ya mama na mtoto na Sh. bilioni 3.7 bado tunasubiri fedha zake ambazo zitajenga jengo la uchunguzi lenye vyumba vitatu vya upasuaji," alisema Ummy.

"Nataka niifanye hospitali hii ya rufani ya Mkoa wa Shinyanga kuwa ya kisasa kabisa, na wananchi kutokwenda kutibiwa Bugando tena, nitaweka vifaa tiba vya kisasa ikiwamo CT-Scan, pamoja na kuajiri madaktari bingwa wanane wa magonjwa mbalimbali ikiwamo ya wanawake na watoto ili kumaliza vifo vya uzazi," alisema.

Katika hatua nyingine aliwataka wananchi wa mkoa huo kujiunga na Mfuko wa Bima ya Afya ya Jamii CHF iliyoboreshwa, ili kuwapunguzia gharama kubwa za matibabu na hasa pale wanapougua ghafla na kujikuta hawana pesa, hali ambayo itasaidia kupata tiba bure na kuokoa maisha yao.

Naye Mganga Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Dk. Rashid Mfaume, akisoma taarifa ya mkoa huo, alisema kuna jumla ya zahanati 199, vituo vya afya 22, hospitali sita na ujenzi wa hospitali hiyo ya rufani ambayo imekoma kwenye jengo la utawala, pamoja na upungufu wa watumishi asilimia 52 na madaktari bingwa 21 na waliopo sita pekee.

# Radi yaua mama, mwanawe wakiwa shambani Geita

**Na Renatus Masuguliko,** GEITA

MAMA na mwanawe mwenye umri wa miezi sita wamefariki dunia papo hapo juzi baada ya kupigwa na radi wakati walipokuwa shambani katika Kijiji cha Msasa, wilayani Geita.

Akithibitisha kutokea kwa tukio hilo jana, Diwani wa Kata ya Busanda, Elias Kisome, aliwataja waliofariki kuwa ni Zainabu William (30) na mwanawe wa kike mwenye umri wa miezi sita, Happiness Bahati.

Akizungumzia mazingira ya tukio hilo, Diwani Kisome, alisema lilitokea saa 10 jioni wakati mama huyo na mwanawe alipokuwa shambani, akipanda mpunga. Alisema mvua iliyoambatana na radi ilimpiga Zainabu na mwanawe aliyekuwa amembeba mgongoni na kufariki papo hapo. Oktoba 17 mwaka jana wanafunzi sita wa darasa la pili na tatu katika shule ya msingi ya binafsi ya Emaco Vission English Medium School, iliyopo kata ya Nyankumbu katika Halmashauri ya mji wa Geita walifariki dunia baada ya kupigwa na radi na wengine 23 wakiwamo walimu wawili kulazwa katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Geita.




Mkuu wa Huduma za Kifedha wa Tigo, Hussein Sayed, akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam jana, wakati wa uzinduzi wa App ya Tigo Pesa katika kampeni inayojulikana kama "Appana Chezea Tigo Pesa App". Kulia ni Ofisa Biashara Mkuu wa Tigo, Tarik Boudiaf na Meneja Bidhaa wa Tigo Pesa App, Ian Ludovic. P**ICHA: JOHN BADI**

# RC apiga 'stop' wananchi kuhamishwa hifadhini

**Na Dege Masoli, TANGA**

MKUU wa Mkoa wa Tanga, Martine Shigela, amefuta notisi ya kuwahamisha zaidi ya wananchi 1,000 wanaoishi katika kitongoji cha Bondo kilichoko eneo la hifadhi ya msitu wa Bondo na kutoa maagizo mazito kwa watendaji mkoani hapa.

Wakazi wa kitongoji hicho kilichoko Kijiji cha Mswaki, wilayani Kilindi, walipewa notisi ya siku 30 na Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) kwa kile kilichoelezwa kuishi eneo la hifadhi hiyo kinyume cha sheria.

Akitoa maelekezo hayo juzi baada ya wakazi hao kulalamikia uhamisho huo, Shigela mbali na kusitisha uhamisho huo, pia alipiga marufuku kutobughudhiwa wananchi wanaoishi maeneo ya hifadhi zingine za mkoa wa Tanga hadi yatakapokamilika mazungumzo kuhusu wakazi hao.

Kwa mujibu wa Shigela, agizo la kutowabughudhi wananchi hao sambamba na kitongoji cha Bondo ni pamoja na wananchi wote waliomo hifadhi za Mwakijembe, wilayani Mkinga na Mkomazi, Korogwe.

Shigela alidokeza kuwa mwezi ujao atafanya vikao na TFS na watendaji wa serikali kwa ajili ya kutoa uamuzi namna wakazi hao wanavyoweza kuendelea kuishi katika maeneo hayo bila kusumbuliwa na kutoathiri uhifadhi wa misitu.

"Rais (John Magufuli) ameshatoa maagizo wananchi wasibughudhiwe na sasa ni jukumu letu viongozi kukaa na kuona ni namna gani wananchi hao wanaweza kuendelea na shughuli zao kwenye maeneo hayo kisheria. Sasa asitokee mtu tena akaenda kinyume cha agizo la Rais," alisema.

Aliwataka watendaji wa ngazi mbalimbali mkoani hapa kuacha kuwabughudhi wananchi wa maeneo hayo kwa kipindi hiki kwa kuwa hakuna maelekezo mengine zaidi ya aliyoyatoa Rais na kwamba kila kitu kimeshawekewa utaratibu wake na ni wajibu wao kuufuata.

Januari 15, mwaka huu, TFS iliwapa notisi wananchi hao ikiwataka hadi Februari 15 kuhama maeneo hayo kabla ya hatua kali dhidi yao kuchukuliwa na mamlaka hiyo.

Hata hivyo, wananchi hao walililalamikia kuwa agizo hilo linakinzana na agizo la Rais Magufuli la kutaka kuwekewa utaratibu wa namna ya wakazi wa vijiji vilivyomo kwenye hifadhi kuishi badala ya kubughudhiwa.

Wananchi hao walisema sababu ya kupinga uhamisho huo kuwa ni kutokana na kuishi katika maeneo hayo kwa miaka mingi, hivyo wamejiendeleza ikiwamo kujenga shule kwa nguvu zao na ulinzi kuhusika na ulinzi wa mazingira ya hifadhi hiyo.

Walisema TFS katika notisi ya kuwataka kuyahama makazi yao, haikuonyesha wanakotakiwa kwenda kuishi na namna watakavyohama, jambo linalowapa utata.

## TANGAZO




215024102

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Tunazalisha taifa gani kwa udanganyifu wa mitihani?

**VITENDO** vya udanganyifu katika matokeo ya mitihani ya taifa ya elimu ya msingi na sekondari vimekuwa ni jambo la kawaida kila mwaka.

Kila matokeo yanapotangazwa, haikosekani kusikia vitendo vya kughushi ambavyo vinawahusisha walimu, wasimamizi, wanafunzi na polisi, ambao wanakwenda kuweka ulinzi.

Matukio haya yamekuwa ni jambo la kawaida kana kwamba yamehalalishwa, kutokana na wahusika kutokuogopa kuchukuliwa hatua kali za kisheria na za kinidhamu.

Tunashangaa kuona wanafunzi wakiendelea kushiriki katika mchezo huo mchafu bila kujali kwamba, wenzao waliofanya hivyo walifutiwa matokeo. Pia walimu hawalioni hili kuwa ni hatari kwao kutokana na wenzao waliofanya hivyo kujikuta wakishushwa vyeo, kufukuzwa kazi na kufunguliwa kesi mahakamani.

Katika matokeo ya mwaka 2017 tulishuhudia jinsi mtandao mpana wa udanganyifu wa mtihani wa taifa wa darasa la saba ulivyofanya udanganyifu mkubwa na matokeo yake idadi kubwa ya wanafunzi kufutiwa matokeo pamoja na hatua kali kwa wahusika wengine wakiwamo walimu na walimu wakuu.

Kabla tukio hilo halijasahaulika, serikali imefichua njama nyingine za udanganyifu katika mtihani wa taifa wa kidato cha nne wa mwaka 2018.

Baraza la Mitihani (Necta), limetangaza matokeo ya mtihani huo, huku likiwafutia matokeo watahiniwa 254 kutokana na udanganyifu na kuandika matusi. Waliofutiwa matokeo ni pamoja na watahiniwa 57 wa Shule ya Sekondari Tumaini Lutheran Seminary iliyoko mkoani Morogoro.

Katibu Mtendaji wa Necta, Dk. Charles Msonde, akitangaza matokeo hayo jana, alisema watahiniwa 252 walibainika kufanya udanganyifu kwa kuingia kwenye chumba cha mtihani wakiwa na notisi, maarufu 'nondo'.

Pia alisema baraza limezuia matokeo ya watahiniwa 381 katika shule za St. Mathew's (228) na St. Mark's (153) yakizuiwa ili kufanyike kwanza uchunguzi wa tuhuma kufanya udanganyifu.

Alisema kwenye Kituo cha Shule ya Sekondari Tumaini baraza lilipokea taarifa kutoka kwa raia mwema kuwa kuna udanganyifu ulikuwa unafanyika kwenye mtihani huo.

Hivyo kwa kushirikiana na Kamati ya Mtihani ya Wilaya na Mkoa, walifika kwenye shule hiyo na kubaini mambo mbalimbali ukiwamo uharibifu wa miundombinu ya madirisha, ili kupitisha majibu ya mtihani, alisema.


Kwamba uongozi wa shule kwa kushirikiana na walimu sita, watahiniwa wa kidato cha nne, baadhi ya wanafunzi wa kidato cha pili na tatu, wasimamizi wawili, askari polisi mmoja aliyekuwa na kazi ya kulinda mtihani, walipanga njama na kutekeleza kufanya udanganyifu wa mtihani.

Dk. Msonde alisema uongozi wa shule uliwapatia jukumu maalum baadhi ya wanafunzi wa kidato cha pili na tatu kuchukua mitihani kutoka kwa watahiniwa kupitia kwenye madirisha na matundu yaliyotobolewa kwenye vyumba vya mitihani na kuwafikishia walimu wa masomo waliokuwa kwenye chumba maalum kwa lengo la kuyatolea majawabu.

Aidha, wanafunzi hao walishirikiana na walimu hao kunakiri majibu yaliyoandaliwa na hatimaye kwa kushirikiana na askari polisi aliyekuwa kituoni, majawabu yalirejeshwa kwa watahiniwa kwenye chumba cha mtihani.

Madudu haya lazima sisi kama taifa tusikubali yaendelee kwa kuwa hayawezi kutusaidia kujenga taifa lenye wataalamu bali wajinga. Tujitafakari!

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Mhariri Wikiendi:** Epson Luhwago
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311.
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




Muungwana Lazima Nilonge



# Wazazi mnapokimbia vikao vya shule, mnategemea nini?

Na Yasmine Protace

**VIKAO** vya shule vinapofanyika, ni moja ya njia za kukutanisha pande mbili; wazazi,walezi dhidi ya walimu wao.

Lengo la kuwapo vikao hivyo ni kujadili mambo mbalimbali ambayo yanaweza kuleta maendeleo katika shule, ikiwamo kuboresha mikakati ya kimasomo.

Inawezekana uongozi wa shule ukaitisha kikao kwa ajili ya kuzungumzia changamoto ambazo zinaikabili shule mbele ya wazazi na kufanyika maamuzi kupitia kikao hicho, juu ya namna ya kukabiliana na changamoto hizo.

Inajulikana shule peke yake haiwezi kukaa na kufikia kuamua jambo fulani linalowahusu wanafunzi, bila ya kuwaridhisha wazazi.

Mtu akiangalia hata katika baadhi ya shule, anakuta kamati zinazoundwa wajumbe, daima hawakosekani wazazi walio na watoto katika shule hizo.

Hiyo yote ni njia ya kuunga mkono juhudi za wazazi walio na watoto masomoni mahali hapo.

Kikubwa kinachonisikitisha ni kwamba, katika shule ambazo wazazi wamewapeleka watoto kusoma, baadhi ya wazazi daima au mara nyingi wana tabia ya kutofika mikutanoni, kadri inavyoandaliwa na shule hizo.

Pamoja na shule kuwa na kalenda ambayo kila mtoto anakuwa na hayo na inaonyesha ratiba za mikutano, lakini wazazi baadhi wao hawafiki.

Sasa tujiulize, kama mzazi ukufika katika mkutano unategemea nani afike kwa niaba yako?

Tunajua mtu anaweza kutingwa na kazi, lakini hiyo sio sababu ya kushindwa kuhudhuria mkutano, kwani unaweza kutuma hata mwakilishi.

> **Kikubwa kinachonisikitisha ni kwamba, katika shule ambazo wazazi wamewapeleka watoto kusoma, baadhi ya wazazi daima au mara nyingi wana tabia ya kutofika mikutanoni, kadri inavyoandaliwa na shule hizo.**

Kutofika katika mikutano ndio kunasababisha hata mazungumzo wakati mwingine kutofikiwa katika muafaka sahihi.

Katika mikutano, kuna suala la kusikiliza historia ya shule, changamoto zake, pia nini kinapaswa kufanyika.

Baada ya kusikiliza hayo, ndipo wazazi wanatoa maazimio na wanakuwa wamekubaliana.

Lakini, kutofika kwa wazazi na maazimio yakiwa yametolewa, baadhi ya wazazi hao wanakuwa wagumu katika utekelezaji wake, kutokana na kwamba awali hawakushiriki katika mkutano.

Cha muhimu ni wazazi kuhudhuria katika mikutano na hata kama hawezi kufika, basi atume mwakilishi ili amjuze yaliyotokea shuleni.

Pia, hata nyie wazazi mnaofika katika mkutano, muwepo hapo kwa wakati kama mnavyoambiwa kupitia taarifa na ratiba stahiki.

Unakuta mkutano unaanza saa nne asubuhi, mzazi anafika saa saba, wanapofika katika majumuisho yeye anaanza kupinga hoja, wakati yeye ndiye aliyefika kachelewa. Nimeshuhudia hayo.

Ushauri wangu ni kwamba, mikutano ya shule tusiidharau kwa sababu ni mikutano kama mikutano mingine kwani inazungumzia maisha ya watoto na misaada ya wazazi inatakiwa ili kuziokoa shule zinapokuwa na changamoto.

Kama wazazi mtaendelea kuikimbia mikutano ya shule, basi muache kulaumu mabadiliko ambayo yanakuwa yanatolewa na shule katika utoaji elimu.

## BARUA/MJADALA

## *Tujipange kidato cha kwanza*

**Mhariri,**

*KATIKA mwaka huu kumeshuhudiwa na kunaendelea kushuhudiwa mtihani mkubwa unaoendana na upungufu ya wanafunzi wanaojiunga na kidato cha kwanza.*

*Mamlaka ya juu kiserikali, ilishaagiza kwamba hakuna mtoto aliyechaguliwa kuendelea na masomo, atakayeachwa nyumbani kwa kigezo chochote kile.*

*Ni aina ya agizo inayoendana na tamko la huko nyuma, ikiwataka mabinti wote waliofaulu kuendelea na masomo wanapewa haki zao.*

*Kikubwa katika hoja yangu ni kwamba, kuna jambo nililogundua kwamba, kama hakutakuwapo hatua thabiti ya kukabili ugumu huo, tatizo tunalolishuhudia hivi sasa, pia itajitokeza mwakani.*

*Nasema hivyo, kwani mazingira na sababu ziko wazi kwamba panawagusa wengi huku mwakani kuna matarajio kwamba waliofaulu ni wengi zadi.*

**Mashilema Gambi, Bunda**

## *Makondakta daladala badilikeni*

**Mhariri,**

*BADO huwa ninashangazwa na tabia ya baadhi ya ama madereva au makondakta wao katika daladala, au wote kwa pamoja, wanaruhusu tabia ya abiria yao kuendelea kuning'inia.*

*Wakati hao wanaendekeza tabia hiyo, ndugu zao polisi wa usalama barabarani ni wakali sana dhidi ya tabia hiyo.*

*Nikiwa katika maoni ninayoyaeleza jijini Dar es Salaam, huwa najiuliza, hawa wachache ambao wameshapata mafunzo mengi, kukumbana na adhabu na mengine ambayo ni kinyume na hicho kwa nini hawataki kubadilika?*


*Rai yangu kwa ndugu wa usalama barabarani, waendelee kuwa wakali sambamba na kuchukua hatua kali dhidi ya tabia hiyo.*

**Magelina Saidi,**
**Dar es Salaam.**

### WASILIANA NASI:

**TUNAKARIBISHA BARUA NA MAONI YA MSOMAJI, UNAWEZA KUTUMA KUPITIA KWA MHARIRI S.L.P. 31042, DAR ES SALAAM AU mhariri@nipashe.co.tz**

# Hii ndio staili inayosaidia, kumaliza migogoro ardhi




**Na Sabato Kasika**

MIGOGORO ya ardhi ni changamoto, inayokuwapo katika maeneo mbalimbali nchini, ikihusisha makundi mbalimbali, inayojumuisha wakulima na wafugaji na hata wananchi na wawekezaji.

Kwa upande wa wafugaji, wamekuwa wakihama kila mara kutoka eneo moja, kwenda jingine kutafuta malisho na maji kwa ajili ya mifugo yao na kujikuta wakituhumiwa kuingiza mifugo katika mashamba ya wakulima.

Mbali na hilo, kumekuwapo na migogoro inayohusisha kuwaondoa wanaodaiwa kuvamia maeneo ya hifadhi, kwa ajili ya kutunza mazingira, hali inayosababisha uhasama kati ya wananchi na viongozi wa serikali.

Hiyo ni miongoni mwa sababu ambazo zimekuwa zikichangia migogoro hadi kuwapo kwa mapigano kati ya makundi hayo mawili na hata kwa wale ambao wamekuwa wakituhumiwa kuvamia maeneo ya hifadhi.

Pia, kumekuwapo jitihada mbalimbali zinazofanywa na serikali, kuhakikisha migogoro hiyo inayojitokeza kila mara, inagekuwa historia.

Hivi karibuni Rais Dk. John Magufuli, aliagiza kusitishwa mara moja uondoaji vijiji na vitongoji vinavyodaiwa kuwapo kwenye maeneo ya hifadhi.

Uamuzi huo wa rais ninauchukulia kwamba unalenga kumaliza migogoro hiyo, ili Watanzania waishi kwa amani katika nchi yao, bila ya kuhasimiana kwa sababu ya kugombea ardhi au kufukuzwa katika maeneo waliomo.

Watanzania ni wamoja na kwa umoja wao wanatakiwa kuendelea kushirikiana kwa mambo mbalimbali ya maendeleo, hivyo ni wazi kwamba kuondoa vitu ambavyo vilikuwa vinasababisha wasielewane, ni jambo zuri.

Anawataka viongozi wabainishe maeneo ya hifadhi za wanyamapori na misitu, ili ambayo hayana wanyamapori au misitu yagawiwe kwa wafugaji na wakulima wanaohangaika kupata maeneo ya kufugia na kuzalisha mazao.

Katika uamuzi huo, pia Rais anaagiza sheria ya vyanzo vya maji iangaliwe upya ili kutowazuia Watanzania wanaozalisha mazao kandokando ya mito.

Aidha, Rais anaelezea kutofurahishwa na vitendo vya kufyeka mazao ya wakulima, kwa madai kuwa wamelima ndani ya mita 60.

Viongozi waliopewa maagizo ni kutoka Wizara za Maliasili na Utalii; Mifugo na Uvuvi; Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi); na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi.

Rais anasema, ni lazima serikali ifanye uamuzi huo kwa sababu idadi ya Watanzania imeongezeka hadi kufikia milioni 55 na mifugo.

Pia, imeongeza hadi kufikia milioni 35 na kwamba kutokana na ongezeko hilo la watu na mifugo, kuna ongezeko kubwa la mahitaji ya maeneo ya ardhi.

Anasema, idadi hiyo ni tofauti ikilinganishwa na wakati nchi inapata uhuru, kwa vile wakati huo Watanzania walikuwa milioni tisa na mifugo milioni 10.

"Mimi sifurahii kuona wafugaji kila mahali wanafukuzwa. Kama kuna eneo ambalo tunafikiri lilikuwa hifadhi ya wanyama, lakini halitumiki, tutabadilisha sheria, tunalimega na tunaligawa kwa wafugaji.

"Vivyo hivyo, hata kwa wakulima kama kuna eneo tunaona, ni hifadhi, lakini halina msitu wala wanyamapori na lina rutuba na wakulima wanataka kulima nalo, tunalimega tunawapa wakulima.

"Baadaye tutajua kabisa eneo hili ni la hifadhi, hili ni la mifugo, hili ni la wakulima, hili ni la makazi. Kwa hiyo, ninyi mawaziri na makatibu wakuu mkakae mkatangulize maslahi ya hawa tunaowaongoza, ambao ni wakulima, wafugaji, wavuvi na kadhalika.

"Lakini, pia tunahitaji wanyamapori, sijasema sasa hifadhi zote za wanyama tunazimaliza. Hapana, hifadhi za wanyama lazima tuzihifadhi," anasema Rais Magufuli.

Kwa ujumla ni kwamba kilichofanywa na rais kinaweza kuwa na mchango mkubwa katika kuepusha migogoro ya ardhi, ambayo imekuwa ikishuhudiwa maeneo mbalimbali nchini.

Ikumbukwe kuwa, watu milioni 55 ni wengi na pia mifugo milioni 35 ni mingi, hivyo ni muhimu yawepo maeneo ya kutosha kwa ajili ya kilimo, ufugaji na shughuli nyingine za maendeleo.

Hivyo ninaamini kwamba kuna uwezekano mkubwa wa migogoro ya ardhi kupungua, kama siyo kumalizika kabisa iwapo kila upande utazingatia maelekezo, ambayo rais ameyatoa.

## KABWELA NA FADHIL MOHAMMED



# Udanganyifu watikisa

INATOKA UK. 2

kufanya udanganyifu wa mtihani.

"Wanafunzi wa kidato cha pili ni Cana Mwalyosi, Focus Ligongo, wanafunzi wa kidato cha tatu ni Edson Mwiche, Hassan Yohana, Francis Maongezi, Asbert Njavale, Juma Magambe, Christopher Tapule na Sharifu Alle," Dk. Msonde aliwataja.

Wengine waliotajwa na mtendaji huyo wa Necta ni wasimamizi Hassan Nguvila na Jovera Lujara, askari polisi G7281 PC Khamis, na walimu wa shule hiyo; Diana Kajanja, Michael Mang'ande, Samwel Mngwasa, Amos Nyenja, Japhary Matengo na Nivodem Libebefu.

Pia walimu wa taaluma; Mpollo na David Kambanyuma na Mkuu wa Shule hiyo, Eliud Payovela.

Dk. Msonde alisema uongozi wa shule uliwapatia jukumu maalum baadhi ya wanafunzi wa kidato cha pili na tatu kuchukua mitihani kutoka kwa watahiniwa kupitia kwenye madirisha na matundu yaliyotobolewa kwenye vyumba vya mitihani na kuwafikishia walimu wa masomo waliokuwa kwenye chumba maalum kwa lengo la kuyatolea majawabu.

"Aidha, wanafunzi hao walishirikiana na walimu hao kunakiri majibu yaliyoandaliwa na hatimaye kwa kushirikiana na askari polisi aliyekuwa kituoni, majawabu yalirejeshwa kwa watahiniwa kwenye chumba cha mtihani," alisema.

Dk. Msonde alisema kamati ilibaini uwapo wa karatasi nyingi zilizokuwa na majibu ya somo la Kemia nje ya vyumba vya mitihani, ambayo yalifanana na maswali yote ya mtihani wa somo hilo uliokuwa unaendelea kufanyika.

Alisema walimu wote walioshiriki hujuma hiyo walikamatwa, kuhojiwa na kukiri kuhusika kwao kufanya udanganyifu katika mitihani ya masomo ya Hisabati, Jiografia, Historia na Kemia ambayo yalikuwa yameshafanyika.

**UAMUZI WA BARAZA**

Dk. Msonde alisema baraza limeamua kufuta matokeo yote ya watahiniwa 57 wa shule hiyo, kuifungia shule hiyo kuwa kituo cha mitihani hadi baraza litakapojiridhisha kuwa kituo hicho ni salama kuendesha mitihani ya taifa.

"Bodi ya Shule ya Tumaini pia iwachukulie hatua kali za kinidhamu wanafunzi wa kidato cha pili na cha tatu walioshiriki kufanikisha udanganyifu huo," alisema.

Aliongeza nguvu baraza limeagiza mamlaka husika iwachukulie hatua stahiki walimu na askari polisi walioshiriki udanganyifu kwa mujibu wa kanuni za utumishi na sheria za nchi.

**SHULE 10 BORA**

Dk. Msonde alizitaja shule 10 bora katika mtihani huo kuwa ni St. Francis Girls (Mbeya), Kemebos (Kagera), Marian Boys na Ahmes (Pwani), Canossa (Dar es Salaam), Maua Seminary (Kilimanjaro), Precious Blood (Arusha), Marian Girls (Pwani), Bright Future Girls (Dar es Salaam) na Bethel Sabs Girls (Iringa).

**SHULE 10 ZA MWISHO**

Kiongozi huyo wa Necta alizitaja shule 10 zilizofanya vibaya zaidi katika mtihani huo kuwa ni Pwani Mchangani (Kaskazini Unguja), Ukutini (Kusini Pemba), Kwediboma (Tanga), Rwemondo (Kagera), Namatula (Lindi), Kijini (Kaskazini Unguja), Komkalakala (Tanga), Kwizu (Kilimanjaro), Seuta (Tanga) na Masjid Qubah Muslim (Dar es Salaam).

**WANAFUNZI 10 BORA**

Aliwataja watahiniwa 10 waliofanya vizuri zaidi mtihani huo kuwa ni Hope Mwaibanje (Ilboru), Avith Kibani (Marian Boys), Maria Manyama, Atughulile Mlimba, Flavia Nkongoki na Leticia Ulaya (wote St. Francis Girls), Gibson Katuma na Bryson Jandwa (wote Marian Boys), Idegalda Kiluba (St. Francis Girls) na Isack Julius (Marian Boys).

**WASICHANA 10 BORA**

Dk. Msonde alisema wasichana 10 waliong'ara zaidi katika mtihani huo Maria Manyama, Atughulile Mlimba, Flavia Nkongoki na Leticia Ulaya, Idegalda Kiluba, Subilaga Mwaisela, Joyce Sapali, Ivory Anangisye, Saraha Kasala (wote St. Francis Girls) na Theresia Karuga (Anwarite Girls).

**WAVULANA 10 BORA**

Kwa upande wa wavulana 10 waliofanya vizuri zaidi katika mtihani huo, Dk. Msonde alisema wanaongozwa na Hope Mwaibanje (Ilboru) akifuatwa na Avith Kibani, Gibson Katuma, Bryson Jandwa na Isack Julius (wote Marian Boys), Justine Byarasobile (Katoke Seminary), Emmanuel Kandege (Uwata), Saitoti Opendo (Ilboru), Peter Kiama (Feza Boys), David Sichone (Pandahili).

**HALI YA UFAULU KITAIFA**

Alisema watahiniwa 426,988 walisajiliwa kufanya mtihani huo. Kati yao, wasichana ni 219,171 (asilimia 51.33) na wavulana 207,817 (asilimia 48.67).

Alisema watahiniwa wa shule ni 7,527 (asilimia 2.5) na wa kujitegemea 5,264 (asilimia 8.93) hawakufanya mtihani huo licha ya kusajiliwa.

Pia alisema watahiniwa 322,965 (asilimia 78.38) wamefaulu. Kati yao, wasichana ni 163,920 (asilimia 77.58) wakati wavulana ni 159,045 (asilimia 79.23).

"Mwaka 2017, watahiniwa waliofaulu walikuwa ni 287,713, sawa na asilimia 77.09," alisema na kubainisha kuwa ufaulu umeongezeka kwa asilimia 1.29 mwaka 2018 ikilinganishwa na mwaka 2017.

Kwa upande wa QT, Dk. Msonde alisema waliofaulu ni 7,642 sawa na asilimia 62.46. Mwaka 2017, walifaulu 8,280 (asilimia 60.11), hivyo ufaulu umeongezeka kwa asilimia 2.35.

Alisema watahiniwa 113,825 wamefaulu kwa daraja la kwanza hadi la tatu. Kati yao, wasichana ni 47,779, sawa na asilimia 26.25 na wavulana ni 66,046 (asilimia 37.43).

Somo la Kiswahili, alisema limeongoza kwa kuwa na ufaulu wa juu (asilimia 89.32 ya watahiniwa wamefaulu), huku somo la hisabati likiendelea kuwa changamoto kwa watahimiwa wengi likiwa na ufaulu wa chini kwa asilimia 20.02.

# Mwanajeshi matatani tuhuma kubaka

**Na Ashton Balaigwa,**
MOROGORO

ASKARI wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ), kambi ya Suku Mikumi, wilayani Kilosa mkoani Morogoro, Godlisten Remngstone (46), anashikiliwa na polisi kwa tuhuma za kufanya mapenzi na binti wa miaka 17, mwanafunzi wa kidato cha nne.

Akizungumza na waandishi wa habari, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Morogoro, Wilbrod Mutafungwa, alisema askari huyo alikamatwa Januari 23, mwaka huu, majira ya alasiri maeneo ya Kikwalaza, Mikumi Wilaya ya Kilosa. Alisema kuwa askari huyo alikamatwa na wananchi na kufikishwa katika kituo cha polisi Mikumi baada ya kumwita mwanafunzi huyo na rafiki yake nyumbani kwake kwa nia ya kufanya naye mapenzi.

Katika tukio lingine Paulo Ilonga (68), anashikiliwa na polisi kwa tuhuma za kuwabaka watoto wawili wa familia moja mmoja akiwa na umri wa miaka minane na mwingine miaka tisa, wakiwa watoto wake wa kufikia.

Kamanda Mutafungwa alisema mtuhumiwa huyo aliwabaka watoto hao baada ya kuwatoa ndani walikolala na kuwapeleka nyuma ya nyumba, huku akiwatishia kuwapiga.

Katika hatua nyingine Jeshi la Polisi linamshikilia Jafari Ramadhani (26), mkazi wa Kidudwe Turiani, kwa tuhuma za kumbaka mwanawe wa kumzaa mwenye umri wa miaka sita baada ya kumwita chumbani.

Tukio hilo lilitokea Januari 21, mwaka huu saa nne asubuhi katika kijiji cha Kidudwe Turiani, baada ya mama mzazi wa mtoto huyo kugundua kuwa mtoto wake amebakwa na hivyo kutoa taarifa polisi.

Watuhumiwa wote watafikishwa mahakamani uchunguzi na taratibu za kisheria utakapokamilika.

# Kinara kidato cha IV atoboa siri ya ushindi

INATOKA UK. 2

ninamshukuru Mungu kwa kuwa hakuniacha kila hatua.

"Endapo mwanafunzi akiamua kuachana na mambo mengine na kufikiria yale tu ambayo yamewapeleka masomoni, kwanini basi mwanafunzi wa namna hii asifikie lengo lake la kupata ufaulu wa juu, ila wasimwache Mungu."

Kinara huyo wa ufaulu alibainisha kuwa, kuanzia darasa la kwanza hadi la saba, akiwa Shule ya Msingi Lioto, Mbeya Mjini, alikuwa miongoni mwa wanafunzi watatu bora, lakini alikutana na wakati zaidi alipojiunga na Ilboru na changamoto kubwa kwake ilikuwa lugha ya Kiingereza.

"Si unajua, unapotoka shule za msingi za serikali, lugha ya Kiingereza huwa changamoto, lakini hili halikunifanya nirudi nyuma, mwaka wa kwanza ulikuwa na changamoto na ufaulu wangu haukuwa mzuri, lakini kuanzia kidato cha pili nilifanya vizuri," alisema.

Mwaibanje alisema alipata taarifa ya kufanya vizuri kwenye mtihani huo jana asubuhi baada ya rafiki yake, Allen Diadoni, kumpigia simu kumjulisha kuwa ameongoza kitaifa.

"Wakati huo nilikuwa nyumbani, sikuamini kwa sababu hayakuwa matarajio yangu, nikajua ananidanganya, lakini simu zilienedelea kupigwa za kupongezwa na baada ya muda nilihakikisha mwenyewe baada ya kuona matokeo yangu namshukuru Mungu," alisema.

# Walimu wote shule iliyoshika mkia

INATOKA UK. 2

tokeo, kwa kweli siyo mazuri, yamechafua shule. Tutaajiri walimu wapya, tunataka kurudisha sifa ya shule kwa sababu hata ukiangalia matokeo ya nyuma, shule haijawahi kushika mkia kama hivi," alisema.

Musa aliongeza: "Miaka ya nyuma, ilishawahi kushika nafasi ya 50 kitaifa, na hapa kwa sasa tuna wanafunzi wa kidato cha kwanza hadi cha sita ambao kidato cha tano na sita wanafanya vizuri, hata matokeo ya mwaka jana hayakuwa mabaya," alisema.

**SABABU ZAIDI**

Licha ya kuamua kuwatimua walimu, Musa alieleza sababu nyingine ambazo anaamini zimechangia shule hiyo kuanguka kielimu kuwa ni pamoja na uongozi uliopita kutowalipa walimu wake kwa wakati na kusababisha shule kupoteza mwelekeo.

"Uchukuaji wa wanafunzi ili kujiunga shule haukuzingatia ufaulu, watoto waliletwa walioshindikana," Musa alisema, "wazazi nao walikuwa hawalipi kwa wakati.

"Shule ilikuwa na chanzo kimoja cha uingizaji mapato ambacho ni ada. Wazazi hawalipi ada kwa wakati au wasilipe kabisa. Ada ilikuwa ni Sh. 700,000 kwa mwaka, mwisho wa siku walimu nao wanakosa mishahara, yaani hakukuwa na usimamizi mzuri kutokana na uongozi mbaya."

Alisema changamoto nyingine shuleni kwake ilikuwa uhaba wa walimu kwenye baadhi ya masomo na usimamizi mbaya wa wanafunzi uliosababisha wengi kuwa watoro bila kuchukuliwa hatua.

"Unakuta wanafunzi hawajaonekana shule miezi mitatu, lakini siku ya mitihani ya mwisho walikuja na kufanya mitihani, sasa hapo ndio unajiuliza, mwalimu alikuwa anategemea kupata matokeo gani ya ufaulu kwa watoto wa aina hii?" Musa alihoji.

Alisema anaamini uongozi mpya ulio chini yake, utaongeza jitihada ili warejeshe heshima ya shule hiyo, akibainisha kuwa matokeo yaliyotangazwa jana, ndiyo mabaya zaidi kwa shuleni hapo tangu mwaka 1988 ilipoanzishwa.

Musa aliitaja mikakati yake anayoamini itarejesha heshima ya shule hiyo kuwa ni pamoja na kuajiri walimu wapya wenye sifa, kukarabati miundombinu ya shule na kujenga uzio ili kukabiliana na utoro.

# Mlinzi wa zahanati ajinyonga chumba cha sindano hadi kufa

**Na Gurian Adolf,** NKASI

MLINZI wa zahanati ya Kijiji cha Katani Kata ya Nkandasi wilayani Nkasi, mkoani Rukwa, Laudifasi Sokoni (60), amejinyonga katika chumba cha kuchomea sindano wagonjwa cha zahanati hiyo kwa kutumia shuka lake.

Tukio hilo lilibainika asubuhi ya Januari 23 muda mfupi baada ya wahudumu kufika kazini kwa ajili ya kuanza maandalizi ya kutoa huduma.

Akizungumzia tukio hilo Mwenyekiti wa Kijiji hicho, Jofrey kisato, alisema kuwa baada ya wahudumu wa zahanati hiyo kufika kazini na kuanza kuandaa mazingira ya kutoa huduma, ndipo walipogundua tukio hilo hali iliyosababisha watoe taarifa kwenye uongozi wa kijiji nao ukatoa taarifa kituo cha polisi.

Alisema marehemu alikua ni mlinzi wa zahanati ya kijiji na alikuwa akiishi peke yake kwa muda mrefu kutokana na mkewe kufariki dunia na hadi sasa hawajui chanzo cha kuamua kujinyonga.

"Inaonekana alidhamiria kujinyonga kwa kuwa alikwenda eneo lake la lindo na shuka, ambalo alitumia kujinyonga, na usiku wa kuamkia siku hiyo aliamua kujitundikia kwa kutumia shuka hilo na wahudumu wa zahanati hiyo waligundua mwili wake ukining'inia wakati wakiandaa mazingira ya kutoa huduma," alisema na kuongeza:

"Hali hiyo ilisababisha baadhi ya wagonjwa kuingiwa hofu na kutimua mbio bila kupata huduma."

Kwa upande wake Kamanda wa Polisi mkoa wa Rukwa, George Kyando, alithibitisha kutokea kwa tukio hilo na kuongeza kuwa marehemu hakuacha ujumbe wowote.

Alisema baada ya polisi kufanya uchunguzi wa awali walibaini kuwa chanzo cha marehemu kuchukua uamuzi huo ni kutokana na kukabiliwa na maisha magumu pamoja na upweke.

Kamanda Kyando alisema tangu mke wa marehemu kufariki dunia, mlinzi huyo aliendelea akionekana kuwa na msongo wa mawazo pamoja na hali ngumu ya maisha inayomkabili ndiyo sababu zilizosababisha kujinyonga.

Alisema polisi wanaendelea na uchunguzi ili kubaini chanzo hasa cha Sokoni kufikia uamuzi wa kujinyonga.

# Wadau wajadili njia za mifugo kwenye mnada

**Na Mwandishi Wetu**

WIZARA ya Mifugo na Uvuvi, imeutaka uongozi wa Mkoa wa Tabora kusimamia ufunguzi njia za muda zinazopendekezwa na wataalamu zitakazotumika kusafirisha mifugo kwenda na kutoka katika mnada wa Ipuli Manispaa ya Tabora.

Lengo ni kuwarahisisha wafanyabiashara kutekeleza majukumu yao na kuondoa migogoro baina yao na manispaa.

Agizo hilo lilitolewa jana na Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, wakati wa kikao cha majumuisho ya ziara yake ya kukutana na wadau wa sekta ya mifugo katika Manispaa ya Tabora, Halmashauri ya Wilaya ya Tabora-Uyui, viongozi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) na viongozi wa Mkoa wa Tabora.

Alisema wakati suluhisho la kudumu likitafutwa juu ya kuendelea au kutoendelea kwa mnada wa Ipuli kuwapo mahali ulipo sasa, ni vema mapendekezo yaliyotolewa na wataalamu ya kuwa na njia mpya ya kupeleka mifugo mnadani baada ya zamani kuvamiwa na kujengwa, ni vema mkoa kwa kushirikiana na wadau kuangalia uwezekano wa kutumia njia hiyo.

Ulega aliongeza kuwa ni pamoja na kuwaondoa watu wote waliopo katika njia ya mgogoro uliojitokeza kati ya wafanyabiashara wa mifugo.

Aidha, aliutaka uongozi wa Mkoa wa Tabora kwa kushirikiana na wadau wengine kuhakikisha wanaweka alama ambazo zitasaidia kuonyesha vivuko vya mifugo ambavyo vitasaidia kuepusha mifugo kugongwa na magari na wakati mwingine mifugo kukamatwa kwa kuvuka sehemu isiyo rasmi, hivyo kuwasababishia hasara wafugaji.

Naibu Waziri huyo aliutaka uongozi wa Manispaa ya Tabora kuratibu vizuri operesheni ya kuwakamata wafugaji wanaovunja sheria bila kuwaonea na kuwanyanyasa na kuongeza operesheni hiyo lazima izingatie taratibu na sheria zilizopo.

Kwa upande wa Mkuu wa Mkoa wa Tabora, Aggrey Mwanri, aliwataka wafanyabiashara wa mifugo kuendelea kufanyakazi zao kwa kuzingatia sheria zinazosimamia Manispaa ya Tabora ya kukataza mifugo kuzurura ovyo katikati ya miji.

Alisema mifugo ambayo itakutwa ikizurura katikati ya mji na maeneo ya huduma za jamii, hatua za kisheria zitachukuliwa dhidi ya mhusika.

Naye mfanyabiashara wa mifugo, Nguji Matemi, alisema kumalizika kwa mvutano kati ya wafanyabiashara na uongo umesaidia kurudisha baadhi ya wenzao ambao walikuwa wanakusudia kuachana na biashara katika eneo hilo.




Wafanyakazi wa kuzoa taka wakifanya kazi bila kutumia vifaa maalum vya kujikinga katika Soko la Kisutu, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Wananchi wajenga vyumba madarasa

**Na Sabato Kasika**

WAKAZI wa Kata ya Bukima, Musoma Vijijini mkoani Mara, wameanza ujenzi wa vyumba vya madarasa ili kuhakikisha wanafunzi wote waliochaguliwa kuanza kidato cha kwanza mwaka huu katika sekondari ya kata hiyo, wanasoma.

Kwa mujibu wa Mratibu wa Elimu wa Kata ya Bukima, Gimasa Ruyembe, wananchi hao ni wa vijiji vya Bukima, Butata na Kastam, ambao wanajitolea kusomba maji, mchanga na mawe kwa ajili ya ujenzi huo.

Ruyembe aliliambia gazeti hili kwa njia ya simu kuwa wanafunzi waliochaguliwa kuanza kidato cha kwanza Bukima Sekondari ni 187, lakini walioanza masomo ni 50 tu, kwa sababu ya uhaba wa vyumba.

"Wanafunzi 137 wanasubiri vyumba vikamilike, ili nao waanze masomo, ndio maana wananchi wanajitolea kwa hali na mali kwa ajili ya kukamilisha ujenzi ili Februari mosi mwaka huu, waanze masomo," alisema Ruyembe.

Alifafanua kuwa kwa sasa vinajengwa vyumba viwili, huku cha tatu kikifanyiwa ukarabati na kwamba hatua hiyo itasaidia kuepusha wanafunzi kukaa mitaani, hali ambayo inaweza kujiingiza katika makundi mabaya.

"Mwitikio wa wananchi kujitolea umekuwa mkubwa, kwa kuwa tulifanya mikutano mingi ya kuwahamasisha tukiwa na Mbunge Profesa Sospeter Muhongo na sasa wanajitolea ili kufanikisha ujenzi huo," alisema.

Ruyembe alisema mbunge naye amechangia mifuko 50 ya saruji kwa ajili ya kufanikisha ujenzi wa vyumba hivyo, na kwamba hakuna mwanafunzi aliyefaulu atakayeendelea kubaki nyumbani.

"Tangu Desemba mwaka jana, mbunge alikuwa huku tukishirikiana naye katika uhamasishaji wa wananchi kwa ajili ya kujitolea kuchangia miradi ya maendeleo ikiwamo elimu, kwa kweli amekuwa na mchango mkubwa kwa maendeleo ya elimu katika kata yetu, hatuna budi kumshukuru," alisema.

Alisema ujenzi wa vyumba vya madarasa unaendelea sasa, hautaishia hapo, bali utakuwa endelevu ili kuhakikisha tatizo la uhaba wa vyumba katika Sekondari ya Bukima linakuwa historia.

# Fedha gari la mkurugenzi kupelekwa katika miradi

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

MADIWANI wa Halmashauri ya Ushetu wilayani Kahama mkoani Shinyanga, wamemtaka Mkurugenzi wao Michael Matomora, kupeleka fedha za mauzo ya gari lake katika miradi ya maendeleo iliyoibuliwa na wananchi ambayo kufikia sasa bado haijakamilika.

Baadhi ya miradi ambayo imeibuliwa na wananchi bado haijakamilika pamoja na maboma ya madarasa ambayo mpaka sasa yamechangia kwa kiasi kikubwa kwa wanafunzi walifaulu kuingia kidato cha kwanza katika halmashauri hiyo kufikia 144.

Hayo yalibainika jana, katika kikao cha maalumu cha Baraza la Madiwani kichokaa kujadili na kupitisha rasimu ya bajeti ya Halmashauri ya Ushetu kwa kipindi cha mwaka 2019/2020, ambapo jumla ya Shilingi bilioni 32.6 zilipitishwa. Madiwani hao walifikia maamuzi hayo baada ya kujadili gari la mkurugenzi wa halmashauri aina Toyota Land Cruiser kuwa na matumizi makubwa ikiwamo kufanyiwa matengenezo, ambapo walisema ni bora gari liuzwe na kununuliwa jingine lenye gharama ndogo.

Diwani wa Kinamapula, Samuel Mwarabu, alisema Shilingi milioni 129.9 zilizotengwa na halmashauri kwa ajili ya kununua gari jingine ni bora fedha hizo zikaelekezwa katika ujenzi wa madarasa, ili wanafunzi waliofaulu na kukosa madarasa waanze masomo.

"Tunaomba fedha za ununuzi wa gari lingine la mkurugenzi zipunguzwe na ziende katika ukamilishwaji wa madarasa ili wanafunzi waliopo majumbani mpaka sasa waweze kuingia madarasani kwa wakati," alisema Mwarabu.

Kwa upande wake Mkurugenzi wa Halmashauri ya Ushetu, Michael Matomora, alisema gari hilo la zamani kwa sasa halina tija kwa halmashauri zaidi ya kuingiza hasara, hata Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali alipopiga mahesabu kuhusu matengenezo ya gari hilo yalikuwa yanagharimu fedha nyingi, huku halmashauri ikiwa haina mapato ya kumudu.

Naye mwakilishi kutoka Ofisi ya Katibu Tawala Mkoa wa Shinyanga, Alphonce Kasanyi, alisema ununuzi wa gari hilo jipya hauwezi kukwepeka kwa sababu usafiri huo sio wa mkurugenzi tu bali ni wa viongozi wote wa serikali.



Daktari Bingwa wa Kinamama, Dk. Geofrey Marandu, akichangia mada katika mkutano ulioandaliwa na uongozi wa Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), kwa ajili ya kujadili jinsi ya kuboresha mfumo wa kliniki ili wagonjwa wahudumiwe kwa wakati, uliofanyika hospitalini hapo, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MNH**

# Watumiaji nyama hatarini magonjwa

**Na Happy Severine,** BARIADI

WATUMIAJI wa nyama katika Halmashauri ya Mji wa Bariadi mkoani Simiyu, wako hatarini kupatwa na magonjwa ya mlipuko kutokana na machinjio ya mji huo kutozingatia usafi na usalama wa chakula.

Wakizungumza na waandishi wa habari, wachinjaji wanaofanya kazi katika machinjio hayo wameilalamikia serikali kutorekebisha miundombinu ya usafi ilhali kila siku wanalipa ushuru kwa kila mfugo unaoingizwa humo.

Aidha, wamesema kutokana na machinjio hayo kukosa umeme, wamekuwa wakifanya kazi katika mazingira magumu kwa kutumia tochi na wakati mwingine kukosa maji ya kufanyia usafi na kusafishia nyama.

"Tunalipa ushuru kwa kila mfugo, maji hayatoshi kwa ajili ya usafi na pia mazingira hayaridhishi kama mnavyoona wanahabari... tunaiomba serikali ituwekee umeme ili tufanye kazi kiurahisi," alisema Fred Dicksoni, mkazi wa Salunda.

Naye Lukuba Masalu, alisema machinjio hayo hayana nondo za kuning'inizia nyama, hali inayosababisha nyama kuwekwa chini na kusababisha kuchafuka, pia inaweza kupatwa na vimelea vya magonjwa kiurahisi.

Alisema wanalipia ushuru wa Shilingi 2,500 kwa kila ng'ombe anayeingizwa katika machinjio hayo na kuitaka serikali kuwasogezea huduma ya umeme ili wasiendelee kutumia tochi alfajiri wanapochinja nyama.

"Tunaweka nyama chini baada ya kuchinja kwa ajili ya ukaguzi badala ya kuning'iniza juu kama inavyotakiwa, pia hatuna vitendea kazi...tunaiomba serikali ituboreshee machinjio haya," alisema Daniel Nyanda.

Msimamizi wa machinjio hayo kutoka Halmashauri ya Mji wa Bariadi, Dk. Yusuph Mchengwa, alisema vyuma (nondo) kwa ajili ya kutundikia nyama zilishakatika na wanakagulia nyama chini kwa sababu ya miundombinu kuwa chakavu, ilhali vyuma vilishakatika, pia eneo hilo halina uzio.

Alisema maelekezo ya serikali yanataka nyama ikaguliwe ikiwa juu ya vyuma, pia miundombinu ya eneo hilo ilishachakaa kwa kuwa ilijengwa tangu mwaka 1974 na kilio cha wachinjaji hao walishakifikisha kwenye mamlaka husika na kwa siku wanachinja ng'ombe wanane hadi 13.

"Tumeshapeleka changamoto hizi katika mamlaka husika ili ukarabati uweze kufanyika, lakini tunatarajia kupata fedha toka mradi wa ULGSP, ili kujenga machinjio ya kisasa...ukosefu wa umeme unafanya uchunaji kutokuwa mzuri kwa sababu ya uono hafifu wa kukosa mwanga," alisema Mchengwa.

Alisema wachinjaji hao wanakwenda na tochi zao, lakini wanalipa ushuru wa Shilingi 1,500 kwa serikali ili kupata huduma hiyo, wakati huo Shilingi 1,000 ikichukuliwa na Baraza la Waislamu Tanzania kwa ajili ya ukaguzi.

Kwa mujibu wa Ofisa wa Afya wa Mkoa, Reuben Malima, alisema mfugo unapaswa kuchinjiwa chini na baada ya kuchinjwa, anatakiwa kuning'inizwa juu kwa ajili ya uchunaji na ukaguzi.

Katika machinjio hayo mnyama anachinjwa akiwa chini, anachunwa, kukaguliwa na kupigwa mhuri wa ukaguzi akiwa chini, huku wanyama kama mbwa, paka na ndege wakizunguka eneo hilo.

## Mafunzo ya urasimishaji biashara kimtandao

**Na Rose Jacob,** MWANZA

WAKALA wa usajili wa biashara na leseni (BRELA) umeanza kutoa mafunzo ya kurasimisha biashara kwa njia ya mtandao mkoani Mwanza.

Lengo ni kuhakikisha kila mwananchi anayejihusisha na biashara kupitia kampuni aweze kujisajili kwa urahisi tofauti na awali.

Msajili Mwandamizi wa BRELA kitengo cha miliki bunifu, Suzana Senso, alisema mfumo huo mpya utawarahisishia wafanyabiashara kusajili kampuni pamoja na huduma nyingine zinazotolewa na wakala huo kwa njia ya mtandao badala ya wa zamani wa kutuma nyaraka.

"Kwa sasa shughuli ya usajili inaendelea vizuri na Mkoa wa Mwanza unafanya vizuri katika kuitumia huduma ya ORS tofauti na zamani, ambapo mwombaji alikuwa anatakiwa kufika yeye mwenyewe katika ofisi zetu zilizopo Dar es Salaam," alisema Senso.

Aidha, Senso, alisema kama ombi la mteja lina upungufu atapewa maelekezo ya vitu ya kurekebisha, kisha akimaliza kufanya marekebisho atatuma tena kwa ajili ya kufanyia marekebisho.

Mafunzo hayo yanayofanyika jijini hapa, yanawashirikisha baadhi ya maofisa biashara, wakaguzi wa ndani wa mahesabu, wanasheria na wafanyabiashara kutoka halmashauri nane za mkoa huo.

Naye Kaimu Mkuu wa Idara ya kampuni na majina, Rehema Kitambi, alisema katika usajili ni lazima mteja afuate mwongozo wa kusajili kampuni kwa njia ya mtandao kupitia mfumo wa ORS ambao ni kufungua akaunti kwenye mfumo wa lazima awe na kitambulisho cha taifa, kama ni mbia kwenye kampuni ni lazima awe na kitambulisho cha taifa, kama ni mkurugenzi wa kampuni anatakiwa na kitambulisho hicho na namba ya utambulisho wa mlipa kodi (TIN) kutoka TRA.

Nao washiriki wa mafunzo hayo waliishukuru BRELA kwa kusogeza huduma karibu kwa kuweka ofisi yao mkoani Mwanza, lakini changamoto kubwa inayowakabili ni sharti la kusajili au kupata huduma kwenye mfumo wa usajili kwa njia ya mtandao na kuwa na kitambulisho cha taifa.

Walisema sharti hili bado ni changamoto kwa wateja, maana wefanyabiashara wengi hawajapata vitambulisho hivyo.

# Mradi wa TEDAP waleta uhakika wa umeme nchini

**Na Joseph Mwendapole,** ARUSHA

MRADI mkubwa wa kukarabati, kuimarisha miundombinu na mifumo ya umeme uliotekelezwa na Shirika la Umeme nchini (Tanesco), umeleta manufaa kwa kuisaidia nchi kuwa na umeme wa uhakika.

Hayo yalisemwa jana na Mhandisi Mwandamizi wa Shirika hilo anayesimamia miradi, Emmanuel Manirabona, wakati wa ziara ya waandishi waandamizi na wahariri wa vyombo vya habari wanaotembelea kuangalia maendeleo ya miradi ya shirika hilo mkoani Arusha.

Alisema kupitia mradi huo ambao kwa Kiingereza unafahamika kama Tanzania Energy Development Access and Expansion Projects (TEDAP), uliofadhiliwa na Benki ya Dunia (WB), Tanesco imeweza kuifanyia marekebisho mitambo mingi na kuweka mipya kila ilipohitajika hali ambayo imewezesha kuwa na umeme wa uhakika. Alisema hata malalamiko ya kukatikakatika kwa umeme kutoka kwa wateja yamepungua sana kutokana na kukamilika kwa mradi huo wa TEDAP, ulioanza kutekelezwa tangu mwaka 2012 na kukamilika mwaka 2017-2018.

"Hivi sasa ukienda kwenye ofisi za Tanesco huwezi tena kuona misururu ya wateja wakipeleka malalamiko au matatizo yanayohusu shirika na hii yote ni kutokana na maboresho makubwa ambayo yamefanyika na kusimika mitambo ya teknolojia ya kisasa," alisema.

Alisema shirika limefanikiwa kuweka mifumo ya kisasa ambayo kila inapotokea hitilafu huweza kuibaini mapema kabla ya wateja kwenda kulalamika na mafundi wa shirika kwenda haraka kutatua tatizo lililopo tofauti na kabla ya utekelezaji wa mradi huo.

Mhandisi Manirabona alisema Tanesco haipendi kuona mteja anakatikiwa umeme au kukosa kabisa nishati hiyo, hivyo ndiyo sababu iliamua kutekeleza mradi huo mkubwa uliohusisha ununuzi wa mitambo na mashine mbalimbali zinazotumia teknolojia ya kisasa.

Mhandisi alisema vituo vingi vya kupoozea umeme nchini vimeongezewa uwezo kupitia mradi huo na vyote vina umeme wa kutosha mahitaji na vimekuwa na njia za umeme za akiba ambazo hazijaanza kutumika.

"Ukitembelea vituo vyetu vingi utashuhudia kuna njia za umeme ambazo hazitumiki zinasubiri wateja sasa kabla ya mradi huu wa TEDAP hili halikuwezekana, limewezekana tu baada ya kukarabati na kuweka vifaa vya teknolojia ya kisasa kwenye vituo vyetu vyote," alisema.

Alisema kutokana na mabadiliko makubwa yaliyofanyika kwenye shirika hilo hivi sasa akijitokeza mwekezaji yeyote anayehitaji umeme mkubwa kwa ajili ya uzalishaji viwandani wanamuunganishia haraka.

Baadhi ya vituo vya mkoani Arusha vilivyonufaika na mradi wa TEDAP ambavyo wahariri walivitembelea jana ni pamoja na kituo cha Njiro B, Mount Meru, Kiltex, Sakina, Themi na Unga Ltd.



Meneja wa Tanesco Mkoa wa Arusha, Mhandisi Herini Mhina, akiwaonyesha jambo waandishi na wahariri wanaotembelea miradi ya umeme ya shirika hilo mkoani humo. Katikati ni Mhandisi Emmanuel Manirabona anayesimamia miradi na kushoto ni Meneja Mawasiliano wa Tanesco, Leila Muhaji. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Rasimu bil. 35.4/- bajeti ya halmashauri yapitishwa

**Na Mwandishi Wetu,** ARUSHA

BARAZA la Madiwani wa Halmashauri ya Wilaya ya Simanjiro, limepitisha rasimu ya mpango wa bajeti ya Sh. bilioni 35.4 kwa mwaka wa fedha wa 2019/20. Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Simanjiro, Yefred Myenzi, akisoma rasimu ya mpango huo wa bajeti juzi, alisema umezingatia vipaumbele sita.

Myenzi alitaja vipaumbele hivyo kuwa ni sekta ya elimu, afya, maji, utawala bora, maendeleo ya jamii, kilimo, mifugo na uvuvi.

Alisema katika rasimu hiyo ya bajeti Sh. bilioni 17.5 ni mishahara, Sh. bilioni 827.4 ni ruzuku ya uendeshaji ofisi, Sh. bilioni 16 ni miradi ya maendeleo na mapato ya ndani Sh. bilioni 1.8.

Alisema kwa vile Simanjiro ni miongoni mwa halmashauri zilizo kwenye mazingira magumu, wamewasilisha maombi maalum kwenye vipaumbele ambavyo havikutengewa fedha.

Alisema kupitia maombi hayo wanatarajia kukamilisha madarasa 42 ya shule za msingi, madarasa 77 ya sekondari na nyumba 74 za walimu na watumishi wa elimu.

Alisema wanatarajia kukamilisha zahanati sita na vituo vya afya viwili na kujenga vituo tisa vya afya na zahanati nne kwenye maeneo ya Msitu wa Tembo, Emboreet na Moipo.

"Pia tunatarajia kukamilisha jengo jipya la makao makuu ya wilaya, umaliziaji wa miradi ya maji vijijini na nyumba mbili za watumishi wa afya," alisema.

Diwani wa Kata ya Endiamtu, Philemon Oyogo, alisema wamepitisha bajeti hiyo ila serikali kuu inapaswa kufikisha fedha kwa kuwa kwenye bajeti ya mwaka jana hawakuwaletea fedha zote.

Diwani wa Kata ya Naberera, Haiyo Yamati, alipongeza bajeti hiyo ila alitarajia sekta ya mifugo kutengewa fedha nyingi zaidi. Diwani wa Kata ya Mirerani, Thomas Yohana, alisema shule mpya ya Sekondari Songambele itanufaika kupitia bajeti hiyo.

# Tanesco sasa mambo kidigitali

**Na Mwandishi Wetu,** ARUSHA

SHIRIKA la Umeme Tanzania (Tanesco), limesema kwa sasa huduma zake nyingi zinatolewa kidigitali kutokana na kukua kwa teknolojia na hivyo kwa kutumia mitambo iliyoko inawawezesha kufanya kazi zao kwa ufanisi zaidi.

Tanesco imesisitiza kuwa inatambua kazi ya kukua kwa teknolojia na hivyo nayo imeamua kujikita katika kuweka mitambo hiyo ya kisasa, ili kwenda na kasi ya ukuaji wa teknolojia katika kuhudumia wananchi na kwa sasa utendaji kazi umekuwa wa ufanisi zaidi.

Kaimu Meneja Uhusiano wa Tanesco, Leila Muhaji, amewaambia wahariri wa vyombo mbalimbali vya habari nchini waliopo kwenye ziara ya kutembelea miradi ya umeme inayotekelezwa na serikali katika Mkoa wa Arusha, amesema shirika hilo kwa sasa haliko nyuma katika kukua kwa teknolojia na hivyo mitambo mingi ambayo imefungwa kwenye vituo vya kusambaza umeme.

"Kama tulivyoona ni kwamba Tanesco tunakwenda sambamba na ukuaji wa teknolojia, vituo vyetu vingi vimekuwa vya kidigitali. Kwa hapa Arusha vituo vyetu vingi mitambo ambayo imefungwa ni ya kisasa ukilinganisha na miaka ya huko nyuma.Wataalamu wetu wakiwa ofisini kupitia mitambo iliyopo kama kuna tatizo lolote kwenye njia ya umeme kompyuta itaonyesha na hivyo inakuwa rahisi kushughulikia tatizo," amesema Muhaji.

Amefafanua: "Hivyo ikitokea gari imegonga nguzo ya umeme, mti umeegemea waya au vyovyote vile kupitia mitambo iliyopo itaonekana moja kwa moja, hii inasaidia kushughulikia matatizo mapema na hivyo kuondoa hata malalamiko kwa kuwa kabla mteja hajafika Tanesco kutoa taarifa, tayari wataalamu wetu wameshaona na kuchukua hatua."

Akizungumzia Mradi wa Kukarabati na Kuimarisha Mifumo ya Umeme Tanzania (TEDAP), Muhaji, amesema kwa Mkoa wa Arusha kupitia mradi huo wamefanya maboresho kwa kutengeneza vituo vipya, ambapo imesaidia kufanya mkoa huo kuwa na umeme wa ziada. Ameongeza kuwa kwa sasa Arusha haina tatizo la umeme na ndiyo maana wanahamasisha watu kuwekeza kwa kujenga viwanda, huku akiwahamasisha wananchi ambao wanahitaji kuunganishwa umeme kufika kwenye shirika hilo kutoa maombi yao.

Pia amesema serikali kupitia Tanesco inatekeleza miradi mbalimbali ya umeme nchini ukiwamo Mkoa wa Arusha na hivyo kuna kila sababu ya jamii kufahamu utekelezwaji wa miradi hiyo, lakini zaidi amewahamasisha wanaotaka kuwekeza kupitia sekta ya viwanda hivi sasa nchi ina nishati ya umeme wa uhakika.





# DC, mwenyekiti wa CCM wakubali kuzika tofauti zao

**Na Paul William,** MWANGA

NAIBU Katibu Mkuu wa Umoja wa Wanawake wa Chama cha Mapinduzi (UWT), Jesca Mbogo, amefanikiwa kuwaunganisha pamoja Mkuu wa Wilaya ya Mwanga, Aaron Mbogho na Mwenyekiti wa CCM wa Wilaya hiyo, Jaffary Kandege, kumaliza tofauti zao.

Kada huyo wa CCM, akiwa katika ziara yake mkoani Kilimanjaro, alikutana na viongozi hao na kuwataka kumaliza tofauti zao ili kutowapa wapinzani nafasi ya kutumia udhaifu huo kulitwaa Jimbo la Mwanga.

"Kama uhusiano wa chama na serikali katika Wilaya ya Mwanga hayatakuwa mazuri, tutawapa fursa wapinzani kuingia katika Jimbo la Mwanga, na hii ni kutokana na serikali kusema lugha yake na chama lugha yake. Ifike mahali sasa viongozi wa chama na serikali kumaliza tofauti zenu," alisema Jesca.

Aliwashangaa viongozi wa chama na serikali kwa pamoja wanajenga nyumba moja kwa kusimamia maendeleo ya wananchi kupitia ilani ya CCM kugombea fito, huku akidai kuwa hiyo ni aibu.

Baada ya kauli hiyo, Naibu Katibu Mkuu huyo, aliwataka viongozi hao wa serikali na chama kuombana msamaha na kila mmoja kukubali upungufu wake, akisisitiza kwamba huu ni wakati wa chama kufanya vizuri katika uchaguzi wa serikali za mitaa utakaofanyika baadaye mwaka huu na uchaguzi mkuu wa mwakani.

Kutokana na wito huo wa Naibu Katibu Mkuu wa UWT, Mwenyekiti wa CCM wa Wilaya hiyo, Kandege, alisema yeye yupo tayari kumsamehe na kimsingi ameshamsamehe Mkuu huyo wa Wilaya ili kuhakikisha chama kinafanya vizuri katika uchaguzi unaokuja.

Kwa upande wake, Mkuu wa Wilaya ya Mwanga, Mbogho, alisema hata yeye yupo tayari kusameheana na Kandege, lakini hakuwa na mgogoro na kiongozi yeyote wa chama, akidai kwamba anasimamia ilani ya uchaguzi.

"Uhusiano baina yangu na viongozi wa chama ni mzuri na tutaendelea kushirikiana, serikali imejipanga kuhakikisha tunawaletea wananchi maendeleo, hatuna mgogoro wowote baina yangu na Mwenyekiti wa CCM wa Wilaya," alieleza DC.



Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, akizungumza na wadau wa sekta ya mifugo na viongozi mbalimbali jana, wakati wa kikao cha majumuisho baada ya kumalizika kwa mgogoro baina ya wafanyabiashara na uongozi wa Manispaa ya Tabora, kuhusu usafirishaji wa mifugo kwenda na kutoka mnada wa Ipuli. Kushoto ni Mkuu wa Mkoa wa Tabora, Aggrey Mwanri na Mkuu wa Wilaya ya Tabora, Kitwala Komanya (kulia). **PICHA: DAUD TIGANYA**

# DC awapa moyo askari mgambo kupata ajira

**Na Godfrey Mushi,** SAME

MKUU wa Wilaya ya Same, Rosemary Staki, amewaahidi askari mgambo 108 waliofuzu mafunzo ya awali, watapewa kipaumbele katika usaili wa vijana wanaotakiwa kujiunga na Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) na wanufaika wa kwanza kwenye ajira zitakazojitokeza wilayani humo.

Alitangaza neema hiyo kwa vijana hao jana, wakati akifunga mafunzo ya jeshi la akiba wilayani humo.

"Nyie ni makamanda sasa, na nina wahakikishia kwamba mtapewa kipaumbele kwenye usaili wa JKT na ajira mkiwa na sifa. Nataka mwendelee kuushawishi umma kwa kutumia mafunzo yenu vizuri mliyoyapata kwa kujitolea kufanya kazi za jamii na kuishi kwa mfano," alisema.

Kufuzu mafunzo ya awali kwa askari hao wa akiba, kumemsukuma Mkuu huyo wa Wilaya kuagiza raia wa kawaida wasiajiriwe kwa kazi ya ulinzi, bali shughuli hiyo wapatiwe askari wa jeshi la akiba la mgambo.

Mara kadhaa, baadhi ya wakuu wa wilaya nchini wamekuwa wakitoa maelekezo kwamba askari wa akiba ndio wanaopaswa kuajiriwa kwa kazi hiyo na si raia wa kawaida anapaswa kulinda ofisi, maeneo ya biashara, taasisi binafsi pamoja na za serikali.

Staki ambaye pia ni Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama wa wilaya hiyo, amewapa morali askari hao wa akiba, akiwataka kuonyesha ukomavu wao kwa kwenda kukomesha biashara ya mirungi na vibaka katika Kijiji cha Makanya.

Vijiji ambavyo bado ni tishio kwa kuzalisha dawa za kulevya aina ya mirungi katika Wilaya ya Same ni Tae, Belle, Mmeni, Irete, Kisesa, Makasa na Vudee.

Wiki iliyopita, mkuu huyo wa wilaya alinukuliwa na Nipashe, akisema kuwa bado anatafakari hatua za kuchukua kwa wananchi waliokaidi amri ya kuharibu mashamba matano mapya ya uzalishaji wa mirungi yaliyogunduliwa katika Kijiji cha Rikweni, Kata ya Tae.

# Uhaba watumishi waikumba hospitali ya wilaya

**Na Paul William,** SAME

HOSPITALI ya Wilaya ya Same, mkoani Kilimanjaro, inakabiliwa na uhaba wa watumishi wa afya kwa asilimia 69.

Taarifa iliyotolewa na Kaimu Mganga Mkuu wa Wilaya hiyo, Dk. Taudesia Kilawe, imeeleza kuwa hali hiyo kwa sasa ni changamoto katika utoaji huduma kwa wananchi kutoka maeneo mbalimbali ya wilaya hiyo.

Dk. Kilawe alikuwa akizungumza na Naibu Katibu Mkuu wa Umoja wa Wanawake wa Chama Cha Mapinduzi (UWT), Jesca Mbogo, aliyeitembelea hospitali hiyo.

"Kimsingi hali hapa ni mbaya, tunao upungufu mkubwa wa watumishi wa idara ya afya ambao ni sawa na asilimia 69. Kazi yote inafanywa na watumishi wasiozidi asilimia 31. Kwetu hii ni mzigo mzito, tunaomba utusaidie kwa Waziri wa Afya tupate watumishi wa kujaza nafasi hizi," alieleza.

Kwa mujibu wa Dk. Kilawe, changamoto nyingine inayoikabili wilaya hiyo ni udogo wa wodi ya wazazi katika hospitali hiyo, ambayo haikidhi mahitaji ya kinamama wajawazito wanaolazwa.

Zaidi Kaimu Mganga Mkuu huyo ameeleza: "Maabara ya hospitali yetu, haina hadhi ya kuwa maabara ya wilaya, pia kuna ugumu wa jiografia ya maeneo mbalimbali ya Wilaya ya Same kufikika, hivyo kusababisha maeneo mengi kutofikiwa vyema na huduma ya afya; jambo hilo limekuwa likiathiri usimamizi na huduma za rufani."

Baada ya kupokea taarifa hiyo, Naibu Katibu Mkuu wa UWT, Jesca Mbogo, alimtaka Mkuu wa Wilaya ya Same, Rosemary Staki, kuwachukulia hatua wale wote wanaokwamisha utekelezaji wa ilani ya uchaguzi, bila kuangalia sura na cheo cha mtu.

"Zipo fedha ambazo zimeletwa na serikali na zitaendelea kuletwa katika wilaya hii ya Same kwa lengo la kuwaletea wananchi maendeleo na kutekeleza ilani ya uchaguzi, hivyo niwasihi kuhakikisha mnazisimamia ili zitumike kama zilivyokusudiwa," alisisitiza.




Ukurasa 14

Je, wajua? Magwiji 62 wamiliki nusu ya utajiri uliopo duniani




Ukurasa 19

Aliyetuhumiwa 'kuiba gari lake' anufaika fidia Sh. trilioni 2.7


# BUFE

Ijumaa Januari 25, 2019

Nipashe

BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA




## Mambo 3 ya UNESCO kuelekea maendeleo 2030

Ukurasa 15



# Uchumi wa madini Mahenge, Ulanga ulivyoangukia mtihani na mwekezaji

**Na Salome Samweli, TUDARCO,**
aliyekuwa Mahenge

UWAZI wa mikataba ya kampuni za wachimbaji wadogo na wakubwa wa madini katika kata ya Nawenge, kijiji cha Epanko, wilaya ya Ulanga mkoani Morogoro, sasa ni vita vya muda mrefu.

Hadi sasa serikali imesimamisha uchimbaji madini ya vito aina ya Rubi, yaliyopatikana kupitia wachimbaji wenye leseni kutoka Ofisi ya Madini Kanda ya Morogoro.

Hapo pamegundulika kuwapo madini aina ya graphite au kinywe au grafiti, yanayotarajiwa kuchimbwa na kampuni zilizokwishapata leseni kutoka Wizara ya Nishati, ambazo ni: Tans Graphite, Mahenge Resource na Graphite Advancement, zilizoko katika hatua za utafiti, ulipaji fidia na tathimini za mazingira.

**INAENDELEA UK.16**

UCHUMI

## Habari katika picha



Ukurasa 17

**KIUCHUMI ZAIDI** Ukurasa 19

**Umuhimu wa Muda kwenye Biashara** Ukurasa 20

Muhtasari wa Soko

**Biashara**

Jumla ya Mauzo (bln) 22,136.24

Mauzo 109,584,255.00
Hisa 58,317

**Kielezo**

| | | |
|---|---|---|
| TSI | 4,207.58 | +0.00 |
| DSEI | 2,296.50 | -37.11 |

**ZILIZOPANDA**

| KAMPUNI | Bei | Badiliko% |
|---|---|---|
| KA | 180 | -2.70% |
| JHL | 9,500 | +1.06% |
| SWIS | 3,760 | +7.43% |
| EABL | 5,320 | -1.66% |

**ZILIZOSHUKA**

| KAMPUNI | Bei | Badiliko% |
|---|---|---|
| TCCL | 1,200 | -11.76% |
| ACA | 5,550 | -2.63% |
| NMB | 1400 | -1.41% |
| NMG | 2,510 | -1.57% |
| KCB | 840 | +2.44% |

UCHUMI

# Je, wajua? Magwiji 62 wa nusu ya utajiri uliopo du

• Maskini wazidi 'kuchoka' kila kukicha

**Na Mwandishi Wetu**

KUNA wakati inaweza kuwa ngumu kuamini, lakini ndio ukweli ulivyo. Takwimu na ripoti za kimataifa zinaonyesha, kuna wastani wa matajiri 62 duniani hivi sasa, ndio wanamiliki zaidi ya nusu ya mali za watu wote wa duniani.

Wakati wadau wa dunia wanakutana jijini Davos Uswisi, kuhudhuria Mkutano wa Kiuchumi Duniani - World Economic Forum (WEF), huko Davos, Uswisi, Shirika la Hisani la Oxfam linadokeza kupitia ripoti yake.

Kwa mujibu wa shirika la Oxfam, utajiri wa watu hao 62 hivi sasa umeongezeka kwa asilimia 44, kulinganisha na ilivyokuwa mwaka 2010.

Vivyo hivyo, katika upande wa pili, kuna kundi la watu maskini wapatao bilioni 3.5, milki zao za mali zimeshuka kwa asilimia 41.

Ripoti hiyo iliyopewa kichwa cha habari "Uchumi wa Asilimia Moja," inabainisha kuwa wanawake wanaathirika zaidi na ukosefu wa usawa duniani.

Takriban nusu ya matajiri zaidi wa dunia wanatokea nchini Marekani na wengine 17 wanatoka barani Ulaya, ambako kunapatikana Umoja wa Ulaya (EU).

Kwa mujibu wa ripoti hiyo, waliosalia ndio wanatoka katika mataifa ya China, Brazil, Mexico, Japan na Saudi Arabia.

**KWANINI HIVYO?**

Moja ya mambo muhimu yaliyoainishwa katika ripoti ya Oxfam, kuelezwa yanachangia ukosefu wa usawa duniani, ni kupungua kwa mgawo wa pato la taifa linalokwenda kwa wafanyakazi karibu katika mataifa yote yaliyoendelea na yanayoendelea.

Ripoti inafafanua kuwa, sehemu kubwa ya kada ya wafanyakazi wanaolipwa kiasi kidogo zaidi cha mshahara ni wanawake.

**MATAJIRI VS WASIO NACHO**

Ingawa viongozi wa dunia wamezidi kuzungumzia haja ya




Wanaharakati wa Oxfam, wakiandamana kupinga ukosefu wa usawa wa kiuchumi.

**"Hili linazinyima serikali rasilimali muhimu zinazohitajika kupambana na umaskini na ukosefu wa usawa.**



Wanaharakati wa Oxfam wakiwa wameva vikaragosi vya baadhi ya viongozi wa dunia washiriki mkutano

UCHUMI

**Uchumi wa madini Mahenge, Ulanga ulivyoangukia mtihani na mwekezaji**

Ukurasa 16

UCHUMI

**Mambo 3 ya UNESCO kuelekea maendeleo 2030**

Ukurasa 15

BIASHARA

**Aliyetuhumiwa 'kuiba gari lake' anufaika fidia Sh. trilioni 2.7**

Ukurasa 19

# amiliki
# niani





wa WEF.



Muasisi wa mkutano wa WEF, Klaus Schwab, kutoka nchini Ujerumani. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

kukabiliana na ukosefu wa usawa, Oxfam inasema pengo kati ya matajiri zaidi na wengine limetanuka zaidi katika kipindi cha miezi 12 iliyopita.

Utabiri wa Oxfam uliotolewa siku moja kabla ua mkutano wa Davos wa mwaka jana, ni kwamba asilimia moja ya matajiri zaidi wa dunia, ndio watamiliki zaidi ya asilimia 99 ya mali dhidi ya waliobaki, ndani ya muda mfupi ujao inaelezwa imeshatimia.

Wakati idadi ya watu wanaoishi katika hali ya umaskini uliyokithiri, ilipingua kwa asilimia 50 kati ya mwaka 1990 na 2010, wastani wa kipato cha asilimia 10 ya watu maskini zaidi duniani kimeongezeka.

Nyongeza hiyo inatajwa ni chini ya dola tatu katika kipindi cha mwaka jana, ambayo kwa sasa ni sawa na chini ya Sh.7,000.

Maandiliko hayo yanaelezwa kuwa hafifu zaidi, kutokana na ukweli kwamba katika kipindi cha robo karne iliyopita, ilikuwa ongezeko la chini ya senti moja (chini ya Sh. 300), katika kipato cha mtu mmoja mmoja kwa mwaka.

Zaidi ya wakuu 40 wa nchi na serikali wanahudhuria mkutano huo wa Davos ulioanza Jumanne jioni wiki hii na unamalizika leo.

Taarifa ya awali iliyotolewa na waandaji wa mkutano huo wa uchumi duniani, ilisema mkutano huo wa ngazi ya juu ulifanyika katika eneo la mapumziko la Davos nchini Uswisi na kushirikisha pia viongozi wapatao 2,500 wa kibiashara na kijamii.

**MAPINDUZI YA VIWANDA**

Akifafanua kuhusu kaulimbiu ya mwaka huu, isemayo 'Mapinduzi ya nne ya viwanda," muasisi wa WEF, Klaus Schwab, anasema inamaanisha kuunganisha teknolojia katika ulimwengu wa kimaumbile, kidigitali na kibaiolojia, kwa kuanzisha uwezo mpya unaoathiri mifumo ya kisiasa, kijamii na kiuchumi.

Mkurugenzi Mkuu wa Oxfam, Winnie Byanyima, ambaye ni mhudhuriaji wa mkutano huo wa Davos baada ya kuwa Mwenyekiti Mwenza wa Mkutano wa Mwaka uliopita, anasema uwiano huo wa miliki ya mali kati ya maskini na matajiri kuwa na miliki maradufu katika kiwango kinachotisha, haukubaliki.

**UTAJIRI WA AFRIKA NJE**

Ikiweka katika nafasi ya kipaumbele, Oxfam inataka kukomeshwa kwa zama za maeneo salama ya kodi, ambayo yameshuhudia ongezeko la matumizi ya vituo vya nje kukwepa kulipa kodi.

"Hili linazinyima serikali rasilimali muhimu zinazohitajika kupambana na umaskini na ukosefu wa usawa," inasema ripoti hiyo.

Inakadiriwa, asimilia 30 ya utajiri wa fedha wa Afrika, unashikiliwa nje ya bara hilo na ripoti hiyo inafafanua kuwa hilo litaigharimu bara hilo dola bilioni 14 katika mapato yanayopotezwa kila mwaka.

Ili kufikia viwango sahihi vya kodi, kutakuwapo umuhimu wa viongozi wa dunia kufikia malengo yao waliojiwekea mwaka uliopita, ya kufuta kabisa umaskini uliokithiri ifikapo mwaka 2030.

Byanyima anawapa changamoto washiriki wa mkutano wa Davos, kwamba watoe mchango wao katika kukomesha 'enzi ya maeneo' ya kodi ambayo yanachochea ukosefu wa usawa wa kiuchumi na kuwazuia mamia ya mamilioni ya watu kujiondoa katika umaskini.

Miongoni mwa watu 62 wanaosemekana kumiliki utajiri sawa

**INAENDELEA UK.20**

SIKU YA ELIMU DUNIANI:

## Mambo 3 ya UNESCO kuelekea maendeleo 2030

JANA Januari 24 ilikuwa Siku ya Kimataifa ya Elimu Duniani, ambayo inaadhimishwa kwa mara ya kwanza tangu kupitishwa na Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa mwezi Desemba mwaka jana. Na hiyo ni kwa kutambua umuhimu wa elimu katika kubadili dunia na kufikia ajenda ya 2030 ya maendeleo endelevu.

Siku ya elimu duniani, UNESCO imesema mwamko katika ushirikiano kimataifa wahitajika kufanikisha SDG4 (malengo ya maeneleo endelevu).

Katika ujumbe wake kwa siku ya jana, Mkurugenzi Mkuu wa shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni, UNESCO, Audrey Azoulay, amesema bila elimu jumuishi na sawa na fursa za kudumu kwa wote, nchi hazitafanikiwa kuvunja mzunguko wa umaskini ambao unawaacha nyuma mamilioni ya watoto, vijana na watu wazima.

Bi. Azoulay amesema, "hatutaweza kupata mafanikio katika kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi, kuendana na mabadiliko ya teknolojia na kufikia usawa wa kijinsia bila dhamira ya kisiasa kuhusu elimu kwa wote."

Akaongeza kuwa, "siku hii Januari 24, ni muhimu katika kusisitiza mambo muhimu, mosi, elimu ni haki ya binadamu, jambo nzuri kwa umma na wajibu wa umma.

Pili, elimu ni moja ya nguvu iliyopo mikononi mwetu kuhakikisha huduma za afya, kuimarisha ukuaji wa kiuchumi, kuzindua uwezo na ubunifu tunaohitaji kwa ajili ya kujenga jamii zilizo na stahamala zaidi na endelevu. Mwisho, tunahitaji kutoa wito kwa pamoja kwa ajili ya kuchukua hatua kimataifa.

Takwimu zinaonyesha changamoto zilizopo kwani watoto milioni 262 ya vijana hawahudhurii shule; watoto milioni 617 na barubaru hawawezi kusoma au kufanya hesabu rahisi, ambapo chini ya asilimia 40 ya watoto wa kike waliopo kusini mwa jangwa la Sahara ndio wanahitimu elimu ya sekondari huku watoto milioni 4 na barubaru wakimbizi hawahudhurii shule kwa sababu ya mizozo. Mkurugenzi mkuu huyo amesema, "kwa sababu dunia haipo katika njia sahihi kufikia lengo namba nne la malengo ya maendeleo endelevu, SDGs, tunahitaji mwamko katika ushirikiano kimataifa na hatua za pamoja.

Changamoto yetu ni kuhakikisha kuwa elimu inamfaa kila mmoja kwa kuchagiza ujumuishwaji na usawa katika kila nyanja, kuhakikisha hakuna anayeachwa nyuma".

Kwa mantiki hiyo, ameongeza kuwa, hali hii inamaanisha kuweka juhudi mahsusi kulenga watoto wa kike, wahamiaji watu waliofurushwa na wakimbizi; kuwasaidia walimu na kuhakikisha elimu na mafunzo vinazingatia jinsia.

UNESCO imetoa wito kwa serikali kuweka elimu kama kipaumbele kwa kusema, "sisi sote ni washikadau kwenye elimu, hebu tuchukue hatua pamoja kufikia malengo". **UN**



Watoto wakimbizi nchini Nigeria, wakiwa darasani. **PICHA: MTANDAO.**

BEI YA MAZAO >> MCHELE 174791.67/- | ULEZI 143809.52/- FEDHA >> RAND 167.40 | KSH 22.54 | USH 0.62

UCHUMI

# Uchumi wa madini Mahenge, Ulanga ulivyoangukia mtihani na mwekezaji

• Halmashauri yalalama kutoambulia kitu • Wakatoliki na 'mgomo baridi' ekari zao 100
• Waziri asimamisha vyote kusaka majibu • Mlalamikiwa ataja mbadala uliojaa neema

Inatoka Uk.13



Sehemu ya mji wa Mahenge. **PICHA ZOTE: SALOME SAMWELI, TUDARCO.**

### HALMASHAURI HAZIJAAMBULIA

Madini inatajwa kuwa chanzo cha mapato cha Halmashauri ya Wilaya Mahenge, asilimia 0.3, lakini tangu halmashauri hiyo kuanzishwa mwaka 1984, haijawahi kupata fedha itokanayo na uchimbaji madini kwenye eneo lake.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya Ulanga, Yusuph Semunguka, anasema wilaya ya Ulanga iko umbali wa kilomita 312 kutoka Morogoro Mjini, ikiwa na akiba ya madini; dhahabu, rubi, spino, gameti na ghaphite.

"Wachimbaji wengi ni wadogowadogo ambao wamepewa leseni ya Ofisi ya Madini Kanda, lakini halmashauri haijawahi kupata hata senti moja.

"Tuna eneo la Epanko ambako kumegundulika madini ya graphite ambao wako kwenye hatua nzuri za kuanza kuchimba," anasema Mkurugenzi.

Anasema, matarajio ya kampuni na wachimbaji wengine, ni kwamba iwapo halmashauri itaingia nao mkataba wa kupata malipo ya asilimia 0.3 ya mapato yao, pia wananchi watapata ajira ya kudumu na muda mfupi.

Semenguka anasema, kampuni hiyo ilitakiwa kuanza kazi mwaka jana, lakini imekwamishwa na ukamilishaji fidia, hivyo utaanza mwaka huu.

"Asilimia 95 ya vyanzo vya mapato ya halmashauri yetu ni kilimo hasa cha mpunga, mahindi, uvunaji wa mbao, minada na uvuvi, anafafanua.

"Kwa mwaka 2017/18, tulishika nafasi ya 13 kwa makusanyo, tulikusanya Sh. bilioni 3.1 sawa a asilimia 86 na mwaka 2018/19 tunatarajia kukusanya Sh. bilioni 3.2," anafafanua.

### MWENYEKITI ULANGA

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya Ulanga, Furaha Lilongile, anasema tangu mwaka 2012, ni kampuni nne tu zilizoonyesha nia ya kuchimba graphite na walitakiwa kulipa fidia kabla ya kuanza kazi.

"Toka uchimbaji uanze halmashauri haijawahi kupata fedha yoyote. Hii ni kutokana na ukweli kuwa, wanapewa leseni na wizara (Madini), nasi tunapata ushuru, lakini imekuwa vigumu kutokana na kwamba sasa kuna wachimbaji wadogo wadogo ambao hawajulikani wanapata kiasi gani," anasema Lilongile.

> "
> **Wachimbaji wengi ni wadogowadogo ambao wamepewa leseni ya Ofisi ya Madini Kanda, lakini halmashauri haijawahi kupata hata senti moja.**



Nyumba ya mkazi ya kijiji cha Epanko, iliyoko Ulanga, katika wilaya ya Mahenge. Mkazi huyo bado hajapatiwa fidia.

Mwaka jana, mwenyekiti huyo aliiambia Nipashe kwamba kuna kampuni ilifanya tahimini, lakini hakuna malipo ya fidia yaliyofanyika na imeshapita mwaka mmoja sasa, hata walipoulizwa walijibu wanasubiri mazungumzo na serikali, baada ya marekebisho ya Sheria ya Madini.

Mwenyekiti anafafanua: "Tunachojua ni kuwa, baada ya muda wa kisheria kupita, watatakiwa kufanya thathimini tena na hali ilivyo wanatakiwa kufanya tathmini upya."

### WADAU MADINI

Aliyekuwa Naibu Waziri wa Madini, ambaye kwa sasa ni Waziri, Doto Biteko, mwaka jana alisitisha uchimbaji madini na akawaagiza wachimbaji wote kupeleka taarifa zao, huku akiunda kamati ya kuchunguza suala hilo.

"Wapo wachimbaji wanapata hadi Sh. milioni 900, lakini hawalipi kodi yoyote au wanalipa pungufu na halmashauri tunabaki kusikia kuwa mchimbaji alipata kiasi fulani.

"Mzunguko wa fedha Ulanga kwa sasa unategemea mishahara ya watumishi, yaani mwisho wa mwezi na baada ya hapo hakuna kitu," anasema Lilongile.

Anasema matarajio ni kuwa timu ya wataalamu itatoa mwelekeo utakaowarejesha wachimbaji wadogo na halmashauri kupata stahiki yake ya asilimia katika pato la madini, ambayo ni asilimia 0.3.

Ofisa Ardhi na Maliasili wa Wilaya ya Ulanga, Haruni Valency, anasema kampuni hiyo ilipewa leseni ya utafiti mwaka 2012 na mwaka 2015 kwa ajili ya uchimbaji.

"Kaya 347 ziko ndani ya eneo la mradi na zimefanyiwa tathimini. Kati yake kaya 62 zimekataa kufanyiwa na wamefungua kesi kupinga kuondolewa," anasema.

Sheria ya madini na sheria ya ardhi zimetaja madini na gesi ni mali ya umma na mwekezaji hatakiwi kuanza kuchimba chochote hadi awe amelipa stahiki za wakazi wa eneo husika.

Anasema, kampuni hiyo inaendelea kushirikiana na jamii katika ulipaji wa fidia na ziliundwa kamati mbalimbali za ufuatiliaji ambazo ni kamati ya ardhi mbadala, kamati ya mila na desturi, kamati ya huduma za kijamii na kamati ya fidia na mambo mbalimbali.

Kuhusu muundo wa kamati hizo zina uwakilishi wa wananchi kutoka kila kitongoji, lengo ni kupata uwanja mpana wa ushirikishaji wananchi.

Ofisa ardhi huyo, anasema malengo ni kutafuta ardhi mbadala ya wananchi kuhamia na ilipendekezwa katika kitongoji cha Mbela, katika kijiji cha Epanko, ambako kutakuwapo mpango wa matumizi bora ya ardhi.

"Kaya 350 zitajengewa nyumba, huduma za kijamii kama kanisa, hospitali. Pia, kampuni itajenga shule mpya yenye madarasa 14, nyumba 13 za walimu, matundu 16 ya vyoo, ofisi ya kijiji na kumalizia ujenzi wa Kituo cha Afya ambacho awali kilikuwa ni zahanati.

"Pia, watajenga jengo la Chekechea katika kitongoji cha Loli, ili kupunguza umbali kwa wanafunzi wadogo, watajenga daraja linalounganisha Epanko na Kisewe, ikiwamo kuboresha miundombinu ya Shule ya Msingi Kisewe."

Kwa mujibu wa Valency, kuna makubaliano maalum yanayoandaliwa, yatakayohusisha usimamizi na ufuatiliaji.

Anataja mengine ni kampuni kuwapa chakula cha miaka miwili wananchi waliohamishwa, mbolea, mafunzo ya kilimo na kuanzisha miradi ya maendeleo.

"Baada ya tathimini tumebaini asilimia 98 wamekubali kujengewa nyumba ya kisasa ambayo ni vyumba vitatu vya kulala, sebule, jiko na choo, na kwamba hadi sasa asilimia mbili watapewa fedha," anasema.

### KWANINI KUCHELEWA?

Valency anasema, kinachoshelewesha ujenzi ni migogoro baina ya wananchi, baadhi hawapo tayari kufidiwa.

Meneja Uhusiano wa Tans Graphite, Benard Mihayo, anasema kampuni yake iko kwenye mazungumzo na serikali na inasubiri mabadiliko ya sheria, baada ya hapo wataendelea na uwekezaji.

Anadokeza kuna vitongoji sita vilivyopo kwenye mpango wa kupewa fidia na watahakikisha kila mwananchi anajengewa nyumba na kupatiwa huduma zote za kijamii.

"Tulipata leseni mwaka 2015 na mwaka 2016 tukapata Cheti cha Tathimini ya Athari za Mazingira. Tuliunda Kamati ya Nyumba Mbadala, ikiwa na wajumbe kutoka vitongoji vyote, mbunge, Mkuu wa Wilaya, Mkurugenzi wa Halmashauri, Kanisa Katoliki, Mwanasheria, Katibu Tawala, Ofisa Madini na mwanasheria wa wananchi. Imeshafanya vikao tisa na vimebaki vikao viwili vya kuthathimini fidia," anabainisha.

Mihayo anasema changamoto kubwa ni kwa familia zilizokataa fidia, akifafanua: "Sheria inatutaka kama kuna watu wamegoma tunajulisha Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi inafanya tathimini ya lazima na kisha inalipwa fidia."

Mihayo anasema, kampuni ilitakiwa kuanza kulipa fidia Novemba 2017 hadi Februari 2018 kwa kaya 347, asilimia 82 wamekubali, lakini baada ya kukamilika taratibu mbalimbali tutaanza kuwalipa," anasema.

Aidha, anasema itawekezwa mtaji wa Sh. bilioni 3.7, Sh.bilioni mbili zikiingizwa katika ujenzi wa makazi, kutekeleza makubaliano ya kuwapa chakula, pembejeo, mafunzo ya kilimo kwa miaka miwili.

"Kwenye eneo la kanisa la ekari 100 kuna wananchi walivamia nao tumewaweka kwenye fidia na kanisa tunalilipa fidia bila kujali waliovamia, lakini bado kuna uzito katika kuamua," anasema.

Mihayo anasema mwaka huu kuna mpango wa ujenzi wa: Nyumba 350 na kuwekewa umeme wa jua; Shule ya Epanko yenye madarasa 14 ikiwamo chekechea kuhudumia wanafunzi 332; kituo cha afya na nyumba tatu za wafanyakazi,pia ofisi ya kijiji na barabara ya Isungu kwa kiwango cha changarawe.

### KANISA LINASEMAJE?

Askofu wa Kanisa Katoliki Jimbo la Mahenge, Agapiti Ndorobo, anasema madini ya jimbo la Mahenge yana faida kwa wakazi wake, iwapo yatatumiwa kuwanufaisha; Mahenge na Ulanga.

"Ni jukumu letu kuona tunapofikiwa na watu wa madini kuna mapatano mawili kwamba anakubali tuwe wabia au anatufidia katika hali inayostahili na thamani ya mahali," anasema na kuongeza:

"Anapokuwa anatufidia, lazima apange muda kama ambavyo sisi tuna mipango katika maisha, kwamba katika miaka mitano kuna programu fulani na kama anatusimamisha tusifanye lolote katika

INAENDELEA UK.18

# Biashara katika picha



Meneja wa Benki ya Afrika Tanzania Tawi la Kahama, Bernadetha Mdendemi (kulia), akikabidhi shilingi milioni moja kwa Aslam Said (kushoto), aliyeibuka mshindi katika droo ya kampeni ya 'Hamia Kwetu' inayendeshwa na benki hiyo. **NA MPIGAPICHA WETU**



Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji, Jumaa Aweso, akichagua embe katika eneo la Masaki wilaya ya Kisarawe mkoani Pwani, embe moja uuza kwa shilingi 200 mpaka 500. **PICHA: HALIMA KAMBI**



Mfanyabiashara wa viatu akimuonyesha mteja wake katika eneo la Posta jijini Dar es Salaam jana. **NA MPIGAPICHA WETU**

BEI YA MAZAO >> MAHINDI 50740.00/-| MAHARAGE 175208.33/-

UCHUMI

# Uchumi wa madini Mahenge, Ulanga ulivyoangukia mtihani na mwekezaji




Makao Makuu ya Halmashauri ya Wilaya Ulanga.

INATOKA UK.18

maeneo yetu, ni lazima alipe au atuache tuwe huru tufanye kazi zetu"

Askofu huyo anasema Kanisa Katoliki linamiliki kisheria ekari 100 tangu mwaka 1921 katika kata ya Epanko, zenye nyumba ya katekista, shule ya msingi, Kanina na huduma nyingine za kijamii.

Anasema wawekezaji wanaokuja kwenye maeneo hayo, wanaanzia juu na kumaliza kila kitu, bila ya kushirikisha jamii husika, inayowekwa ya mwisho na si vyema mwekezaji kufika na kauli ya bei ya fidia.

"Maeneo haya yanatufanya tupate chakula na mji wa Mahenge ulikuwa unapata maharage, kabeji, miwa kutoka Epanko.

"Unapofika unamwambia mtu 'ondoka' lazima uangalie mazingira yake yote, imepita miaka mitano toka mchakato wa kutaka kuwaondoa wananchi," anasema.

Askofu Ndorobo anasema, hivi sasa chakula kimepanda bei, huku akitoa mfano wa maharage kupanda hadi Sh. 2,000 kwa kilo, ambayo wananchi wengi hawamudu.

"Kanisa linamiliki ekari 100 ambazo sehemu yake inatumika kama shamba la ng'ombe, eneo letu tuna mipango ya muda mrefu. Lakini, walipokuja wakagundua madini tunakubaliana nao lakini watueleze kwa uwazi watafidia kiasi gani," anasema na kuongeza:

### KAMPUNI HIZO HAPA NCHINI NI KINA NANI?

Askofu huyo anasema hadi sasa hakuna uwazi wa kujua kampuni hizo na nyingine ni za wapi, wanahisa wake wa nje na ndani na mikataba yao lilivyo.

> "Kanisa lina programu zake za muda mrefu na tunafikisha miaka 102 toka kanisa limiliki eneo hilo, leo unataka lihamishwe au lidhurike kwa namna yoyote ile lazima kila mmoja atafakari.

"Hadi sasa tunachojua kampuni zinakuja kuchimba madini ya Ghraphite, hawajajitambulisha vizuri ili tuwajue wamiliki wa ndani ya nchi bali tunasikia ni ya Australia," anasema.

Anasema hadi sasa kampuni ya Kibaran inayomiliki kampuni ya Tans Graphate na Mahenge Resource wameongea na kanisa hilo, lakini hawajasema kanisa itafidia kiasi gani, na kwamba ndiyo maana Kanisa linataka wafuate taratibu na kuwapo uwazi.

"Kanisa lina programu zake za muda mrefu na tunafikisha miaka 102 toka kanisa limiliki eneo hilo, leo unataka lihamishwe au lidhurike kwa namna yoyote ile lazima kila mmoja atafakari," anasisitiza.

Aidha, anasema wanachojua madini yapo mengi, huku akitetea hoja yake kwa kurejea kauli ya Mwalimu Julius Nyerere kuhusu kutahmini madini. Askofu Ndorobo, analalamika kwamba kila wanapohoji kuwapo madini mengine katika uchimbaji, kampuni hizo zinakataa. Anaendelea:

"Graphite haiwezi kuwapo bila madini mengine na hakuna anayejibu swali hilo zaidi ya kutaka kupata ardhi hiyo."

### UWAZI WA MIKATABA

Askofu Ndorobo anasema, kuna uhitaji wa wananchi wa eneo husika washirikishwe kwenye mkataba wajue wanavyonufaika:

"Siyo mtu anakuja kwako anakwambia ameshapewa leseni na nyie hamna haki, Je serikali ya eneo husika iliposhirikishwa ilisema nini? Mwenyekiti wa kijiji hana upeo mkubwa lazima aulize anaowaongoza," anasema na kuongeza:

"Ni jukumu la serikali kuona maisha ya baadaye ya wananchi wake, vinginevyo wanaweza kubaki kuwa wahamaji katika mkoa au wilaya yao.".

Pia, anampongeza Rais Dk. John Magufuli, kwa kuingilia kuchukua hatua katika sekta ya madini, Askofu Ndorobo anaongeza:

"Jimbo la Mahenge lina sehemu nyingi sana zenye madini ya aina mbalimbali. Kwa kuendelea kuruhusu watu kuhamishwa bila utaratibu endelevu, watu wetu hawatatulia.

"Kanisa linajiuliza tunajenga kanisa la aina gani kwa kuwa hatuwezi kujenga kama la mwaka 1921, ni mambo ya kichungaji na huwezi kumpa Mlei yeyote.

"Ndiyo maana tunataka kujua wanatuhamisha lini? Wanatufidiaje na mikataba ikoje? Lazima kuwe na mpango na siyo suala la kusema 'ondoka.' Kila mtu ana mpango wake kuwa hadi wakati huu nitakuwa nimefanya hiki na kile."

Askofu analalamika kwamba umaskini ni mkubwa licha ya Mahenge na Ulanga kuwa tajiri wa ardhi inayovuna mengi, ana anahimiza elimu kwa wananchi kupewa mikataba inayoacha faida kwa jamii.

### MTAALAMU MIAMBA

Mtaalamu wa miamba kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Profesa Hudson Nkotagu, anasema madini ya graphite, yanapatikana katika ukanda unaoitwa 'Mozambican belt'kuanzia Ethiopia, pia Afrika Mashariki; Kenya, Msumbiji na Tanzania.

"Mara nyingi ukanda huo una miamba yenye umri wa zaidi ya miaka bilioni 1.2 'metamophic' ambazo zina joto la chini, kati na juu sana. Miamba ambayo imetengezwa kwenye joto la chini ndiyo inaweza kuwa na hiyo miamba yenye madini ya graphite ambayo ni kama viumbe hai kama mimea ambayo hupikwa kwenye joto la chini na kutengeneza madini hayo," anasema.

Anasema nchini, madini hayo yapo Mirerani mkoa Arusha, Mahenge, Morogoro na Ngachu mkoa wa Lindi, ikifahamika kama ukanda wa Usagarani.

Profesa Nkotagu, anasema ni magumu zaidi ya malighafi duniani, mara 200 ya chuma cha pua.

"Hiyo sifa inayafanya yaweze kutumika kwenye vitu vingi kama kutengeneza madaraja, bodi za ndege, gari, kofia za pikipiki na vitu vingine vigumu vigumu. Pia yanaweza kuvutika sana kwa asilimia 20 hadi 25 ya urefu wake," anafafanua.

Anataja sifa nyigine ni kwamba nyembamba, mepesi sana kuliko unyoya wa kuku, uwezo wa kusafirisha joto kuliko vitu vingi na kusafirisha umeme, kuliko nyaya za shaba, inayofanya itumiwe zaidi.

"Ndiyo maana wanatumia kwenye ndege, maana kwenye ndege kunahitaji vitu kama hivyo," anafafanua mtaaluma huyo.

Sifa nyingine ni uwezo wa kuchuja maji na kuondoa madini mengine yote, hivyo inatumika kuchuja maji ya bahari hata kupata maji ya kunywa.

"Madini hayo yanatengeneza betri za magari na magari aina ya Volkswagen na Mecedeze Benz na BMW. Nchini wanataka katika miaka 2020 hadi 2025, asilimia 25 ya magari wanayotengenezwa duniani yawe ya umeme kwa kutumia graphite," anafafanua.

Kwa mujibu wa mtaalamu huyo, kupunguza hewa ya ukaa, mataifa mengi yameanza kutengeza gari la umeme ambalo litawashwa kwa umeme na ili lifanye kazi vizuri, graphite ina uwezo wa kupitisha na kuhifadhi umeme kwa muda mrefu.

Anajata sifa nyingine ni kutumika kutengenezea breki za magari na viwandani, kwa ajili ya vilainishi mbalimbali na ina soko kubwa duniani.

Profesa Nkotagu, anasema nchi inayoongoza kwa kuwa na madini hayo duniani ni Uturiki, mwaka 2017 ilikuwa na tani milioni 90; Brazili tani milioni 70; China milioni 55; huku Tanzania na Msumbiji zikiwa na tani milioni 17.

**FEDHA >>** USD 2294.16| Pauni 2952.13| Euro 2615.11

# Aliyetuhumiwa ‘kuiba gari lake’ anufaika fidia Sh. trilioni 2.7

**Na Mwandishi Wetu**



Lawrance Crosby, akiwa mikono juu chini ya ulinzi wa Polisi, mwaka 2015. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

MMAREKANI mweusi, Lawrence Crosby, aliyetiwa nguvuni na polisi jijini Illinois, Chicago, Marekani akidaiwa kuiba gari, sasa ‘ameibadilishia kibao’ mamlaka za umna ziliomchukulia hatua, baada ya kugundulika ni mali yake.

Hiyo ni baada ya gari alilodaiwa kuliiba zaidi ya miaka mitatu iliyopita, kugundulika ni mali yake na amesingiziwa na Polisi, pia mamlaka za umma.

Sasa kilichofanyika, ni kwamba amefikia makubaliano nje ya mahakama alipwe fidia ya thamani ya fedha inayofikia Sh. Trilioni 2.7, mlipaji akiwa mamlaka za jiji hilo.

Wakati sakata hilo lilitokea mwaka 2015, Lawrence Crosby, alikuwa mwanafunzi wa Shahada ya Uzamivu (PhD) katika Chuo Kikuu cha Northwestern, akiwa na umri wa miaka 25.

Mkata ulianza pale mwanamke mmoja alipiga simu polisi wakati Crosby, alipokuwa akirekebisha gari yake, akimtuhumu ni mwizi anayejaribu kuliiba.

Mzigo huo sasa unaiangukia Mamlaka ya Mji wa Evanston, ambayo walalamikaji katika kesi hiyo wanajadili kama wataridhia malipo hayo kama yalivyodaiwa na wakili wa Crosby au la.

Timothy Touhy, ambaye ni wakili wa Dk, Crosby, ndiye aliwakilisha kiwango cha madai hayo ya mteja wake na wakili huyo anaeleza hilo kuwa ni tukio ubaguzi wa rangi na itasaidia kukabili, kama si kukomesha kabisa tabia hiyo.

Mwanasheria wa jiji, amenukuliwa akieleza msimamo wa upande wake kwamba: “Ni kielelezo tu cha nia njema na si kukubali tuhuma.”

Anakiri mlalamikaji alikuwa anarekebisha gari lake na ndipo mwanamke aliyemdhania anaiiba, alipiga simu kuifahamisha Polisi jinai aliyoihisi.

Inaelezwa, mwanamama huyo aliendelea kumfuatilia Crosby alipowasha gari kuelekea kwenye makazi yake chuoni, kisha akawapigia simu polisi, ambao nao mara moja walichukua hatua ya kumfuatilia na kumkamata mara moja.

Baada ya Dk. Crosby kusimamishwa na polisi, alitoka kwenye gari akiwa mikono juu, analalamika kwamba polisi walimvamia.

Polisi wanadai hakulala chali mara baada ya kuamriwa kufanya hiyo na ndio maana wakatumia nguvu zaidi.

Crosby alidai katika hatua iliyofuata alipiugwa makonde na mateke zaidi ya 10 na ndipo akatiwa mbaroni, katika tukio linaloelezwa na kamera ya polisi ilizinasa tukio zima.

Hata hivyo, baada ya uchunguzi wa maofisa wa polisi, waligundua alimiliki kihalali gari hilo, lakini wakaendelea kumshikilia kwa jingine la kugoma kukamatwa, jambo ambalo mlalamikjai analipinga.

> Mkanda uliorekodiwa, ulionyesha Crosby, alimfahamisha kupitia simu yake ya mkononi akiwa ndani ya gari, akimwambia anafuatiliwa.

Msemaji wa Polisi katika eneo hilo, alitetea matumizi ya nguvu kwenye tukio hilo, akidai awali walidhani ilikuwa kesi ya wizi wa gari.

Dk, Crosby aliachiwa huru na kufutiwa mashtaka yote, hata hivyo, katika mkono wa pili wa shilingi mtuhumiwa huyo, hakukubaliana na alichofanyiwa na alifungua mashtaka dhidi ya jiji husika na polisi.

Kwa mujibu wa televisheni za nchini, Crosby, alisikika alijieleza kwa polisi kwamba alikuwa anajaribu kujieleza kwamba aliinama kwa ajili ya matengenezo ya gari lake.

Mkanda uliorekodiwa, ulionyesha Crosby, alimfahamisha kupitia simu yake ya mkononi akiwa ndani ya gari, akimwambia anafuatiliwa.

Katika maelezo yake ya kisheria, Crosby anajieleza kwamba akiwa mtu mweusi yuko katika mtihani hajiwezi hata kusimama hadharani kushughulikia gari lake, anakuwa si salama.

Mkanda wa video unaohusu mkasa huo, unamuonyesha Crosby akitoka nje ya gari lake chini ya ulinzi na mkono mmoja ameshikilia simu yake.



Dk. Lawrence Crosby.

Polisi wenye bunduki walimuagiza kulala chini na akatii, lakini walivamia na kuanza kumpiga miguuni.

Hata baada ya kugudulika anamiliki gari hilo kihalali, waliamuachia na akafungiliwa shitaka jingine, la kutotii amri ya polisi, shitaka ambalo jaji wa kesi hiyo alilitupa na ndipo Crosby, akafungua shitaka la madai ya fidia ya kuonewa.

Msemaji wa Polisi anawatetea askari wake kwamba, mateke waliopiga ni kwa misingi ya namna ya walivyofunzwa kumdhibiti mtuhumiwa.


# Takwimu za Biashara

Na Edward Ntwale & Elias Samweli

Bei ya Mazao Ya Chakula kwa Sh/kilo 100 Januari 20, 2019

| Mkoa | Arusha | D'Salaam | Dodoma | Kagera | Kigoma | Morogoro | Rukwa | Singida | Tabora | Tanga |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Mahindi | 45,000 | 70,000 | 45,000 | 66,000 | 50,000 | 50,000 | 50,000 | 52,000 | 55,000 | 47,000 |
| Mchele | 200,000 | 220,000 | 190,000 | 180,000 | 160,000 | 170,000 | 160,000 | 150,000 | 200,000 | 170,000 |
| Mtama | 35,000 | 80,000 | 35,000 | 100,000 | 70,000 | 95,000 | 80,000 | 60,000 | 100,000 | 80,000 |
| Uwele | 45,000 | 70,000 | 41,000 | 150,000 | 60,000 | 95,000 | NA | 54,000 | NA | 100,000 |
| Ulezi | 75,000 | 140,000 | 65,000 | 160,000 | 150,000 | 160,000 | 180,000 | NA | 190,000 | 120,000 |
| Ngano | 70,000 | 150,000 | 160,000 | NA | 150,000 | 175,000 | 100,000 | NA | NA | 100,000 |
| Maharage | 150,000 | 200,000 | 180,000 | 150,000 | 145,000 | 180,000 | 200,000 | 180,000 | 180,000 | 180,000 |
| Viazi Mviringo | 80,000 | 80,000 | 68,000 | 75,000 | 90,000 | 82,500 | 90,000 | 85,000 | 85,000 | 68,000 |

## Mwenendo wa Shilingi




## Mafuta

Bei : Kuanzia Januari 2, 2019

| MKOA | DSM | Arusha | Kibaha | Dodoma | Geita | Iringa | Katavi | Kigoma | Mwanza | Ruvuma |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Petroli | 2,295 | 2,255 | 2,300 | 2,354 | 2,461 | 2,359 | 2,503 | 2,527 | 2,445 | 2,419 |
| Dizeli | 2,224 | 2,299 | 2,228 | 2,283 | 2,389 | 2,288 | 2,432 | 2,455 | 2,374 | 2,347 |
| M'Taa | 2,202 | 2,286 | 2,206 | 2,260 | 2,367 | 2,266 | 2,410 | 2,433 | 2,352 | 2,325 |

## Soko la Hisa la Dar es Salaam Kikao cha Januari 23, 2019

### Muhtasari

| | | |
|---|---|---|
| TSI | 3,620.01 | -22.47 |
| DSEI | 2,008.02 | +0.75 |

Thamani za Hisa (bln)19,355.18

Mauzo 1,124,727,500.00

Hisa 294,740

### Zilizopanda na Zilizoshuka

| Kampuni | Bei | Badiliko |
|---|---|---|
| TBL | 12,400 | -1.59% |
| NMG | 1,320 | -1.49% |
| KCB | 900 | -1.10% |
| KA | 180 | +2.86% |
| EABL | 3,840 | +0.52% |

### Viwango vya kubadilisha

| Fedha | Nunua | Uza |
|---|---|---|
| EUR | 2,591.28 | 2,617.65 |
| USD | 2,268.07 | 2,290.76 |
| KES | 22.38 | 22.56 |
| GBP | 2,947.82 | 2,977.52 |

### Bei za hisa hadi kikao cha Januari 23, 2019

| Kampuni | Bei ya mwisho | Bei Iliyopita | Ba'liko % |
|---|---|---|---|
| ACA | 5,250 | 5,150 | +1.94 |
| CRDB | 140 | 140 | +0.00 |
| DCB | 340 | 340 | +0.00 |
| DSE | 1,320 | 1,320 | +0.00 |
| EABL | 3,840 | 3,820 | +0.52 |
| JHL | 9,750 | 9,550 | +2.09 |
| KA | 180 | 175 | +2.86 |

| Kampuni | Bei ya mwisho | Bei Iliyopita | Ba'liko % |
|---|---|---|---|
| KCB | 900 | 910 | -1.10 |
| MBP | 500 | 500 | +0.00 |
| MCB | 500 | 500 | +0.00 |
| MKCB | 800 | 800 | +0.00 |
| MUCOB | 400 | 400 | +0.00 |
| NICO | 265 | 265 | +0.00 |
| NMB | 2,340 | 2,340 | +0.00 |

| Kampuni | Bei ya mwisho | Bei Iliyopita | Ba'liko % |
|---|---|---|---|
| TBL | 12,400 | 12,600 | -1.59 |
| TCC | 17,000 | 17,000 | +0.00 |
| TCCL | 640 | 640 | +0.00 |
| TICL | 385 | 385 | +0.00 |
| TOL | 660 | 660 | +0.00 |
| TPCC | 2,060 | 2,060 | +0.00 |
| TTP | 120 | 120 | +0.00 |

## VIWANGO VYA KUBADILISHA FEDHA

| FEDHA | KUNUNUA | KUUZA |
|---|---|---|
| KENYA SHS | 22.44 | 22.62 |
| UGANDA SHS | 0.58 | 0.62 |
| RWANDAN FRANC | 2.53 | 2.56 |
| BURUNDI FRANC | 2.18 | 2.19 |
| USD | 2271.64 | 2294.36 |
| POUND STG | 2960.18 | 2990.01 |
| EURO | 2582.63 | 2608.69 |
| CANADIAN $ | 1706.85 | 1723.40 |
| SWITZ. FRANC | 2278.94 | 2301.03 |
| JAPANESE YEN | 20.71 | 20.92 |
| SWEDISH KRONOR | 252.17 | 254.60 |
| NORWEG. KRONOR | 264.79 | 267.28 |
| DANISH KRONOR | 345.95 | 349.30 |
| AUSTRALIAN $ | 1620.36 | 1636.80 |
| INDIAN RPS | 31.86 | 32.17 |
| PAKISTAN RPS | 15.55 | 16.27 |
| ZAMBIAN KWACHA | 188.35 | 191.36 |
| MALAWIAN KWACHA | 2.90 | 3.11 |
| MOZAMBIQUE-MET | 36.49 | 36.80 |
| ZIMBABWE $ | 0.43 | 0.43 |
| SDR | 3159.02 | 3190.61 |
| GOLD (T/O) | 2918812.10 | 2949835.71 |
| S. AFRICAN RAND | 163.90 | 165.42 |
| UAE DIRHAM | 618.50 | 624.57 |
| SINGAPORE $ | 1671.68 | 1687.77 |
| HONK KONG $ | 289.55 | 292.43 |
| SAUD ARABIAN RIAL | 605.72 | 611.72 |
| KUWAIT DINAR | 7489.51 | 7561.66 |
| BOTSWANA PULA | 214.67 | 218.19 |
| CHINESE YUAN | 334.74 | 338.04 |
| MALAYSIA RINGGIT | 549.37 | 554.19 |
| SOUTH KOREA WON | 2.02 | 2.03 |
| NEWZEALAND | 1541.99 | 1558.10 |

## Interbank Foreign Exchange Market (IFEM)

| Tarehe | Idadi (Mn USD) | Juu | Chini | Wastani |
|---|---|---|---|---|
| **23/Jan/2019** | **.70** | **2,300.00** | **2,293.40** | **2,294.36** |
| 22/Jan/2019 | .80 | 2,300.70 | 2,293.35 | 2,294.29 |
| 21/Jan/2019 | .90 | 2,301.80 | 2,293.30 | 2,294.27 |
| 18/Jan/2019 | .80 | 2,301.00 | 2,293.25 | 2,294.24 |

## Inter-bank Local Money Markets

| Tarehe | Kiasi (million-TZS) | Juu | Chini | Wastani (WAR) |
|---|---|---|---|---|
| **23/Jan/2019** | **44,500** | **4.20** | **2.50** | **3.38** |
| 22/Jan/2019 | 36,300 | 4.25 | 2.50 | 3.51 |
| 21/Jan/2019 | 23,000 | 4.20 | 3.50 | 3.59 |
| 18/Jan/2019 | 34,800 | 4.20 | 3.50 | 3.65 |
| 17/Jan/2019 | 19,000 | 4.20 | 3.00 | 3.84 |
| 16/Jan/2019 | 13,600 | 4.20 | 3.50 | 3.88 |

# Je, wajua? Magwiji 62 wamiliki nusu ya utajiri uliopo duniani

na asilimia 50 ya maskini zaidi, Oxfam inasema kati yao 53 ni wanaume na tisa tu ndiyo wanawake, hali inayoonyesha kuwapo uwiano sahihi, ikiwemo kwenye ngazi za juu.

Hiyo inaonyesha kwamba, wanawake wanawakilishwa vibaya.

**KUTOKA KONGAMANO**

Waziri Mkuu wa Canada, Justin Tradeau, ni miongoni mwa waliowasilisha ajenda kuu ya mwaka huu ya mataifa yaliyoinukia kiuchumi G7. Canada inachukua uenyekiti wa kundi hilo mwaka huu.

Ajenda kuu ni: "Mustakabali wa pamoja katika dunia iliyofarakana," ikitajwa kuwa inapingana moja kwa moja na sera ya Rais wa Marekani Donald Trump ya "Marekani kwanza," akihusisha sheria za kulinda soko la Marekani na sera za kujitenga.

Mwanzilishi wa Kongamano hilo la Kiuchumi Duniani, Klaus Schwab, anasema kuna hatari dhahiri katika nyakati zizizopo za kuvuruga mfumo wa kidunia.

Amesema hakuna namna ya kukabiliana na hali hiyo, iwapo hakutakuwapo ushirikiano wa kimataifa, katika kukabiliana na changamoto zinazoikabili dunia, suala ambalo jukwaa hilo linalisimamia.

Rais wa kongamano, Borge Brende, aliwaambia waandishi wa habari, kuwa mkusanyiko la wakuu 70 wa serikali mbalimbali duniani na wafanyabiashara wenye nguvu duniani, kunaweza kuleta mchango muhimu katika kukabiliana na vikwazo vya sasa vya sekta ya biashara duniani.

Rais wa Marekani, Donald Trump anatarajiwa kuhutubia kongamano hilo siku ya mwisho ya kongamano hilo.

Tangu alipochukua madaraka mwaka mmoja uliopita, Trump anonekana kuwa nyuma, katika kuunga mkono masuala ya utandawazi na utangamano, ambayo yanapewa nafasi kubwa katika kusanyiko hilo la Davos.

Kansela wa Ujerumani Angela Merkel, akiwa mtu muhimu anayetoka Umoja wa Ulaya, naye alipangwa kutoa hotuba kuhusu ushirikiano ndani ya Umoja wa Ulaya (EU).

Msemaji wa serikali ya Ujerumani, Steffen Seibert, anasema Ujerumani ni mshirika muhimu katika masuala ya kiuchumi na siasa ndani ya EU.

Anaongeza kuwa Ujerumani inajihusisha kwa sehemu kubwa katika mijadala ya kisiasa, kuhusu mustakabali wa maendeleo wa umoja huo na ndio maana Kansela Merkel amechagua kueleza mawazo yake kuhusu EU kwenye kongamano hilo la Davos.

Kansela Merkel, alipangwa kuzungumza siku moja pamoja na Rais wa Ufaransa, Emmanuel Macron.

Kiongozi wa Kanisa Katoliki Duniani, Papa Francis, kwa upande wake amewataka wafanyabiashara na wanasiasa katika kongamano hilo, kuandaa mazingira yatakayoruhusu ujenzi wa jamii inayohusisha makundi yote.

Alituma ujumbe huo kwa washiriki wa kongamano hilo la Davos, baada ya ziara yake nchini Chile na Peru.

Papa Francis, anasema wafanyabiashara wana nafasi muhimu ya kuleta mabadiliko, ambayo ni pamoja na kuunda nafasi za ajira mpya, kuheshimu sheria za kazi , kukabiliana na ufisadi na pia kuhamasisha haki ya jamii.

Ni kongamano linalowakutanisha zaidi ya washiriki 3,000 ambao miongoni mwao ni wanasiasa, wasomi, wakuu wa serikali, na viongozi wa taasisi za fedha dunia, pia makundi muhimu yasiyo ya kibiashara. **DW.**



# Serikali yaweka wazi upungufu wa walimu kwa asilimia 49

**Na Nebart Msokwa,** CHUNYA

NAIBU Katibu Mkuu wa Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Tixon Nzunda, amesema nchi inakabiliwa na upungufu wa walimu kwa asilimia 49 kwenye shule za umma.

Alitoa kauli hiyo juzi wilayani Chunya wakati wa ziara yake ya kukagua miundombinu ya elimu katika Mkoa wa Mbeya, ambapo alisema serikali itaendelea kuajiri walimu ili kuimarisha sekta ya elimu kwenye shule zote za umma.

Alisema lengo la serikali sasa hivi ni kuboresha elimu kwenye shule za umma na kuzifanya kuwa kimbilio la wanafunzi tofauti na ilivyo sasa, ambapo wazazi wengi huwa wanakimbilia kuwapeleka watoto wao kwenye shule za watu binafsi.

Nzunda alisema walimu wachache waliopo wana uwezo mkubwa wa kufundisha kuliko hata wale wanaofundisha kwenye shule za binafsi, lakini wakati mwingine wanashindwa kufanya vizuri kutokana na mazingira ya kazi.

"Kwa taarifa zilizopo ni kwamba upungufu wa walimu katika Wilaya ya Chunya ni asilimia 35 ambayo inaonyesha kuwa ninyi mna nafuu maana kitaifa upungufu ni asilimia 49, pamoja na hilo tutaendelea kuwaletea walimu katika ajira mpya zijazo," alisema Nzunda.

Alisema walimu wanaolengwa kuajiriwa zaidi na serikali ni wale wa masomo ya sayansi kwa madai kuwa hao ndio wachache zaidi na wanatakiwa kuajiriwa zaidi ili kuendana na serikali ya awamu ya tano inayolenga kuimarisha uchumi wa viwanda.

Hata hivyo aliwataka walimu wanaofanya kazi katika shule za serikali kuongeza juhudi katika kufundisha, ili kurejesha heshima ya shule hizo kama ilivyokuwa miaka ya nyuma ambapo zilikuwa zinafanya vizuri kuliko shule za watu binafsi.

Alisema walimu wanaofundisha shule za binafsi sio kweli kwamba wana uwezo mkubwa zaidi wa kufundisha kuliko wale wanaofundisha shule za umma, lakini tatizo ni kutojituma kuwasaidia watoto wa maskini.

"Walimu wanaofundisha shule za umma na wanaofundisha za watu binafsi wote wanasoma vyuo vikuu vya hapa hapa nchini, wanasoma Chuo Kikuu cha Dar es Salaam wote, Dodoma na vyuo vingine hakuna anayesoma vyuo vya nje ya nchi, sasa kwa nini wao wafanye vizuri zaidi?" Alihoji Nzunda.

Alisisitiza kuwa, kwa sasa serikali ya awamu ya tano inagharimia elimu kuanzia darasa la awali mpaka kidato cha nne na inatumia zaidi ya Shilingi milioni 23 kila mwezi, hivyo lazima kila mtu atimize wajibu wake ili thamani ya elimu ipande.

Aliwataka wazazi kushiriki kikamilifu katika kuboresha miundombinu kwenye shule za serikali ili kuunga mkono juhudi za uboreshaji wa elimu.



Wanafunzi wa Shule ya Sekondari Ileje, wakionyesha furaha yao baada ya kupokea msaada wa stuli 184 zenye thamani ya Shilingi milioni 5, uliotolewa na benki ya NMB, kwa ajili ya kuboresha masomo ya sayansi katika wilaya za Ileje na Momba za jijini Mbeya juzi. Benki hiyo, pia juzi ilitoa mabati 254 kwa Halmashauri ya Tunduma wilayani Momba, madawati 50 kwa Shule ya Msingi Nyerere na Kafule vyote vikiwa na thamani ya Shilingi milioni 25. **PICHA: NMB**

## Diwani atoboa siri wanawake kukosa wenza kliniki

**Na Grace Mwakalinga,** MBARALI

BAADHI ya wanawake wanaopata ujauzito kabla ya kuolewa katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali mkoani Mbeya, wanashindwa kwenda kliniki na wenza wao kwa kuwa wengi ni waume za watu.

Hayo yalisemwa jana na diwani wa viti maalum wilaya hiyo, Lucy Ngondo (Chadema), wakati wa kikao cha kawaida cha Baraza la Madiwani wa Halmashauri hiyo kilichofanyika katika ukumbi wa halmashauri hiyo.

Ngondo alisema kipindi hiki kuna taratibu katika hospitali mbalimbali kuwa kila mwanamke mjamzito anapohudhuria kliniki kwa mara ya kwanza analazimika kwenda na mwenza wake ili wachukuliwe vipimo mbalimbali kikiwamo kipimo cha Ukimwi.

Alisema kutokana na wanawake hao kupewa ujauzito na waume za watu, huwa wanakosa ushirikiano kwa wanaume wanapoenda kliniki na hivyo kupata wakati mgumu kwenye huduma.

"Tunaomba itungwe sheria ndogo ndogo ya kuwabana wanawake wajawazito wasiopima maambukizi ya virusi vya Ukimwi wanapokuwa wajawazito, kuna wengine wanazaa na waume za watu, hivyo na huwa wanafanya kwa kificho, huwa wanapata wakati mgumu kuwashawishi kwenda nao kliniki," alisema Ngondo.

Akichangia hoja hiyo Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali, Bahati Salum, alisema baadhi ya wanaume walio kwenye ndoa wanaogopa kwenda kliniki na wanawake waliowasababishia ujauzito.

Alisema halmashauri kwa kushirikiana na taasisi mbalimbali kuandaa mpango kutoa elimu kwa wajawazito kuwatambua na kuwashauri umuhimu wa kupima afya zao.

# Vijana wanaoishi mazingira magumu wanolewa

**Na Mwandishi Wetu,** MBEYA

VIJANA 121 wanaoishi katika mazingira magumu kutoka katika halmashauri tatu za Mkoa wa Mbeya wamehitimu mafunzo ya wiki tatu ya ujenzi wa vyoo bora katika Chuo ya Ufundi Stadi Veta cha jijini Mbeya.

Mafunzo ya vijana hao kutoka vijiji 24 na mitaa minne ya halmashauri hizo yamegharimiwa na serikali kwa kushirikiana na sekta binafsi ya usafi wa mazingira (YESB), inayoendeshwa na shirika lisilo la kiserikali la Catholic Relief Service (CRS) kwa lengo la kulinda afya za wananchi kwenye maeneo husika.

Halmashauri ambazo vijana hao wanaoishi mazingira magumu wamechukuliwa ni Mbarali, Mbeya na Chunya ambazo zimekuwa zikikumbwa na maradhi ya mlipuko hasa kipindupindu kila mwaka.

Akifunga mafunzo ya vijana hao, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Chunya, Sophia Kumbuli, alisema mradi huo wa ushirikishwaji wa vijana katika biashara ya ujenzi wa vyoo bora pia utawasaidia vijana hao kujiajiri na kujiingizia kipato.

Kumbuli ambaye alizungumza kwa niaba ya wakurugenzi wenzake aliahidi halmashauri hizo kuwasaidia vijana hao kupata mitaji kwa kuwakopesha fedha kupitia fedha zinazopaswa kukopeshwa kwa vikundi vya vijana ambazo ni asilimia nne ya mapato ya ndani ya halmashauri.

"Serikali ilishatoa maelekezo na sasa ni sheria kwamba kila halmashauri itumie asilimia nne ya mapato yake ya ndani kuwakopesha vijana, mimi pamoja na wakurugenzi wenzagu tunaahidi kutumia fedha hizo kuwakopesha ili mpate mtaji wa kuendeshea shughuli zenu za ujenzi wa vyoo bora kwenye jamii yetu," alisema Kumbuli.

Hata hivyo Kumbuli aliwataka vijana hao kuunda vikundi ili waweze kupata sifa ya kukopea fedha hizo kwa mujibu wa sheria na miongozo iliyotolewa na serikali.

Akizungumza kwa niaba ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali, Uswege Kaminyoge, aliwataka vijana hao kutumia vizuri fursa za mikopo watakayoipataka kutoka kwenye halmashauri kwa lengo la kuhakikisha wanafikia malengo yaliyokusudiwa.

Kwa upande wake, Meneja wa mradi (CRS), Mhandisi Ephraim Tonya, alisema lengo ni kuongeza msukumo na jitihada za serikali katika kuhakikisha jamii ya Watanzania wanatumia vyoo bora hususani kuwaondoa vijana hao katika makundi yasiyofaa na hivyo kuwapatia nyenzo za kuajiri na kutoa ajira kwa vijana wasio na ajira nchini.


Alisema kuwa wamelenga kulisaidia kundi la vijana kutokana na changamoto mbalimbali wanazokumbana nazo hususan kunyanyapaliwa na kutengwa na jamii na kuonekana sio sehemu ya jamii yenye uhitaji wa kupata fursa ya elimu kuajiriwa na kujiajiri.

"Mradi huu ulianza kutekelezwa mwezi Mei mwaka jana na ukomo wake ni Aprili 2021 na lengo kuu ni kuwajengea uwezo vijana ambao wanaishi katika mazingira magumu na wasio katika sekta rasmi za ajira katika wilaya tatu, Chunya, Mbarali na Mbeya Vijijini," alisema.

Mkazi wa kijiji cha Isewe wilayani Chunya, Muone Mkumbo ambaye amehitimu mafunzo hayo, alisema yatakuwa chachu na kuwapatia mbinu mbalimbali za ujenzi wa vyoo bora hususan katika jamii na kuwa wajasiriamali katika nyanja mbalimbali nchini.

Naye Jesta Nyambega mkazi wa Kata ya Ubaruku wilayani Mbarali, aliiomba serikali kuwatengenezea mfumo rasmi wa tenda za ujenzi wa vyoo bora kutoka katika halmashauri, taasisi binafsi na kampuni ili kuondokana na changamoto ya kukaa na ujuzi majumbani.

Alisema kwa kutambua sera ya kitaifa ya serikali ya awamu ya tano ya kutaka kila kaya na kijiji kuwa na choo bora ni wakati sasa hata jamii kushirikishwa na kupatiwa elimu ya matumizi ya vyoo visivyo na ubora katika kukabiliana na magonjwa ya milipuko.





# Profesa Mbarawa avunja Bodi ya Maji kwa uzembe

**Na Paul Mabeja,** KONGWA

WAZIRI wa Maji, Profesa Makame Mbarawa, amevunja Bodi ya Maji mji mdogo wa Kibaigwa (KIBAWASA), wilayani Kongwa mkoani Dodoma, kutokana na Mwenyekiti wake Simoni Mitumba, kuwa mlevi, hivyo kushindwa kusimamia uendeshaji wa majukumu yake.

Profesa Mbarawa aliivunja bodi hiyo juzi, wakati alipofanya ziara ya kutembelea miradi mbalimbali ya maji katika wilaya hiyo.

Awali kabla ya kuvunja bodi hiyo, Mbunge wa Jimbo hilo, Job Ndugai, alimweleza Waziri Mbarawa, kuwa bodi hiyo imeshindwa kutekeleza majukumu yake hali ambayo inasababisha wananchi kukosa maji.

Ndugai alisema kuwa tatizo la maji katika eneo hilo la Kibaigwa kwa kiasi kikubwa sio la serikali bali ni utendaji mbovu wa mamlaka ya mji huo kushindwa kutimiza majukumu yake.

"Tatizo la maji hapa kwetu mheshimiwa waziri sio serikali, kwa sababu serikali yetu inaleta fedha nyingi kabisa kwa ajili ya miradi ya maji, lakini shida imekuwa ni kwa watendaji wetu kushindwa kusimamia majukumu yao na kusababisha wanachi kukosa maji," alisema Ndugai.

Alisema kuwa kama serikali inataka kuwasaidia wananchi wa Kibaingwa katika kuwatatulia tatizo la maji inatakiwa kuivunja bodi hiyo ambayo imekuwa ikiendeshwa na mwenyekiti ambaye muda wote anakuwa amelewa. "Huyu mwenyekiti mimi ni mzee wangu tunaheshimiana sana lakini, kama mnavyoona hapa alipo amelewa yuko safi na hivi tuu waziri yupo hapa kalewa, je, siku ambayo waziri hayupo si ndio itakuwa hatari kabisa," alihoji Ndugai.

Kutokana na hali hiyo Waziri Prof. Mbarawa, alitangaza kuivunja bodi hiyo na kuahidi kuleta watu wengine ambao watakuja kusimamia na kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi.

"Mheshimiwa Spika hata kama usingeniomba kuivunja bodi hii, lazima ningeivunja, hatuwezi kuendelea kuwa na bodi ambayo haijitambui imeshindwa hata kuwezesha mamlaka ya maji kujiendesha yenyewe hata kununua pampu tuu ya kusukumia maji wanataka wizara tuwafanyie," alisema Mbarawa.

Aliongeza kuwa yeye akiwa kama Waziri wa Maji atahakikisha kuwa wilaya hiyo inapata huduma ya maji kwa asilimia 90 ifikapo 2020. "Hapa Kongwa tayari upo mradi mkubwa ambao umegharamiwa na serikali wa Sh. bilioni 1.7 ambao ukimalika utaweza kufanya tatizo la maji katika mji wa Kongwa kuwa historia kwa kuwa tutaweza kuzalisha maji lita zaidi ya Sh. milioni 3.91 kwa siku," alisema.

Aidha, alisema wizara hiyo itahakikisha inamlipa mkandarasi SAJO CBC ambaye anaidai serikali zaidi ya Sh. milioni 300, ili aendelee na utekelezaji wa miradi ya maji ili kuwaondolea adha wananchi katika maeneo mbalimbali katika wilaya hiyo.

"Pia wizara tutatoa Sh. milioni 25 kwa ajili ya kununulia pampu ya kusukumia maji ambayo itafungwa katika mji mdogo wa Kibaingwa ambao umekuwa na tatizo la maji kutoka na bodi yake kushindwa kutimiza majukumu yake," alisema.

Hata hivyo alimtaka Meneja wa Mamlaka ya Maji ya mji mdogo wa Kibaingwa, Boniphace Bihemo, kuhakikisha kuwa anakusanya zaidi ya Sh. milioni 52 kwa mwezi badala ya Sh. milioni 32, ambazo wanakusanya hivi sasa.




Msemaji wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji nchini, Insp. Joseph Mwasabeja, akitoa taarifa kwa waandishi habari jijini Dodoma jana, kuhusu uanzishaji mpya wa makusanyo ya mapato ya mfumo wa serikali wa kielektroniki jijini humo. **PICHA: PETER MKWAVILA.**

# Serikali yamwagiwa sifa mapambano ujangili

**Na Renataha Msungu,** DODOMA

MAOFISA wa usalama pamoja na vitengo mbalimbali vya kupambana na ujangili nchini, wamepongeza hatua iliyochukuliwa na serikali pamoja na taasisi isiyo ya kiserikali ya PAMS Foundation kuwapatia elimu na kuunganisha nguvu kwa vitengo vyote katika kudhibiti ujangili.

Akizungumza na gazeti hili Wakili wa Serikali, Salim Msemo, alisema mafunzo ni muhimu kwa vyombo hivyo kwa kuwa itapunguza mlolongo mrefu wa kushughulikia kesi za ujangili.

"Kwetu sisi hii inatusaidia kupambana na hawa majangili ambao wamekuwa wakifanya rasilimali za nchi kama zao na kufanya watakavyo," alisema Msemo.

Kwa upande wake Elisifa Ngowi mmoja wa washiriki, alisema kitendo cha kujenga nguvu moja katika kupambana na ujangili linakuwa ni jambo nzuri sana, kwa sababu tembo ni mali ya Watanzani ambao wanatakiwa kutunzwa ili kulileta taifa fedha kwa vizazi na vizazi.

"Huu ni urithi wa Watanzania kwa vizazi na vizazi, kwa hiyo ni muhimu tuliyobahatika kuwepo leo tuutunze urithi wa Tanzania kwa gharama zote,"alisema Ngowi.

Semina hiyo ya siku tano inayohusisha taasisi zote zilizopewa jukumu la kudhibiti ujangili pamoja na magendo nchini, imefanyika chini ya udhamini wa PAMS Foundation taasisi isiyo ya kiserikali inayojihusisha na mapambano ya ujangili wa tembo toka 2016, hapa nchini mpaka sasa.

Wajumbe hao wa semina wanatoka katika vyombo vya National Task Force Ant-poaching (NTP), maofisa wa polisi, waendesha mashtaka wa serikali,

Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) na Mamlaka ya Hifadhi ya Taifa katika kukabiliana na ujangili.

Akizungumza kwenye semina hiyo mkurugenzi msaidizi wa kuzuia ujangili ambaye pia ni mwenyekiti wa kikosi cha taifa cha kupambana na ujangili, Robert Mande, amesema mafunzo ni muhimu.

"Unajua wakati wa nyuma tulikuwa tunakwamishwa na kitu kinaitwa protoko ambazo ukimkamata mhalifu mpaka uje umfikishe mahakamani, inachukuwa muda mrefu sana, jambo ambalo majangili wanatumia mwanya huo kujinasua,"alisema Mande.

Kwa upande wake mkurugenzi wa PAMS Foundation, Krissie Clark, alisema kampeni hiyo iliyoanza mwaka 2016 mpaka sasa inaonyesha mafanikio makubwa sana na uuaji wa tembo umepungua kwa kasi kubwa.

"Sisi kama wadau tunafurahi tunapoona lengo letu linafanikiwa, kumaliza mauaji ya tembo hapa nchini ambayo yalikuwa yanatishia amani ya wanyama hawa, ilikuwa kama walikosewa na Mungu kuzaliwa Tanzania," alisema Krissie.

Kwa mujibu wa Katibu wa Wizara ya Maliasili akizungumza juzi, wakati wa ufunguzi, alisema suala hili la kuwaweka wadau pamoja litasaidia kabisa na kufikisha asilimia sifuri mauaji ya tembe hapa nchini ifikapo 2024 kama ilivyo mkakati wa serikali.

## DC atangaza neema skimu ya umwagiliaji

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

MKUU wa Wilaya ya Mpwapwa mkoani Dodoma, Jabir Shekimweri, amesema mradi wa skimu ya umwagiliaji ya Msagali ukikamilika utaweza kulisha makao makuu ya nchi na kuzuia athari za miundombinu zitokanazo na mafuriko.

Kutokana na faida hizo ameiomba serikali kupitia wizara zinazohusika pamoja na wadau kuwekeza katika mradi huo, ili uweze kuleta tija ya uzalishaji na hivyo kutoa matokeo chanya.

Akizungumza katika bwawa hilo juzi, wakati wa ziara ya Kamati ya Siasa ya CCM ya Mkoa wa Dodoma, Shekimweri, alisema kupitia mradi huo chakula, mboga na samaki vitapatikana kwa wingi na hivyo kuweza kulisha Mkoa wa Dodoma na maeneo ya jirani.

"Mradi huu ulibuniwa siku nyingi, lakini utekelezaji wake ulikuwa wa kusuasua, kwa mujibu wa maandiko ya mwaka 2004/2005, ulihitaji Sh. bilioni 11, ili ukamilike lakini uliingiwa na sintofahamu na mradi kushindwa kutekelezwa," alisema Shekimweri. Alisema mradi huo ni mtambuka na unahitaji ushirikiano wa pamoja kwa kuhusisha wizara mbalimbali.

"Sasa hivi kipato cha mkazi wa Dodoma kwa mwaka ni Sh. milioni 1.5, lakini kupitia mradi huu na faida nilizotaja kipato kitaongezeka kwa mkazi wa Dodoma hadi kufikia Shilingi milioni tatu kwa mwaka, kupitia mradi huu miundombinu ya barabara na reli haitaharibika kutokana na mafuriko hasa katika maeneo ya Godegode na Kilosa ambayo yanatokea mafuriko mara kwa mara," alisema mkuu huyo.

Kutokana na faida za mradi huo alisema kama wilaya wamefanya jitihada mbalimbali za kufufua mradi huo, ambapo alikutana na watu wa umwagiliaji kanda, mhandisi wa umwagiliaji mkoa na wataalamu wa mkoa kuona namna gani wanaweza kufanya. Pia mradi huo ni moja kati ya miradi mikakati ya wilaya, ambapo wanawakaribisha wawekezaji wenye mitaji mikubwa ya kiwango hicho kuweza kuwekeza na katika kongamano la fursa la uwekezaji linalotarajiwa kufanyika hivi karibuni wataeleza fursa hiyo iliyopo.

Akizungumza katika ziara hiyo baada ya kukagua mradi huo Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Mkoa wa Dodoma, Godwin Mkanwa, aliitaka halmashauri na timu ya wataalamu kukaa chini kutengeneza andiko linalobeba mradi mzima ili lipelekwe panapohusika.

"Andiko hilo mkishaliandaa lipitisheni kwenye vikao, tupeleke mbele ili tuone serikali itakavyosaidia kunusuru mradi huo," alisema.

# Matukio ya ukatili wa kijinsia yamwibua waziri hadharani

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WIZARA ya Uwezeshaji Wanawake, Watoto na Wazee, imesikitishwa na matukio ya mauaji ikiwamo msichana wa miaka (19), kufanyiwa ukatili wa kijinsia kwa kubakwa na baadaye kuuawa kikatili nyumbani kwao.

Waziri wa Uwezeshaji Wanawake na Watoto, Mauldlic Castico, alisema hayo wakati alipozitembelea familia mbili ambazo watoto wao wameuawa kikatili hivi karibuni. Castico aliitembelea familia ya msichana aliyefahamika kwa jina la

Zuhura Ali Abdalla (19), ambaye alibakwa Januari 12, akiwa nyumbani kwao Uholanzi Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja.

Waziri Castico alisikitishwa na tukio hilo ambalo linaonyesha kwamba jamii bado inakabiliwa na ukatili wa kutisha.

"Nimesikitishwa na taarifa za ukatili aliofanyiwa marehemu kubakwa hadi kufariki dunia ... matukio haya yanalitia doa kubwa wa nchi yetu ambayo inaaminika kuwa ni kisiwa cha amani na utulivu," alisema.

Aidha, alivitaka vyombo vya ulinzi kuharakisha kukamilisha uchunguzi wa tukio hilo na wahusika kufikishwa mbele ya vyombo vya sheria kwa hatua zaidi.

Alilaani tukio lingine la kubakwa kwa mtoto mwenye ulemavu miaka (16) na kusababisha kupata maumivu makali. "Matukio yote haya ni ya kusikitisha sana yakionyesha ukatili dhidi ya mwanamke na kutishia ustawi wa maisha yake katika kupiga hatua kubwa ya maendeleo," alisema.

Naye askari wa upelelezi kutoka Jeshi la Polisi Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja, alisema Jeshi la Polisi kwa sasa linawashikilia watuhumiwa wawili kwa uchunguzi zaidi kutokana na mauaji ya msichana huyo.

"Kwa sasa tunawashikilia watu wawili kuhusiana na tukio hili na uchunguzi zaidi unaendelea kuhakikisha watuhumiwa wanafikishwa mbele ya vyombo vya sheria," alisema Mussa.




Makamu wa Rais, Samia Suluhu Hassan, akizungumza na Mwenyekiti wa Chama cha Majaji na Mahakimu Wanawake Tanzania (TAWJA), Jaji Imani Aboud, wakati wa hafla ya ufunguzi wa Mkutano Mkuu wa TAWJA, uliofanyika kwenye Hoteli ya Verde, Zanzibar juzi. **PICHA: OMR**

# Wanafunzi wachekelea matunda ya elimu bure

**Na Mwandishi Wetu,**
ZANZIBAR

SHIULE za msingi za Wilaya ya Micheweni Pemba zimepata mgawo wa madaftari kwa ajili ya wanafunzi wake ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa elimu bure na kuondosha michango inayokuwa wakichangia wazazi.

Ofisa Elimu Msingi Wilaya ya Micheweni Pemba, Tarehe Khamis, alisema usambazaji wa madaftari hayo ni sehemu ya agizo la serikali la kuwapatia huduma zote muhimu wanafunzi bila ya malipo.

Alisema tayari Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imetangaza elimu bure kwa wanafunzi wote na kufuta michango ya ada ikiwamo vifaa vya shule kama madaftari.

"Wizara ya Elimu tunachokifanya ni kutekeleza agizo la serikali kufuta michango na vifaa vya shule ikiwamo madaftari kwa wanafunzi wa shule zote za msingi," alisema.

Ofisa Elimu wa Halmashauri ya Wilaya Micheweni anayeshughulika na ugatuzi, Suleiman Juma, alisema kinachofanywa na serikali ni sehemu ya utekelezaji wa mpango unaohusisha sekta ya elimu.

Alisema shule za msingi zote zipo katika mpango wa ugatuzi ambao umelenga katika kuboresha sekta hiyo na kuleta mabadiliko makubwa. Alieleza kuwa kitendo cha kugawa madaftari bure kwa wanafunzi wote wa shule za msingi kwa kiasi kikubwa kitapunguza mzigo uliokuwa ukibebwa na wazazi kuchangia sekta ya elimu.

"Serikali ya Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni inatekeleza mpango wa ugatuzi katika sekta ya elimu ambayo imetangazwa kuwa bure," alisema.

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imetangaza mpango wa ugatuzi na kuzihusisha sekta tatu muhimu ikiwamo elimu ya msingi,

## Wanachama Saccos kujazwa mifuko yao

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

UONGOZI wa kikundi cha ushirika cha kuweka na kukopa (Melinne Saccos) unatarajia kutoa jumla ya Sh. milioni 79 kwa wanachama wake, ili ziweze kuwasaidia katika harakati za kimaendeleo.

Akizungumza na waandishi wa habari huko ofisini kwake Mjini Zanzibar, Abubakar Mtumwa Ali, alisema mgao huo umetolewa kwa mujibu wa sheria na kila mmoja atapewa kulingana na akiba aliyoweka.

Alisema miaka kadhaa iliyopita wanachama walikuwa wanaridhia mgao huo kubaki katika Saccos na kutumika katika harakati za maendeleo.

Alisema mkutano mkuu wa mwaka jana wa Saccos hiyo umeridhia akiba irejeshwe kwa wanachama wenyewe.

Aidha, alisema mgao huo utatolewa kwa mujibu wa katiba yao na kuwaomba wanachama kuweka akiba kwa wingi ili waweze kunufaika na migao inapotokea.

Aliwaomba wananchi kujiunga na Saccos zilizo imara ili waweze kuweka na kukopa.

Aliwataka wananchi kuondokana na dhana potofu ya kuwa kujiunga na vikundi vya ushirika ni kuibiana fedha jambo ambalo alisema halina ukweli ndani yake.

Naye Katibu wa Ushirika, Njuma Ali Juma, alisema tangu kuanzishwa ushirika huo wamepata mafanikio makubwa ikiwamo kukopa pesa na kufanya biashara, kununua viwanja na kujenga makazi ya kudumu kupitia ushirika huo.

Aidha, alisema kutokana na biashara wanazofanya zimesaidia kusaidia familia na kuondokana na hali ya utegemezi kutoka kwa waume zao.

# RATIBA

## CAPITAL TELEVISION

**Mon 21 Jan**
- 06:00 Al jazera
- 08:00 CNN International News
- 09:00 Al Jazeera
- 10:00 Kumekucha
- 10:30 Kumekucha Michezo
- 11:30 Kumekucha Kishindo
- 12:00 Turning the spotlight rpt:
- 12:30 Drive it rpt
- 13:00 Series rpt : Inkulo
- 13:45 Series rpt: Ode To Joy
- 14:30 Usafiri wako rpt
- 15:00 Cookery rpt: Culinary Delight
- 15:30 Toyota world of wildlife rpt
- 16:00 CNN International
- 17:00 Eco@Africa rpt
- 17:30 Meza huru
- 19:00 The Décor rpt
- 19:30 Business edition
- 20:00 Series: Inkulo
- 20:45 The Monday Agenda
- 21:30 Capital Prime News
- 22:00 Kipima Joto
- 00:00 Al Jazeera

**Tues 22 Jan**
- 06:00 Al Jazeera
- 08:00 CNN International News
- 09:00 Al Jazeera
- 10:00 Kumekucha
- 10:30 Kumekucha Michezo
- 11:30 Kumekucha Kishindo
- 12:00 The Decor rpt
- 12:30 Mizengwe rpt
- 12:45 Aibu Yako
- 13:00 Series rpt: Inkulo
- 13:45 Series rpt: Ode To Joy
- 14:15 Local pgm rpt: Business Edition
- 15:00 Bundesliga kick off
- 15:30 Out and About rpt
- 16:00 Capchat rpt
- 17:00 Ripoti Maalum rpt
- 17:30 Meza huru
- 19:00 Innovation
- 19:30 Ripoti Maalum
- 20:00 Series: Inkulo
- 20:45 Series: Ode To Joy
- 21:30 Capital Prime
- 22:00 Turning the Spotlight rpt
- 22:30 Iron Chef rpt
- 23:30 Al Jazeera

**Wed 23 Jan**
- 06:00 Al jazeera
- 08:00 CNN International News
- 06:00 Al Jazeera
- 08:00 CNN International News
- 09:00 Al Jazeera
- 10:00 Kumekucha
- 10:30 Kumekucha Michezo
- 11:30 Kumekucha Kishindo
- 12:00 Turning the Spotlight rpt
- 12:30 Culinary delight rpt
- 13:00 Series rpt: Inkulo
- 13:45 Series rpt: Ode To Joy
- 14:30 Local Pgm: The Monday Agenda Rpt
- 15:15 Capchat rpt
- 16:15 CNN International
- 17:00 Innovation rpt
- 17:30 Meza Huru
- 19:00 Sports Gazette
- 19:30 Business edition rpt
- 20:00 Series: Inkulo
- 20:45 Series: Ode To Joy
- 21:30 Capital Prime News
- 22:00 Dakika 45:
- 22:45 The Décor
- 23:15 Al Jazeera

**Thurs 24 Jan**
- 06:00 Al Jazeera
- 08:00 CNN International News
- 09:00 Al Jazeera
- 10:00 Kumekucha
- 10:30 Kumekucha Michezo
- 11:30 Kumekucha Kishindo
- 12:00 Sports Gazette
- 12:30 Out n' about rpt:
- 13:00 Series rpt: Inkulo
- 13:45 Series rpt: Ode To Joy
- 14:30 Business Edition rpt
- 15:00 Korean Drama rpt: Emperor of the sea
- 16:00 Dakika 45 rpt
- 17:00 In good shape
- 17:30 Meza Huru
- 19:00 Turning the spotlight
- 19;30 Usafiri wako
- 20:00 Series: Inkulo
- 20:45 Series: Ode To Joy
- 21:30 Capital Prime News
- 22:00 Capchat rpt
- 23:00 Al Jazeera

**Frid 25 Jan**
- 06:00 Al Jazeera
- 08:00 CNN International News
- 09:00 Al Jazeera
- 10:00 Kumekucha
- 10:30 Kumekucha Michezo
- 11:30 Kumekucha Kishindo
- 12:00 Innovation rpt
- 12:30 The Decor rpt
- 13:00 Series rpt: Inkulo
- 13:45 Series rpt: Ode To Joy
- 14:30 Ripoti Maalum rpt
- 15:00 Korean Dram rpt: Emperor of the sea
- 16:00 CNN International
- 16:30 The Monday Agenda rpt
- 17:30 Meza Huru
- 19:00 Drive it
- 19:30 Eco@Africa
- 20:00 Aibu yako
- 20:15 Local Pgm: Business Edition
- 20:45 Series: Ode To Joy
- 21:30 Capital Prime News
- 22:00 Malumbano ya hoja rpt
- 00:00 Al Jazeera

**Sat 26**
- 08:00 CNN International
- 09:00 Drive It rpt
- 09:30 Turning the Spotlight rpt
- 10:00 Culinary delight rpt
- 10:30 Innovation rpt
- 11:00 Out n'about rpt
- 11:30 Sports Gazette rpt
- 12:00 Usafiri wako rpt
- 12:30 Eco@Africa rpt
- 13:00 Business edition rpt
- 13:30 Korean Drama rpt: Emperor of the sea
- 14:30 Telenovela rpt: Ode To Joy
- 17:15 Ripoti Maaalum rpt
- 17:45 Bundesliga kick off
- 18:15 Capchat rpt
- 19:15 Mizengwe
- 19:30 The Decor
- 20:00 Iron Chef.
- 21:00 Out n' about
- 21:30 Vienna Philharmonic New Year's concert
- 23:00 The other side rpt
- 01:00 Al Jazeera

**Sun 27 Jan**
- 08:00 CNN International
- 09:00 In good shape
- 10:00 Capchat rpt
- 11:00 Sports Gazette rpt
- 11:30 Iron chef rpt
- 12:00 Out n about rpt
- 12:30 Bundesligga Kick Off rpt
- 13:00 Ripoti Maalum
- 13:30 Series rpt: Inkulo
- 15:15 Aibu yako
- 15:30 Drive it rpt
- 16:00 Dakika 45 rpt
- 16:45 Mizengwe rpt
- 17:00 The Decor rpt
- 17:30 Meza huru
- 19:00 Turning the Spotlight rpt
- 19:30 Cookery pgm:Culinary Delights
- 20:00 Korean Drama rpt: Emperor of the sea
- 21:00 Shift
- 21:15 Capchat live
- 22:15 Telenovela: Ode To Joy
- 00:00 Al Jazeera

## ITV Daima WEEKLY-SCHEDULE

**MONDAY 21 Jan**
- 05:30 Uwanja wa Mazoezi
- 06:00 Habari
- 06:40 Kumekucha
- 07:30 HABARI
- 08:00 Kumekucha Michezo
- 08:55 Habari za saa
- 09:00 Kumekucha Kishindo
- 09:30 Isidingo
- 09:55 Habari za saa
- 10:00 Watoto wetu
- 10:30 Igizo: Hatua
- 10:55 Habari za saa
- 11:00 Kimya Milele
- 11:55 Habari za saa
- 12:00 Al Jazeera
- 12:30 Jungu kuu rpt
- 12:55 Habari za saa
- 13:00 Mjue Zaidi
- 13:55 Habari za saa
- 14:00 Telenovela: Destiny (Destino)
- 14:55 Habari za saa
- 15:00 Meza Huru
- 16:30 Watoto Wetu
- 17:00 The Base
- 18:00 Jiji Letu
- 18:10 Aibu yako rpt
- 18:15 Huduma ya kwanza
- 18:30 Shamba shape up
- 19:00 Afya ya Jamii
- 19:30 Isidingo
- 20:00 Habari
- 21:05 Dakika 45
- 22:00 Telenovela: Destiny (Destino)
- 23:00 Habari
- 23:30 The Base
- 00:30 Al Jazeera
- 02:00 CNN International

**TUESDAY 22 Jan**
- 05:30 Uwanja wa Mazoezi
- 06:00 Habari
- 06:40 Kumekucha
- 07:30 HABARI
- 08:00 Kumekucha Michezo
- 08:55 Habari za saa
- 09:00 Kumekucha Kishindo
- 09:30 Isidingo
- 09:55 Habari za saa
- 10:00 Watoto wetu
- 10:30 Hawavumi lakini wamo
- 10:55 Habari za saa
- 11:00 Hawavumi lakini wamo
- 11:15 Igizo: Mtego
- 11:55 Habari za saa
- 12:00 Al Jazeera
- 12:30 Afya ya jamii rpt
- 12:55 Habari za saa
- 13:00 Uchumi na biashara
- 13:30 Kipindi Maalum rpt : TFDA
- 13:55 Habari za saa
- 14:00 Huduma ya kwanza
- 14:15 Telenovela: Destiny (Destino) rpt:
- 14:55 Habari za saa
- 15:00 Meza Huru
- 16:30 Watoto wetu
- 17:00 The Base
- 18:00 Jiji Letu
- 18:15 Korean drama rpt: The Great Queen
- 19:00 Jarida la wanawake
- 19:30 Isidingo
- 20:00 Habari
- 21:00 Kipindi maalum:
- 22:00 Telenovela: Destiny (Destino)
- 23:00 Habari
- 23:30 The Base
- 00:30 CNN International

**WEDNESDAY 23 Jan**
- 05:30 Uwanja wa Mazoezi
- 06:00 HABARI
- 06:40 Kumekucha
- 07:30 HABARI
- 08:00 Kumekucha Michezo
- 08:55 Habari za saa
- 09:00 Kumekucha Kishindo
- 09:30 Isidingo
- 09:55 Habari za saa
- 10:00 Watoto wetu
- 10:30 Shamba shape up
- 10:55 Habari za saa
- 11:00 Korean: The Great Queen
- 11:55 Habari za saa
- 12:00 Al Jazeera
- 12:30 Jarida la wanawake rpt
- 12:55 Habari za saa
- 13:00 Dakika 45
- 13:55 Habari za saa
- 14:00 Telenovela rpt: Destiny (Destino):
- 14:55 Habari za saa
- 15:00 Meza Huru
- 16:30 Watoto Wetu
- 17:00 The Base
- 18:00 Jiji Letu
- 18:15 Igizo: Mizengwe
- 18:30 Ijue Sheria
- 19:00 Kipindi Maalum: TFDA
- 19:30 Isidingo
- 20:00 Habari
- 21:00 Biko Draw
- 21:05 Aibu Yako! Hata wewe?
- 21:10 Kipindi Maalum : Tanesco
- 21:40 Ripoti Maalum
- 22:15 Telenovela: Destiny (Destino)
- 23:00 Habari
- 23:30 The Base
- 00:30 Al Jazeera
- 02:00 CNN International

**THURSDAY 24 Jan**
- 05:30 Uwanja wa Mazoezi
- 06:00 HABARI
- 06:40 Kumekucha
- 07:30 HABARI
- 08:00 Kumekucha Michezo
- 08:55 Habari za saa
- 09:00 Kumekucha Kishindo
- 09:30 Isidingo
- 09:55 Habari za saa
- 10:00 Watoto wetu
- 10:30 Igizo: Hatua
- 10:55 Habari za saa
- 11:00 Igizo: Hatua
- 11:15 Usafiri wako
- 11:55 Habari za saa
- 12:00 Al jazeera
- 12:30 Ijue Sheria
- 12:55 Habari za saa
- 13:00 Sanaa na wasanii
- 13:30 Jungu Kuu
- 13:55 Habari za saa
- 14:00 Telenovela rpt: Destiny (Destino)
- 14:55 Habari za saa
- 15:00 Meza Huru
- 16:30 Watoto Wetu
- 17:00 The Base
- 18:00 Jiji Letu
- 18:15 Igizo rpt: Damu Nzito
- 19:00 Usafiri wako
- 19:30 Isidingo
- 20:00 Habari
- 21:00 Malumbano ya hoja
- 23:00 Habari
- 23:30 The Base
- 00:30 CNN International

**FRIDAY 25 Jan**
- 05:30 Uwanja wa Mazoezi
- 06:00 HABARI
- 06:40 Kumekucha
- 07:30 HABARI
- 08:00 Kumekucha Michezo
- 08:55 Habari za saa
- 09:00 Kumekucha Kishindo
- 09:30 Isidingo
- 09:55 Habari za saa
- 10:00 Watoto wetu
- 10:30 Hawavumi lakini wamo
- 10:55 Habari za saa
- 11:00 Hawavumi lakini wamo
- 11:20 Usafiri wako
- 11:55 Habari za saa
- 12:00 Al Jazeera
- 12:30 Kipindi Maalum rpt: TCRA
- 12:55 Habari za saa
- 13:00 Kipindi maalum: Tanesco
- 13:30 Ripoti Maalum rpt:
- 13:55 Habari za saa
- 14:00 Mapishi
- 14:15 Telenovela rpt: Destiny (Destino)
- 14:55 Habari za saa
- 15:00 Meza huru
- 16:30 Watoto wetu
- 17:00 The Base
- 17:30 Ibada ya kiislamu
- 18:00 Jiji Letu
- 18:15 Igizo: Mizengwe
- 18:30 Uchumi na biashara
- 19:00 Kipindi maalum: TCRA
- 19:30 Isidingo
- 20:00 Habari
- 21:05 Kipima joto
- 23:00 Habari
- 23:30 The Base
- 00:30 CNN International

**SATURDAY 26 Jan**
- 05:30 Uwanja wa Mazoezi
- 06:00 HABARI
- 06:40 Kumekucha
- 07:00 Habari
- 08:00 Al Jazeera
- 09:00 Watoto wetu
- 10:00 Mjue Zaidi rpt
- 11:00 Jungu kuu rpt
- 11:30 Usafiri wako
- 12:00 Shamba Shape up
- 12:30 Telenovela rpt: Destiny (Destino)
- 14:45 Igizo rpt: Damu nzito
- 15:15 Igizo rpt: Hatua
- 15:45 Igizo rpt: Mizengwe
- 16:00 Igizo rpt: Kimya Milele
- 16:30 Igizo: Mtego rpt
- 17:00 Shamsham za Pwani
- 18:00 Jiji Letu
- 18:15 Mapishi
- 18:30 Igizo: Riziki
- 19:00 Sanaa na wasanii
- 19:30 Jungu Kuu
- 20:00 Habari
- 21:00 Igizo: Kimya Milele
- 21:30 Hawavumi lakini wamo
- 22:30 Isidingo rpt
- 01:00 CNN International

**SUNDAY 27 Jan**
- 05:30 Uwanja wa Mazoezi
- 06:00 HABARI
- 06:40 Kumekucha
- 07:00 Habari
- 08:00 Al jazeera
- 09:00 Watoto Wetu
- 10:00 Isidingo
- 11:45 Aibu Yako
- 11:50 Hawavumi lakini wamo rpt
- 12:50 Bongo Movie rpt: DNA 2
- 14:00 Tamasha la Michezo
- 15:00 Mwangaza
- 16:00 Korean drama: The great queen Seonduk
- 16:45 Mjue zaidi
- 17:30 Kipindi cha kikristo
- 18:00 Jiji Letu
- 18:15 Mapishi
- 18:30 Mizengwe rpt
- 18:45 Matukio ya wiki
- 19:30 Igizo: Mtego
- 20:00 Habari
- 21:00 Biko draw
- 21:05 Mizengwe
- 21:30 3Mzuka
- 22:00 Bongo Movie: Fundi Rama
- 23:15 Telenovela rpt: Destiny (Destino)


5 EATV

LEO USIKU SAA 3:00



IJUMAA
11:00 DADAZ (live)
13:30 Kali Za Wana
14:00 Radio PlanetBongo Live
15:00 Funguka
16:30 #HASHTAG
17:00 5SELEKT
17:55 Kurasa
18:00 eNewz
18:30 Skonga
19:00 EATV SAA 1
21:00 Friday Night Live

FRIDAY NIGHT LIVE (FNL) ni mlipuko wa burudani unaoounganisha EATV na East Africa Radio kukuletea Muziki mnene, burudani ya kupagawisha na mahojiano na wageni wanaoalikwa kutoka ndani na nje ya nchi.

eastafrica RADIO
05:00 EA Breakfast
09:00 Supamix
12:00 Kipenga Xtra
13:00 Planet Bongo
16:00 EA Drive
20:00 Kipenga
21:00 The Cruise

88.1FM DAR ES SALAAM


## RADIO One WEEKLY-SCHEDULE

**MONDAY**

| TIME | PROGRAMME |
|---|---|
| 05.00 AM | HALI YA HEWA / KUMEPAMBAZUKA |
| 06.00 AM | AMKA NA BBC |
| 06.30 AM | NIPASHE |
| 06.50 AM | MATANGAZO |
| 07.00 AM | NEWS BULLETIN |
| 7:10 AM | MATANGAZO |
| 07.15 AM | TAARIFA ZA BARABARANI |
| 07.25 AM | UDONDOZI WA MAGAZETI |
| 07.40 AM | KUMEPAMBAZUKA II |
| 08.00 AM | HABARI NYEPESI |
| 08.10 AM | KUMEPAMBAZUKA III |
| 09.00 AM | HABARI ZA BIASHARA |
| 09.10 AM | MATANGAZO |
| 09.20 AM | BRAND TALK |
| 10.00 AM | NEWS BRIEF |
| 10.03 AM | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 10.10 AM | YALIYOMO YAMO |
| 13.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 13.10 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 13:30 HRS | DJ SHOW |
| 16.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 16.03 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 16.30 HRS | HOJA YA LEO |
| 18.30 HRS | DIRA YA DUNIA BBC |
| 19.30 HRS | SPOTI LEO |
| 20.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 20.10 HRS | RADIO ONE DOCTOR |
| 21.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 21.05 HRS | DAKIKA 45 |
| 22.00 HRS | NEWS BULLETIN (24 HRS) |
| 22.15 HRS | AFRO TIZII |
| 23.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 23.03 HRS | AFRO TIZII |
| 01:00 -03:00HRS | YALIYOMO YAMO ( MARUDIO ) |
| 03:00 - 05:00HRS | DK 45 ( MARUDIO ) |
| 23.00 HRS | |

**TUESDAY**

| TIME | PROGRAMME |
|---|---|
| 05.00 AM | HALI YA HEWA / KUMEPAMBAZUKA I |
| 06.00 AM | AMKA NA BBC |
| 06.30 AM | NIPASHE |
| 06.50 AM | MATANGAZO |
| 07.00 AM | NEWS BULLETIN |
| 7:10 AM | MATANGAZO |
| 07.15 AM | TAARIFA ZA BARABARANI |
| 07.25 AM | UDONDOZI WA MAGAZETI |
| 07.40 AM | KUMEPAMBAZUKA II |
| 08.00 AM | HABARI NYEPESI |
| 08.10 AM | KUMEPAMBAZUKA III |
| 09.00 AM | HABARI ZA BIASHARA |
| 09.10 AM | MATANGAZO |
| 09.20 AM | BRAND TALK |
| 09.30 AM | KUMEPAMBAZUKA SHERIA |
| 10.00 AM | NEWS BRIEF |
| 10.03 AM | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 10.10 AM | YALIYOMO YAMO |
| 13.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 13.10 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 13:30 HRS | DJ SHOW |
| 16.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 16.03 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 16.30 HRS | HOJA YA LEO |
| 18.30 HRS | DIRA YA DUNIA BBC |
| 19.30 HRS | SPOTI LEO |
| 20.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 20.10 HRS | UCHUNGUZI KAMILI |
| 21.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 21.05 HRS | DURU ZETU |
| 22.00 HRS | NEWS BULLETIN (24 HRS) |
| 22.15 HRS | AFRO TIZII |
| 23.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 23.03 HRS | AFRO TIZII |
| 01:00 - 03:00HRS | YALIYOMO YAMO ( MARUDIO ) |
| 03:00 - 05:00HRS | HOJA YA LEO ( MARUDIO ) |

**WEDNESDAY**

| TIME | PROGRAMME |
|---|---|
| 05.00 AM | HALI YA HEWA / KUMEPAMBAZUKA I |
| 06.00 AM | AMKA NA BBC |
| 06.30 AM | NIPASHE |
| 06.50 AM | MATANGAZO |
| 07.00 AM | NEWS BULLETIN |
| 7:10 AM | MATANGAZO |
| 07.15 AM | TAARIFA ZA BARABARANI |
| 07.25 AM | UDONDOZI WA MAGAZETI |
| 07.40 AM | KUMEPAMBAZUKA II |
| 08.00 AM | HABARI NYEPESI |
| 08.10 AM | KUMEPAMBAZUKA III |
| 09.00 AM | HABARI ZA BIASHARA |
| 09.10 AM | MATANGAZO |
| 09.20 AM | BRAND TALK |
| 09.30 AM | KUMEPAMBAZUKA MICHEZO |
| 10.00 AM | NEWS BRIEF |
| 10.03 AM | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 10.10 AM | YALIYOMO YAMO |
| 13.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 13.10 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 13:30 HRS | DJ SHOW |
| 16.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 16.03 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 16.30 HRS | HOJA YA LEO |
| 18.30 HRS | DIRA YA DUNIA BBC |
| 19.30 HRS | SPOTI LEO |
| 20.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 20.10 HRS | UCHUNGUZI KAMILI |
| 21.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 21.05 HRS | DURU ZETU |
| 22.00 HRS | NEWS BULLETIN (24 HRS) |
| 22.15 HRS | AFRO TIZII |
| 23.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 23.03 HRS | AFRO TIZII |
| 01:00-03:00HRS HRS | YALIYOMO YAMO ( MARUDIO ) |
| 03:00 - 05:00HRS | HOJA YA LEO ( MARUDIO ) |

**THURSDAY**

| TIME | PROGRAMME |
|---|---|
| 05.00 AM | HALI YA HEWA / KUMEPAMBAZUKA I |
| 06.00 AM | AMKA NA BBC |
| 06.30 AM | NIPASHE |
| 06.50 AM | MATANGAZO |
| 07.00 AM | NEWS BULLETIN |
| 7:10 AM | MATANGAZO |
| 07.15 AM | TAARIFA ZA BARABARANI |
| 07.25 AM | UDONDOZI WA MAGAZETI |
| 07.40 AM | KUMEPAMBAZUKA II |
| 08.00 AM | HABARI NYEPESI |
| 08.10 AM | KUMEPAMBAZUKA III |
| 09.00 AM | HABARI ZA BIASHARA |
| 09.10 AM | MATANGAZO |
| 09.20 AM | BRAND TALK |
| 09.30 AM | KUMEPAMBAZUKA UKIMWI |
| 10.00 AM | NEWS BRIEF |
| 10.03 AM | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 10.10 AM | YALIYOMO YAMO |
| 13.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 13.10 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 13:30 HRS | DJ SHOW |
| 16.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 16.03 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 16.30 HRS | HOJA YA LEO |
| 18.30 HRS | DIRA YA DUNIA BBC |
| 19.30 HRS | SPOTI LEO |
| 20.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 20.10 HRS | UCHUNGUZI KAMILI |
| 21.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 21.05 HRS | MALUMBANO YA HOJA |
| 23.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 23.03 HRS | AFRO TIZII |
| 01:00-03:00HRS | YALIYOMO YAMO ( MARUDIO ) |
| 03:00-05:00HRS | HOJA YA LEO ( MARUDIO ) |

**FRIDAY**

| TIME | PROGRAMME |
|---|---|
| 05.00 AM | HALI YA HEWA / KUMEPAMBAZUKA I |
| 06.00 AM | AMKA NA BBC |
| 06.30 AM | NIPASHE |
| 06.50 AM | MATANGAZO |
| 07.00 AM | NEWS BULLETIN |
| 7:10 AM | MATANGAZO |
| 07.15 AM | TAARIFA ZA BARABARANI |
| 07.25 AM | UDONDOZI WA MAGAZETI |
| 07.40 AM | KUMEPAMBAZUKA II |
| 08.00 AM | HABARI NYEPESI |
| 08.10 AM | KUMEPAMBAZUKA III |
| 09.00 AM | HABARI ZA BIASHARA |
| 09.10 AM | MATANGAZO |
| 09.20 AM | BRAND TALK |
| 10.00 AM | NEWS BRIEF |
| 10.03 AM | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 10.10 AM | HIZI NAZO |
| 13.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 13.10 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 13:30 HRS | DJ SHOW |
| 16.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 16.03 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 16.30 HRS | HOJA YA LEO |
| 18:30 HRS | DIRA YA DUNIA BBC |
| 19.30 HRS | SPOTI LEO |
| 20.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 20.10 HRS | UCHUNGUZI KAMILI |
| 21.0O HRS | NEWS BRIEF |
| 21.05HRS | KIPIMA JOTO |
| 23.00 HRS | WEEKEND SHOW |
| 01:00 - 03:00HRS | HIZI NAZO ( MARUDIO ) |
| 03:00 - 05:00HRS | HOJA YA LEO ( MARUDIO ) |

**SATURDAY**

| TIME | PROGRAMME |
|---|---|
| 05.00 AM | HALI YA HEWA / KUMEPAMBAZUKA I |
| 06.00 AM | AMKA NA BBC |
| 06.30 AM | NIPASHE |
| 06.50 AM | COMMERCIALS |
| 07.00 AM | NEWS BULLETIN |
| 07.15 AM | NEWSPAPERS REVIEW |
| 07.30 AM | KUMEPAMBAZUKA KISWAHILI |
| 09.00 AM | WATOTO SHOW |
| 10.00 AM | NEWS BRIEF |
| 10.03 AM | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 10.15 AM | MIWANI YA MAISHA |
| 11:00 AM | MTAA WA MAGOMA |
| 13.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 13.10 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 13:30 HRS | CHAGUO LAKO |
| 15:00 HRS | MUZIKI NA MICHEZO |
| 16.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 16.03 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 16.15 HRS | MIDUNDO MOTOMOTO |
| 18:00 HRS | BONGO TEN |
| 19.30 HRS | SPOTI LEO |
| 20.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 20.15 HRS | CHEMSHA BONGO |
| 21.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 21.03 HRS | WEEK END SHOW I |
| 22.00 HRS | NEWS BULLETIN (24 HRS) |
| 22.15 HRS | WEEK END SHOW II |
| 23.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 23.03 HRS | WEEK END SHOW III |
| 01:00-03:00HRS | KISWAHILI ( MARUDIO ) |
| 03:00-05:00HRS | MUZIKI & MICHEZO ( MARUDIO ) |

**SUNDAY**

| TIME | PROGRAMME |
|---|---|
| 05.00 AM | HALI YA HEWA / KUMEPAMBAZUKA I |
| 06.00 AM | AMKA NA BBC |
| 06.30 AM | NIPASHE |
| 06.50 AM | COMMERCIALS |
| 07.00 AM | NEWS BULLETIN |
| 07.15 AM | NEWSPAPERS REVIEW |
| 07.30 AM | KUMEPAMBAZUKA - FAMILIA |
| 10.00 AM | NEWS BRIEF |
| 10.03 AM | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 10.15 AM | SUNDAY SPECIAL |
| 11: 00 HRS | TOP 20 |
| 13.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 13.10 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 13.30 HRS | NANI ZAIDI |
| 16.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 16.03 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 16.30 HRS | MAMBO YA PWANI |
| 18:00 HRS | AFRICAN PANORAMA |
| 19.30 HRS | SPOTI LEO |
| 20.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 20:10 HRS | MBAVU ZANGU |
| 21.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 21.03 HRS | MAMBO MSETO |
| 22.00 HRS | NEWS BULLETIN (24 HRS) |
| 22.15 HRS | RAFIKI I |
| 23.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 23.03 HRS | RAFIKI II |
| 01:00 - 03:00 | FAMILIA ( MARUDIO ) |
| 03:00 - 05:00 HRS | RED CARPET ( MARUDIO ) |

## CAPITAL RADIO

### CAPITAL RADIO 2017 101.3 FM
### FAHARI YA MSIKILIZAJI/THE LISTENERS PRIDE

**MONDAY**
- 05:00-09:00HRS MORNING JAM
- 09:00-13:00HRS LETE RAHA
- 13:00-14:00HRS DW-RADIO
- 14:00-16:00HRS CLUB 101
- 16:00-18:00HRS DALA DALA
- 18:00-18:10HRS HABARI
- 18:10-20:00HRS BOZOUK TIME
- 20:00-21:00HRS HALI HALISI
- 21:00-22:00HRS SPORTS
- 22:00-01:00HRS LADHA LAINI

**TUESDAY - FRIDAY**
- 05:00-09:00HRS MORNING JAM
- 09:00-13:00HRS LETE RAHA
- 13:00-14:00HRS DW-RADIO
- 14:00-16:00HRS CLUB 101
- 16:00-18:00HRS DALA DALA
- 18:00-18:10HRS HABARI
- 18:10-21:00HRS BOZOUK TIME
- 21:00-21:30HRS SPORTS
- 21:30-01:00HRS LADHA LAINI
- 01:00-05:00HRS MUSIC & JINGLES

**SATURDAY**
- 05:00-07:30HRS MUZIKI
- 07:30-09:00HRS DK 90 DUNIANI
- 09:00-10:00HRS MUZIKI
- 10:00-12:00HRS KADOGOO
- 12:00-13:00HRS BONGO HITS 1
- 13:00-14:00HRS DW RADIO
- 14:00-15:00HRS BONGO HITS 2
- 15:00-16:00HRS ZAIDI YA UMJUAVYO
- 16:00-18:00HRS THE SPLASH
- 18:00-21:00HRS LAID BACK
- 21:00-21:30HRS SPORTS
- 21:30-01:00HRS AK 47 LIVE
- 01:00-05:00HRS MUSIC

**SUNDAY**
- 05:00-07:30HRS MUZIKI
- 07:30-09:00HRS GOSPEL MUSIC
- 09:00-11:00HRS THE SUNDAY
- 11:00-13:00HRS TOP TWENTY
- 13:00-14:00HRS DW RADIO
- 14:00-15:00HRS CAPITAL MICHEZONI
- 15:00-16:00HRS UKURASA WA MBELE
- 16:00-18:00HRS UNLIMITED REQUEST
- 18:00-21:00HRS JIACHIE
- 21:00-21:30HRS SPORTS
- 21:30-01:00HRS LADHA LAINI

## HABARI KIMATAIFA

# Tshisekedi aapishwa rais mpya wa DRC

**KINSHASA,** DRC

KIONGOZI wa chama cha upinzani Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), Felix Tshisekedi, jana aliapishwa kuwa rais mpya wa nchi hiyo.

Tshisekedi mwenye umri wa miaka 55, mtoto wa marehemu, Icon Etienne, aliyekuwa mwasisi wa upinzani, aliapishwa kushika madaraka katika Kasri ya Wananchi, ambako liko Bunge la Taifa katika mji mkuu wa Kinshasa.

Shughuli ya kuapishwa kwa Tshisekedi ilifanyika katika Ikulu ya Rais mjini Kinshasa majira ya saa sita kamili kwa saa za Congo.

Tshisekedi amechukua mikoba ya uongozi kutoka kwa Rais Kabila, ambaye sasa akiwa na umri wa miaka 47, ameitawala Congo kwa miaka 18, baada ya kumrithi marehemu baba yake Laurent-Desire Kabila, aliyeuliwa mwaka 2001.

**Shughuli ya kuapishwa kwa Tshisekedi ilifanyika katika Ikulu ya Rais mjini Kinshasa majira ya saa sita kamili kwa saa za Congo.**

Wafuasi wake ambao kwa miongo kadhaa walimuunga mkono Tshisekedi katika kutafuta madaraka walijitokeza katika mtaa huo wakiwa na bendera zilizo kuwa zimepachikwa kwenye nywele zao, huku wengine wakiwa wamevaa kofia zenye picha ya chui.

Wakongo wengi wanamatumaini kuwa Tshisekedi ataleta mabadiliko baada ya miaka 18 ya utawala wa Rais Joseph Kabila, ambaye katika hotuba yake ya mwisho Jumatano usiku alihimiza nchi iungane katika kumuunga mkono kiongozi huyo.

Kwenye hotuba hiyo Kabila alisema kuwa anaachia madaraka bila masikitiko yoyote.

Hotuba hiyo iliyoonyeshwa moja kwa moja katika televisheni ya taifa RTNC, Rais Kabila alisema hataiendea kinyume katiba ya nchi hiyo.

"Kwa kuheshimu katiba nitakabidhi madaraka pasipo kuwa na majuto wala kutubu kwa sababu licha ya upungufu unaotokana na kazi zote za mkono wa binadamu, Congo imetoka mbali na imepiga hatua kubwa na leo iko katika msingi imara," alisema Rais Kabila.

Katika hotuba hiyo ambayo ilikuwa ya kwanza tangu uchaguzi uliofanyika Desemba 30 mwaka uliopita, Rais Kabila pia alitoa wito wa umoja wa kitaifa akitaka kuundwa kwa muungano wa vyama mbalimbali vya kisiasa, ambao utawakabili wale ambao wameungana na watakaojaribu kila mara kushirikiana kumiliki na kujinufaisha na rasilimali za Congo.

Hata hivyo, Tshisekedi ni lazima afanye kazi na bunge ambalo lina wabunge walio wengi wa chama tawala cha Kabila. **VOA**



Felix Tshisekedi akiwa ameshika Katiba ya Congo baada ya kuapishwa jana, kuwa Rais wa nchi hiyo. **PICHA: ALLIANCE**

## Marekani yataka waandamanaji kuachiwa huru

**KHARTOUM,** Sudan

MAREKANI imetoa wito kwa serikali ya Sudan kuanzisha uchunguzi wa watu waliouawa katika maandamano yaliyozuka hivi karibuni nchini humo na kutaka kuwaachiliwa huru waandamanaji wanaozuiliwa.

Marekani imetoa kauli hiyo ikisema kuna uwezekano wa kurejesha uhusiano mzuri kati ya Khartoum na Washington.

Taarifa ya Wizara ya Mambo ya Kigeni ya Marekani ni ya kwanza tangu kuanza kwa maandamano nchini Sudan Desemba 19.

Maandamano hayo yalizuka kufuatia uamuzi wa serikali wa kuongeza mara tatu bei ya mkate. Maandamano ambayo yalibadili mwelekeo na kuwa maandamano dhidi ya utawala wa Rais Omar al-Bashir, ambaye anaongoza nchi hiyo kwa mkono wa chuma tangu mapinduzi ya kijeshi ya mwaka 1989.

Kwenye taarifa hiyo Marekani ilisema ina wasiwasi na idadi kubwa ya watu wanaokamatwa na kufungwa nchini Sudan.

"Pia tunatoa wito kwa serikali kuruhusu uchunguzi wa kuaminika na huru kwa watu waliouawa na waliojeruhiwa wakati wa waandamanaji," ilieleza taarifa hiyo iliyotolewa na msemaji wa Wizara ya Mambo ya Kigeni ya Marekani, Robert Palladino.

Ilieleza kuwa serikali ya Sudan inapaswa kushughulikia malalamiko ya wananchi pia inapaswa kujenga mazingira salama kwa kuweka mbele uhuru wa kujieleza na mazungumzo na upinzani pamoja na mashirika ya kiraia. **RFI**

## 19 kuwania urais Comoro

**MORONI,** Comoro

WAGOMBEA 19 wamejiandikisha kushindana na Rais anayeondoka madarakani, Azali Assoumani, nchini Comoro katika uchaguzi unaotarajiwa kufanyika Machi 24 mwaka huu.

Kati ya wagombea hao ni wagombea watano tu katika kinyang'anyiro hicho wanaungwa mkono na vyama katika taifa hilo la visiwa lililoko katika bahari ya Hindi.

Comoro ni miongoni mwa nchi ambayo iliingia katika makubaliano ya kubadilishana madaraka miongoni mwa visiwa vitatu vya nchi hiyo yalisaidia kukomesha upinzani na mapinduzi katika miaka ya mwisho ya 1990.

Wagombea wengine 15 wanagombea nafasi ya urais ni wagombea binafsi, kwa mujibu wa orodha iliyotolewa na tume huru ya uchaguzi nchini humo CENI.

Taarifa zaidi zinaeleza kuwa upinzani nchini humo umevurugika baada ya wapinzani wengi kukamatwa.

Mahakama ya usalama imetoa hukumu ya kifungo kwa wanasiasa wengi ambao wanapinga kura ya maoni kumruhusu Azali kujiongezea muda wake madarakani. **DW**

# Venezuela yakumbwa na mgogoro

**CARACAS,** Venezuela

NCHI ya Venezuela imeingia katika mgogoro mkubwa wa kisiasa baada ya kiongozi wa upinzani Juan Guaido kujitangaza kuwa kaimu rais kama njia ya kumwondoa madarakani Rais Nicolas Maduro.

Kiongozi wa upinzani nchini humo, Juan Guaido, ambaye pia ni Spika wa Bunge ameishangaza dunia kwa kujitangaza kuwa ni kaimu rais wa nchi hiyo.

Hatua hiyo imeigawanya jumuiya ya kimataifa ikiwamo Marekani na nchi nyingine kadhaa ambazo zinamuunga mkono Guaido, huku nchi ya Urusi ikilaani Marekani kwa hatua ya kuingilia masuala ya Venezuela.

Maduro amekuwamo madarakani tangu alipopata ushindi wa utatanishi katika uchaguzi uliofanyika mwaka 2013 baada ya kifo cha Rais Hugo Chavez.

Lakini jana kiongozi wa upinzani, Guaido alijitangaza kuwa Rais wa muda na kuungwa mkono na Marekani, Brazil, na nchi kadhaa za Amerika ya Kati.

Rais wa Baraza la Umoja wa Ulaya, Donald Tusk, alitoa wito wa kuheshimiwa kwa uamuzi wa wananchi na kueleza kuwa njia bora ni kufanya uchaguzi.

Serikali ya Ujerumani ilieleza kuwa Bunge la Venezuela lina dhima mahususi katika kuleta mustakabali huru wa nchi yao.

Rais Maduro anayepingwa na kiongozi wa upinzani aliapishwa kutumikia muhula wa pili baada ya uchaguzi wa utatanishi uliofanyika mwezi Mei mwaka jana, uliosusiwa na wapinzani ambao walisema haukuwa wa haki.

Jana, waandamanaji waliokadiriwa kufikia maelfu walijitokeza barabarani nchini Venezuela kumtaka Rais Maduro ajiuzulu. Katika maandamano hayo watu 13 waliuawa.

Vyombo vya habari nchini Venezuela viliripoti kuwa gesi ya kutoa machozi ilitumiwa katika kuwakabili waandamanaji hao.

Wachambuzi wa masuala ya kisiasa wanaeleza kuwa tangu kuanza kwa migogoro ya kisiasa na kiuchumi nchini Venezuela watu wapatao milioni tatu wameikimbia nchi hiyo.

Rais Maduro bado anaungwa mkono na nchi za Urusi, Uturuki, China, Bolivia na Cuba. **DW**

# Mshtakiwa utakatishaji fedha kuhojiwa mahabusu

**Na Hellen Mwango**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam, imekubali upande wa Jamhuri kwenda mahabusu kumhoji mshtakiwa wa pili, Alloycious Mandago, anayekabiliwa na kesi ya kuisababishia serikali hasara ya Sh. bilioni mbili.

Maombi hayo yaliwasilishwa jana mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Huruma Shaidi.

Wakili wa Serikali, Leonard Swai, alidai kuwa kesi hiyo ilipangwa kwa ajili ya kutajwa lakini upande wa Jamhuri unaomba kibali cha kwenda kumhoji mshtakiwa wa pili.

"Tuko katika hatua za mwisho za kukamilisha upelelezi wa Jamhuri, tunaomba kibali cha kwenda kumhoji mshtakiwa Mandago ili tukamilishe na baadaye tuwasomee washtakiwa maelezo ya mashahidi," alidai Swai.

Hakimu Shaidi alisema mahakama imeridhia Jamhuri kwenda kumhoji mshtakiwa huyo na kesi hiyo itatajwa Februari 8, mwaka huu.

Mbali na Mandago washtakiwa wengine katika kesi hiyo ni mfanyabiashara Mohamed Yusuali, Isaack Kasanga, Taherali Sujjauddin Taherali na Mohamed Seif ambao wanakabiliwa na mashtaka 39 likiwamo la kuisababishia serikali hasara ya Sh. bilioni mbili.

Washtakiwa hao wanadaiwa kuwa kati ya Machi 2, 2010 na Aprili 26, 2016 katika maeneo tofauti ndani ya Jiji la Dar es Salaam, walikula njama kwa kugushi, kukwepa kulipa kodi na kutakatisha fedha.

Katika shtaka la pili linalomkabili Kassanga, inadaiwa kuwa katika ofisi za Wakala wa Usajili wa Majina na Leseni za Biashara (Brela) zilizoko manispaa ya Ilala, aliwasilisha nyaraka za uongo yenye fomu namba 128 ya Mei 2, 2016 akionyesha kuwa Machi 4, 2012 wakurugenzi wa kampuni ya Superior Financing Solutions Limited ni Mohamed Mustafa Yusufali , Isaack Kassanga na Maria Barnett.

Katika shtaka lingine la utakatishaji fedha kinyume cha sheria linalowakabili washtakiwa wote, inadaiwa kati ya Machi 4, 2011 na Aprili 13, 2016 katika maeneo tofauti ndani ya mkoa wa Dar es Salaam, wakiwa wamiliki na Mkurugenzi wa kampuni ya Superior Financing Solutions Limited, walijihusisha na muamala wa Sh. 2,967,959,554 huku wakijua fedha hizo zinatokana na zao la pesa haramu.



Mkuu wa Kitengo cha Mikopo Benki ya Stanbic Tanzania, Daniel Mbotto (watatu kulia), akipeana mkono na meneja wa kituo cha mahabusu ya watoto Upanga wakati wa makabidhiano ya hati ya malipo yenye thamani ya Shilingi milioni moja, iliyotolewa na benki hiyo kwa ajili ya ujenzi wa mfumo wa maji taka kituoni hapo. Wengine ni Mkurugenzi wa Kampuni ya EGOM Investment Co. Limited, Fikiri Mnyenyelwa (katikati) na wafanyakazi wa benki ya Stanbic. **NA MPIGAPICHA WETU**

# Pepsi yaja na 'kubwa lao'

**Na Mary Geofrey**

KAMPUNI ya vinywaji baridi ya SBC inayozalisha Pepsi, Mirinda na 7up, imezindua muundo mpya wa chupa wenye ujazo wa mililita 500 ijulikanayo kama 'kubwa lao' zitakazouzwa kwa Sh. 600.

Meneja Mafunzo na Uzalishaji wa SBC, Rashid Chenja, alitangaza uzinduzi wa chupa hizo jana, jijini Dar es Salaam na kumtangaza balozi wa mwaka mmoja wa bidhaa hizo msanii wa muziki wa kizazi kipya, Nassib Abdul, maarufu Diamond Platnumz.

"Kazi yetu ni kuburudisha, tulitaka kuwaletea chupa inayoburudisha zaidi. Chupa hii imeundwa kwa kutumia teknolojia za kisasa na kuipa mwonekano unaovutia zaidi wakati ikiwa ni nyepesi zaidi hata kuliko chupa za kawaida za milimita 350. Tulitaka kuizindua kwa mara ya kwanza katika soko la Afrika Mashariki," alisema.

Alisema jambo la muhimu walilolenga ni kuwafurahisha, kuwaburudisha na kuwapa bei nafuu wateja wao kwa kile wanachokipenda.

"Tumeipa chupa hii jina hili kwa sababu ina ujazo mkubwa kuliko zote nyingine katika soko. Tumeiita hivi kwa sababu pamoja na ukubwa, unapata burudani na bei nafuu zaidi," alisisitiza Chenja.

Alisema waliona vyema uzinduzi huo wa mkubwa wao kwenda sambamba na msanii maarufu wa ndani na nje ya nchi ili kuburudisha zaidi watumiaji wa bidhaa hiyo.

"Diamond Platnumz ameonyesha kwamba amefurahi kujihusisha na Pepsi pamoja na Mirinda hasa uzinduzi wa chupa hii mpya ya glasi yenye ujazo wa mililita 500. Pia ameonyesha ataendelea kushirikiana nasi kuendelea kuwaburudisha Watanzania," alisema.

Alisema kwa sasa wameanza uzinduzi jijini Dar es Salaaam na baadaye wataelekea Mkoa wa Mwanza na maeneo mengine nchini.

Kwa upande wake Diamond aliahidi kuendelea kuwa balozi mzuri na kuhakikisha watumiaji wa bidhaa hizo wanapata burudani na kinywaji cha uhakika kilicho katika ujazo na chupa nyepesi.

# Tamwa yahamasisha habari za kupinga mila kandamizi

**Na Hellen Mwango**

WAANDISHI wa habari nchini, wamehamasishwa kuonyesha na kuandika habari na picha zinazopinga mila kandamizi za wanawake na watoto, ili kuzitokomeza.

Rai hiyo ilitolewa jijini Dar es Salaam na Mkurugenzi Msaidizi wa Chama cha Wanahabari Wanawake Tanzania ((Tamwa), Davis Lumala, katika uzinduzi wa maonyesho ya upigaji picha za habari ya 2018.

Aliwataka waandishi watumie taaluma ya picha kutoa elimu kwa jamii kupitia matukio mbalimbali yanayoirudisha nyuma jamii.

"Waandishi wa Tanzania wajitahidi kuonyesha na kuandika habari picha zinazotokana na mila kandamizi kwa wanawake na watoto, Tamwa ni miongoni mwa washiriki tunaoonyesha picha za watoto na wanawake katika maonyesho haya," alisema Lumala kwa niaba ya Mkurugenzi Mtendaji wa Tamwa Rose Reuben.

Naye Mratibu wa maonyesho hayo, Sophie Boshouwers, alisema maonyesho hayo yaliyoandaliwa na Ubalozi wa Ufalme wa Uholanzi kwa kushirikiana na Tamwa, yataonyesha picha za waandishi wa habari walioshinda kwenye shindano la 'World Press Photo' la 2018.

Alisema maonyesho ya mwaka huu ni muhimu sana kwa Tanzania kwa sababu moja ya hadithi za picha zilizoshinda zilipigwa visiwani Zanzibar na Anna Boyiazis.

Alisema shindano la 2018 lilishirikisha wapigapicha mbalimbali duniani 4,548 kutoka nchi 125 na kwamba waliwasilisha picha 73,044.

"Februari mosi, Voice na Tamwa wataandaa majadiliano ya wazi kuhusu upigaji picha za habari Afrika Mashariki, watachangia uzoefu wao na mawazo yao," alisema Boshouwers.

Alisema mradi huo unalenga kuwapa fursa watu wenye vipaji vya kupiga picha kutoka kila bara, nafasi ya kuonyesha kazi zao kupitia jukwaa hilo.

ITV

**KIPIMA JOTO: SAA 3:05 USIKU**

KATIKA KIPINDI HIKI KINACHOKUJIA MUBASHARA KUTOKA STUDIO FUATILIA MADA YA LEO "KUIBUKA KWA UCHINJAJI HOLELA WA MIFUGO NA KUHATARISHA AFYA ZA WALAJI. JE, MAMLAKA HUSIKA ZINAWAJIBIKA IPASAVYO KUDHIBITI TATIZO HILO?". WATAZAMAJI MNAKARIBISHWA KUPIGA SIMU NA KUULIZA MASWALI AU KUTOA USHAURI KWA JOPO LETU.

# TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## HUDUMA MBALIMBALI

**MKOPO WA HARAKA NA NAFUU** Pata mkopo wa dharura ndani ya siku 2. Kwa wafanyakazi na Wafanyabiashara kutoka ENTERPRISE FINANCE LIMITED (EFL). Kwa mawasiliano Zaidi piga: 0768 928516 / 0653 258662. KARIBU EFL.


## NIPASHE NI JIBU LAKO

NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0767 223311


## CHETI KIMEPOTEA



**DENIS P. MALONGO** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.1925-0137** kilichotolewa na **NGOKOLO SEKONDARI** mwaka 2015.

**Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi.**

**Taarifa ya polisi: SHY/RB/8136/018.**

115024301

## KUPOTEA KWA CHETI




**Athumani B. Mkubwa** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye **index namba S.2879/0053,** kilichotolewa na shule ya Sekondari Kidete mwaka 2015. Yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.

Polisi Taarifa: **KGD/RB/1029/2019**

115023502

## KUPOTEA KWA CHETI



**Fratern Ambrose Sawacky** anatangaza kupotelewa na cheti cha Ualimu chenye **index namba E.506/257** kilichotolewa na Chuo cha Ualimu Marangu, mwaka 2003 mkoani Kilimanjaro. Yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.

Polisi Taarifa: **AR/RB/647/2019**

115023402

## KUMBUKUMBU YA MAREHEMU BABA YETU FAUSTINE PETER NYAKI



Leo umetimiza **miaka 19** tangu ututoke ghafla alfajiri ile ya tarehe **25/01/2000** Magumu na shida tunayapata kila tunapokukumbuka lakini tunajua haya ni ya muda tuu kwani hakika Mungu ni mwema na yupo nasi siku zote.

Baba tutaendelea kukukumbuka Daima

***Amina***

115021802

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**Florah Martin Kasanga** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye usajili wa namba **T307 BWU** aina ya TOYOTA STARLET. Yenye chasis namba **EP910359038,** engine namba **4EFE1477.** Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. Polisi Taarifa: **KJN/RB/525/2019**

115022902

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika mahakama ya mwanzo**

**MJINI MOROGORO**

**Usimamizi wa mirathi No.17/2019**

**Ombi la THERESIA JOHN WAHINDI Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu TELESPHORY MICHAEL MKOBA**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 04/02/2019 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia ya marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 22/01/2019

215023802

**IN THE COURT OF DISTRICT DELEGATE OF DODOMA**

**AT DODOMA**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO…80.. OF 2018**

**In the matter of the Estate of the late OSCAR GERALD LUKOSI of Isanga within Dodoma Region.**

**AND**
**In the matter of the Application for letters of Administration by EDINA PASCHAL JOSEPH**

**GENERAL CITATION**

***RULE 75 OF PR0BATE RULES GN 369 OF 1963)***

**ALL PERSONS** claiming to have any interest in the Estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of administration is made to the above named petitioners.

Objections to the grant should be filled on or before the 7th Day of February 2019
Dated at Dododma this 29th day of November 2018

………………………………………………
**PETITIONER**

21502402

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**METHOD MARTIN KILASARA** Amepotelewa na kadi ya gari aina ya **TOYOTA HILUX** Yenye usajili wa namba **T 941 AKH.** Yenye chasis namba **RN450020115** na injini namba **RR3013574.** Yeyote atakaeiona atoe taarifa Kituo chochote cha polisi RB namba **MOR/TR/RB/45/2019.**

215023902

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**JSP MARKETING LINK LTD** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya **MITSUBISH FUSO** yenye namba za usajili **T 614 DPJ.** Chassis namba **FM65FNB00146.** Engine namba **6M60076732.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **KJN/RB/534/2019.**

115024502

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**JSP MARKETING LINK LTD** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya **MITSUBISH FUSO** yenye namba za usajili **T 612 DPJ.** Chassis namba **FM65FNB10140.** Engine namba **6M60100740.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **KJN/RB/534/2019.**

115024702

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**KONOIKE CONSTRUCTION COMPANY LTD** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili T 475 AKQ NISSAN. CHASSIS NO; CWA45HDNT03275. ENGINE NO; 101513T.

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

**Taarifa ya polisi: KJN/RB/BI/I/VOLIV/1290/2019.**

115023702

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**JUMA ATHUMANI MHANDO** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya TOYOTA NOAH yenye namba za usajili **T. 889 DGL.**

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

**Taarifa ya polisi: OB/RB/1791/19.**

115024402

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**Msimbe Pius Msimbe** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye usajili namba **T673 CHU** aina ya **ALTEZA.** Yenye chasis namba **JTDBJI19260091367.** Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.

Polisi Taarifa: **CID/TR/RB/0324/2018**


115023002


***Uza,***
***Chenye Thamani Kubwa***
***Kwa Kutangaza Nasi***
***Kwa Bei Poa***
***Tupigie***
***0767 223311***

***Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku***

***Tupigie 0767 223 311***

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.



# MAMBO 10 USIYOYAJUA YA OLIVER MTUKUDZI 'TUKU'

**HARARE,** Zimbabwe

KIBAO chake cha Neria ambacho pia kilitumika katika filamu ya Neria iliyotoka mwaka 1993 iliyoongozwa na Goodwin Mawuru na kuandikwa na Tsitsi Dangarembga, ndio haswa kilichomtambulisha mwanamuziki, Oliver Mtukudzi maarufu kama Tuku kwenye macho na masikio ya Watanzania wengi.

Lakini sasa nguli huyu wa muziki kutoka nchini Zimbabwe, hatutamuona tena, kwani alifariki dunia Januari 23 mwaka huu kwenye Hospitali ya Avenues Clinic, iliyopo jijini Harare baada ya kuugua kwa muda mrefu. Amefariki akiwa na umri wa miaka 66.

Awali katika shughuli zake za muziki, Mtukudzi amekuwa akifanya ziara mbalimbali kabla ya kuanza kuugua.

Hivi karibuni alilazimika kuahirisha baadhi ya ziara zake za muziki katika mataifa kadhaa duniani kutokana na kuugua kwake.

Mtukudzi atakumbukwa kwa aina yake ya muziki ya mtindo wa Afro-Jazz uliovuka mipaka na kupata mashabiki wengi kote duniani.

Alipata umaarufu nchini Zimbabwe kabla ya nchi hiyo kupata uhuru mwaka 1980 alipojiunga katika jeshi na muimbaji mwenza wa Zimbabwe anayeishi Marekani, Thomas Mapfumo kwa lengo la kupaza sauti ya mapinduzi wakati ambapo nchi hiyo ilikuwa ikikaliwa na wakoloni chini ya Serikali ya Mwingereza, Ian Smith.

Mtukudzi amekuwa katika fani ya muziki kwa zaidi ya miongo minne, na amefanikiwa kutoa albamu 67 huku albamu yake ya mwisho ikihusika zaidi na hali ya kisiasa ya sasa iliyoko Zimbabwe na matatizo ya kijamii.

Nyota huyo alikuwa akipewa heshima ya muziki wa Afrika kama ilivyo kwa wasanii, Hugh Masekela, Steve Dyer, Miriam Makeba, Yousssou N dour, Angelique Kidjo, Yvonne Chaka Chaka na Lady Smith Black Mambazo.

Wengi wanamfahamu kutokana na umahiri wake mkubwa katika medani ya muziki, utambulisho wake mkubwa ukiwa ni sauti yake nzito na ya kipekee.

Nyimbo zake zinazohamasisha amani na kutoa burudani barani Afrika, zimesababisha yeye kutumika kama alama katika taifa hilo hususan kwa upande wa sanaa ya nchini mwake.

## MAMBO 10 USIYOYAJUA KUHUSU TUKU

Mtukudzi au alizaliwa Septemba 22, mwaka 1952 katika kitongoji cha Highfield jijini Harare.

Alianza kutambulika zaidi kimuziki baada ya kuingia katika Kundi la Wagon Wheels mwaka 1977 akiwa na wenzake kadhaa, akiwamo Thomas Mapfumo.

Wimbo wake wa kwanza ulikuwa wa 'Dzandimomotera' ulioheshimika mno na hapo ndipo Tuku alipotoka na albamu yake ya kwanza iliyomletea mafanikio makubwa zaidi.

Aidha, Mtukudzi pia ni mmoja wa wanakundi la Mahube, kundi la muziki la nchi ya Afrika Kusini.

Ni baba wa watoto watano na mpaka sasa ana wajukuu wawili. Watoto wawili kati ya hao ni wanamuziki. Oliver ana dada zake wanne. Kaka yake alikwishafariki.

Tuku hufurahia zaidi kuogelea katika bwawa lake (swimming pool) ambalo lina umbo la gitaa.

Ameshinda tuzo nyingi mno hata nyingine hawezi kuzikumbuka.

**Mtukudzi amekuwa akidaiwa mara kwa mara kwamba ni mwathirika wa ugonjwa wa Ukimwi, ingawa mwenyewe amekuwa akikanusha vikali madai hayo.**

Mwanamuziki huyo amekwishatunukiwa tuzo ya tatu iliyobeba heshima ya udaktari kutokana na kuwa mshauri na balozi mzuri wa muziki.

Mwaka 2003 alitunukiwa tuzo kubwa ya heshima na Chuo Kikuu cha Zimbabwe kwa kutambua miongo kadhaa ya mchango wake na kujitolea katika kujenga muziki na msukumo kwa wasanii wa kizazi kipya nchini humu, huku akionyesha ushawishi kwenye kazi za wasanii hao.

Mwaka 2009, Chuo Kikuu cha Wanawake cha Afrika, kilimpatia tuzo ya shahada ya sanaa na kumwelezea mwanamuziki huyo kama mbunifu wa hali ya juu kuwahi kutokea nchini Zimbabwe katika kipindi cha miongo mitatu iliyopita.

Wengi wanamfahamu Mtukudzi kutokana na umahiri wake mkubwa katika medani ya muziki, utambulisho wake mkubwa ukiwa ni sauti yake nzito na ya kipekee.

Licha ya Tuku kuwa mwanamuziki, pia ni mfanyabiashara, mwanaharakati wa haki zabinadamu na balozi wa UNICEF Kusini mwa Bara la Afrika.

Mara nyingi Tuku huimba nyimbo katika lugha tatu tofauti za Kishona, Kindebele na Kiingereza.

Huchanganya ala za muziki wa kiasili kwenye nyimbo zake, jambo lililompa umaarufu mkubwa dunia nzima.

Tofauti na wenzake katika Kundi la Wagon Wheels waliokuwa wakimuimba vibaya Rais wa zamani wa nchi hiyo, Robert Mugabe, Mutukudzi alikuwa akimsifia na kusababisha anufaike kwa misaada mbalimbali kutoka serikalini.

Mwaka 2010, mwanae kipenzi, Sam Mtukudzi, ambaye naye alikuwa mwanamuziki, alifariki dunia kutokana na ajali mbaya ya gari.

Mtukudzi amekuwa akidaiwa mara kwa mara kwamba ni mwathirika wa ugonjwa wa Ukimwi, ingawa mwenyewe amekuwa akikanusha vikali madai hayo.

Kati ya wasanii wenzake waliokuwa wakiunda kundi la Wagon Wheels, ni yeye pekee aliyebaki hai hadi kifo kumkuta hapo juzi. Wenzake wote walikufa kwa ugonjwa wa Ukimwi.

Hivi karibuni, mashabiki wake nchini humo walipatwa na mshangao mkubwa baada ya kitabu kiitwacho 'Tuku Backstage' kuvuja kikiwa na kashfa nyingi za ngono zinazomhusu gwiji huyo, mwandishi akiwa ni Shepherd Mutamba.

Baadhi ya albamu za mwanamuziki huyo ni 'Ndipeiwo Zano' ya mwaka 1978, ikarudiwa tena mwaka 2000, 'Chokwadi Chichabuda' na 'Muroi Ndiani?' za mwaka 1979, 'Shanje' na 'Pfimbi' za mwaka 1981, 'Nhava' ya mwaka 2005, 'Wonai' ya 2006, 'Tsimba Itsoka' na nyingine nyingi.

Mtukudzi katika maisha yake ameoa mara mbili, mke wake wa kwanza ni Melody Murape aliyemuoa mwaka 1979 na ndoa yao ikadumu hadi mwaka 1993 na mke wake wa pili ni Daisy Mtukudzi.

HABARI MICHEZO

# REAL MADRID KLABU TAJIRI ZAIDI DUNIANI

**MADRID,** Hispania

REAL Madrid imeipiku Manchester United na kuwa klabu tajiri zaidi duniani ikiwa imeingiza kiasi cha euro milioni 750 kwa msimu wa 2017/18.

Mabingwa hao wa Ulaya wameshika nafasi ya kwanza kwa mujibu wa Kampuni ya Deloitte Money League ikiwa ni mara ya 12 kwa kipindi cha miaka 22, huku mpinzani wake katika soka la Hispania, Barcelona pia ikiipita United na kushika nafasi ya pili ikiwa imeingiza kiasi cha euro milioni 690.

United wameshuka katika orodha hiyo baada ya kufanya vibaya kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa msimu uliopita, ikishika nafasi ya tatu kwa kuingiza kitita cha euro milioni 660, iikiwa ni ongezeko la asilimia 2%.

Mashetani wekundu hao waliongoza kwenye orodha hiyo mwaka jana, lakini wamebakia kuwa ndio timu inayoingiza mapato makubwa zaidi kwa England.

Bado Ligi Kuu ya England imetawala kwenye 20 bora, huku ikiwa na klabu tisa.

Katika orodha hiyo, Manchester City imeendelea kubakia nafasi ya tano ikiwa na euro milioni 568.4.

Liverpool wapo nafasi ya saba kwa kuingiza euro milioni 513.7, Chelsea nafasi ya nane (euro 505.7), nafasi ya tisa imekwenda kwa Arsenal (euro milioni 439.2) na Tottenham nafasi ya 10 (euro 428.3).

Everton, Newcastle na West Ham pia zipo kwenye orodha hiyo ya 20 bora.

**Orodha kamili ya 20 bora ni hii:**

Real Madrid (euro mil. 750.9), Barcelona (euro mil. 690.4), Manchester United (euro mil. 666), Bayern Munich (euro mil. 629.2), Manchester City (euro mil. 568.4), Paris Saint-Germain (euro mil. 541.7), Liverpool (euro mil. 513.7), Chelsea (euro mil. 505.7), Arsenal (euro milm 439.2), Tottenham (euro mil. 428.3), Juventus (euro mil. 394.9, Borussia Dortmund (euro mil. 317.2), Atletico Madrid (euro mil. 303.4), Inter (euro mil. 280.8), AS Roma (euro mil. 250), Schalke 04 (euro mil. 243.8), Everton (euro mil. 212.9), AC Milan (euro mil. 207.7), Newcastle United (euro mil. 201.5), West Ham United (euro mil. 197.9).




# AC Milan wakamilisha usajili wa Krzysztof Piatek

**MILAN,** Italia

AC Milan imekamilisha usajili wa Krzysztof Piatek kutoka Genoa kwa ada ya uhamisho inayoaminiwa kuwa ni euro milioni 35.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Poland ameondoka Genoa baada ya kuitumikia kwa kipindi cha miezi sita na amesaini mkataba wa miaka mitano wa kukaa hapo San Siro hadi mwaka 2023.

Piatek alikuwa akivutiwa na klabu kubwa Ulaya, baada ya kufunga mabao tisa katika mechi saba za kwanza alizoichezea Genoa, akifunga angalau bao moja katika kila mechi.

Aliichezea timu yake ya taifa kwa mara ya kwanza Septemba, mwaka jana, akifunga kwenye mchezo wake wa kwanza wa mashindano dhidi ya Ureno.

Pia alifunga mabao yote manne kwa Genoa wakati wakiwafumua Lecce katika mchezo wa raundi ya tatu ya Kombe la Coppa Italia Novemba mwaka jana.

Anaondoka klabuni hapo baada ya kufunga jumla ya mabao 19 katika mechi 21 akiwa na wastani wa kufunga bao moja kila baada ya dakika 93.

Ada iliyolipwa kwa Piatek imeongezeka kwa asilimia 775% kutoka ile ya euro milioni 4 ambayo Genoa walilipa kwa KS Cracovia, wakati wakimnunua kipindi cha majira ya joto kilichopita.

Mshambuliaji huyo atarithi mikoba ya Gonzalo Higuain hapo Milan, baada ya nyota huyo wa kimataifa wa Argentina kujiunga na Chelsea, ambaye amekwenda kuchukua nafasi ya Alvaro Morata, anayetarajiwa kusaini Atletico Madrid.

Kama ilivyo kwa Piatek, Higuain hakuwapo kwenye mchezo wa Milan wa Serie A dhidi ya Genoa Jumatatu, kwa sababu kocha, Gennaro Gattuso, alihisi kwamba hakuwa kwenye saikolojia nzuri ya kucheza.

Akiwa na mabao sita kwenye mechi 15 alizoichezea Milan, hakuwa suluhisho la kupatikana kwa mabao kwa timu hiyo.

Ada ya Piatek imeweka rekodi kwa Genoa na kuipita ile ya euro milioni 28 waliyolipa Inter Milan kwa ajili ya kumsajili Diego Milito mwaka 2009.




# Barcelona yamsajli rasmi De Jong




**BARCELONA,** Hispania

KLABU ya Barcelona imetangaza rasmi kumsajili Frenkie de Jong kutoka Ajax, huku kiungo huyo akijipanga kujiunga na klabu hiyo wakati wa kipindi cha majira ya joto kwa ada ya euro milioni 86.

Barça imekuwa ikimwania Mholanzi huyo kwa muda mrefu na sasa imethibitisha rasmi kuwa wamewapiku Paris Saint-Germain na Manchester City kuitwaa saini yake. Katika taarifa rasmi, vinara hao wa La Liga wamebainisha kwamba: "FC Barcelona na Ajax wamefikia makubaliano ya usajili wa kiungo Frenkie de Jong, ambaye atajiunga na miamba hao wa Catalunya kuanzia Julai Mosi mwaka huu.

"Gharama ya uhamisho wake ni euro milioni 75, pamoja na nyongeza ya euro milioni 11 kama ataonyesha kiwango cha juu zaidi.

Mchezaji huyo atasaini mkataba wa miaka mitano utakaomweka hapo hadi msimu wa 2023/24.

Licha ya kuwa mchezaji kijana, ameichezea Ajax mechi 65, akifunga mabao sita na kutoa pasi za mwisho 10.

Ataingia kwenye orodha ya wachezaji wakubwa waliowahi kuichezea La Blaugrana hao, akiwamo Johan Cruyff, Ronald Koeman, Patrick Kluivert na Frank de Boer.

# DOND SOKA MAGA ULAYA




# HIGUAIN ATUA RASMI CHELSEA

## ●●● Ametua Stamford Bridge kwa mkopo huku kukiwa na uwezekano wa...

**LONDON,** England

CHELSEA imekamilisha usajili wa mshambuliaji wa Juventus, Gonzalo Higuain kwa mkopo mpaka mwisho wa msimu huku wakali hao wa Stamford Bridge wakiwa na nafasi ya kumsajili jumla kwa ada ya pauni milioni 31.

**Aidha, Chelsea wana nafasi ya kuongeza mkataba huo wa mkopo mpaka Juni 2020 kwa ada ya pauni milioni 18.**

Higuain (31), alitumia nusu msimu kucheza kwa mkopo kwenye klabu ya AC Milan huku akifunga mabao nane kwenye michezo 22 aliyocheza.

Higuain ameonyesha kufurahishwa kukamilika kwa usajili huo ambapo alisema ni ngumu kuacha nafasi ya kujiunga na timu hiyo.

"Wakati nafasi hii ya kujiunga na Chelsea ilipokuja, ilikuwa ni lazima niichukue," alisema Higuain.

"Ni timu ambayo siku zote nimekuwa nikipendezwa nayo, ina historia kubwa, ina uwanja mzuri na inashiriki ligi kuu, ambayo siku zote nilikuwa natamani kucheza," alisema Higuain.

Mshambuliaji huyo aliwahi kucheza chini ya kocha wa sasa wa Chelsea, Maurizio Sarri wakati akiwa wote kwenye klabu ya Napoli msimu wa mwaka 2015-16 ambao aliweka rekodi ya kufunga mabao 36 kwenye Serie A.

Kocha Sarri, alisema amefurahishwa kuungana tena na Higuain kwenye klabu ya Chelsea baada ya kufanya naye kazi Napoli.

"Ni mshambuliaji mwenye nguvu, hasa kwenye msimu wangu wa kwanza nikiwa Napoli alifanya kazi nzuri sana, kwangu ni mmoja wa washambuliaji bora kuwahi kuwaona," alisema Sarri.

## ZISIKUPITE

### BAYERN WAMTAKA ODOI

LIVER|POOL wameungana na Bayern Munich katika mbio za kumuwania winga wa Chelsea, Callum Hudson-Odoi, ***(Bild - in German)***

### HENRY AKALIA KUTI KAVU

THIERRY Henry anatarajiwa kutimuliwa kwenye nafasi ya ukocha kwenye klabu ya Monaco baada ya kudumu kwa kipindi cha miezi mitatu tu. Leonardo Jardim anatajwa kutaka kuchukua nafasi hiyo. ***(Mirror)***

### ZAHA MBADALA WA PULISIC

BORUSSIA Dortmund wanavutiwa na mpango wa kutaka kumsajili winga wa Crystal Palace, Wilfried Zaha, kwenye dirisha la usajili majira ya joto kwa ajili ya kuziba nafasi ya Christian Pulisic, ambaye atajiunga na Chelsea. ***(Guardian)***

### KUIPIKU CHELSEA KWA PAREDES

PSG imejipanga kuishinda Chelsea kwenye mbio za kutaka kumsajili kiungo wa Zenit St Petersburg, Muargentina Leandro Paredes mwenye miaka 24. ***(Telegraph)***

### DE JONG AICHAGUA BARCA

KIUNGO wa Ajax, Frenkie de Jong, amesema alifanya mazungumzo na klabu zote za Manchester City na PSG kabla ya kuamua kujiunga na Barcelona. ***(NOS, via Mirror)***

### SPURS YAMTAKA RABIOT

TOTTENHAM wamejiunga kwenye mbio za kumuwania kiungo wa PSG, Adrien Rabiot ambaye anahusishwa na klabu za Barcelona na Bayern Munich. ***(France Football, via Star)***

### MOSES HUYOO FENERBAHCE

BEKI wa Chelsea na timu ya Taifa ya Nigeria, Victor Moses, anakaribia kukamilisha usajili wa mkopo kwenda kwenye klabu ya Fenerbahce atakapocheza mpaka mwisho wa msimu. ***(Goal)***

### GIGGS AMTABILIA RAMSEY

KOCHA wa timu ya Taifa ya Wales, Ryan Giggs, amesema kiungo wa Arsenal, Aaron Ramsey, ataimarika zaidi kama atajiunga na mabingwa wa Italia, Juventus akitokea Arsenal. ***(Sky Sports)***

### SUAREZ APEPERUKA ARSENAL

KIUNGO Mhispania, Denis Suarez, huwenda akabaki kwenye klabu yake ya Barcelona mpaka mwisho wa msimu baada ya mazungumzo ya kujiunga na Arsenal kukwama. ***(ESPN)***

### PSG YAMGANDA GUEYE

KLABU ya PSG bado inavutiwa na mpango wa kumsaili kiungo wa Everton, Idrissa Gueye, lakini hakuma ofa yoyote iliyotajwa licha ya tetesi za ofa ya pauni milioni 22 iliyotajwa mapema wiki hii. ***(Liverpool Echo)***

### MARCELO KUMFUATA RONALDO

BEKI wa Real Madrid, Marcelo anataka kuungana na mchezaji mwenzake wa zamani kwenye klabu hiyo, Cristiano Ronaldo Juventus na amewaambia mabosi wa Real wakubali ofa kutoka kwa Waitalia hao. ***(Marca via Tuttosport)***

HABARI MICHEZO

## Mgosi awatupia lawama waamuzi

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

KOCHA wa Simba Queens ya jijini Dar es Salaam inayoshiriki Ligi Kuu ya Soka ya Wanawake, Mussa Hassan "Mgosi", amemtupia lawama mwamuzi aliyechezesha mechi yao dhidi ya Baobab Queens kuwa alikuwa akiwapendelea wenyeji wa mechi hiyo.

Baobab Queens ilipata ushindi wa mabao 3-1 katika mchezo huo wa raundi ya nane ya ligi hiyo uliochezwa juzi jijini hapa.

Akizungumza na gazeti hili baada ya kumalizika kwa mchezo huo, Mgosi alisema mwamuzi wa mchezo huo hakuchezesha kwa haki jambo ambalo liliwaumiza wachezaji wake na halipendezi kwa faida ya soka la wanawake.

Mgosi alisema hiyo ndio sababu kuu iliyoifanya timu yake ishindwe kucheza vizuri na kusababisha kupoteza mchezo huo wa pili nje ya Dar es Salaam.

Mgosi ambaye aliwahi kuichezea Simba na Timu ya Taifa ya Tanzania (Taifa Stars) alisema kama hali hiyo itaendelea, itasababisha soka la wanawake nchini lishindwe kusonga mbele.

"Hebu angalieni mwamuzi hakuwa vizuri, alikuwa haelewi kabisa na aliipendelea sana Baobab Queens, kiukweli inauma na nimeumia, haukuwa mchezo wa kupoteza huu," alisema kocha huyo.

Kiungo huyo wa zamani wa JKT Ruvu na Mtibwa Sugar alilitaka Shirikisho la Soka nchini (TFF), kuongeza umakini katika ligi hiyo ili kutoruhusu matukio ya upendeleo yanayofanywa na baadhi ya waamuzi yaendelee.

## Z'bar wapongezwa kulinda utamaduni

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

NAIBU Waziri wa Wizara ya Vijana, Sanaa, Utamaduni na Michezo wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Lulu Mshamu, amelipongeza Baraza la Sanaa, Sensa ya Filamu na Utamaduni kwa kuendelea kusimamia mila, silka na utamaduni wa visiwani hapa.

Mshamu alisema hayo katika kikao cha pamoja kilichowashirikisha watendaji kutoka Baraza la Sanaa, Sensa ya Filamu Zanzibar pamoja na viongozi wa wizara yake.

Akizungumza kwa niaba ya waziri wa wizara hiyo, Mshamu, alisema lengo la wizara yao ni kuhakikisha sanaa ya Zanzibar inafanya vizuri ndani na nje ya nchi bila ya kuathiri utamaduni wao.

Kiongozi huyo alisema baraza hilo limejitahidi kuhakikisha wanasimamia vyema utamaduni wa Zanzibar hususani katika sanaa inayofanywa hapa visiwani, kuanzia muziki wa kizazi kipya, taarabu na sanaa ya maigizo.

Naye Mwenyekiti wa Baraza la Sanaa, Sensa ya Filamu na Utamaduni, Mariam Hamdani, alisema changamoto iliyopo ni uhaba wa fedha katika kuendesha shughuli zao ikiwamo kufanya maonyesho ya sanaa za majukwaani katika maeneo mbalimbali visiwani humo.

# ZAHERA AJIPANGA KUMBEBA TAMBWE

**Na Faustine Feliciane**

KOCHA wa Yanga, Mwinyi Zahera, amesema anatamani mshambuliaji wake, Amissi Tambwe, angekuwa na umri mdogo ili aweze kumtumia kila wakati katika mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara na mashindano mbalimbali ambayo timu hiyo inashiriki.

Zahera alisema anafahamu mshambuliaji huyo raia wa Burundi ana uwezo mkubwa wa kufunga na mwepesi kufuata maelekezo, lakini suala la umri mkubwa alionao linamnyima uhuru wa kumtumia mara kwa mara.

"Wengi wananiuliza kwa nini simwanzishi Tambwe...nafikiri kila mtu anafahamu kuwa Tambwe ana umri mkubwa, mchezaji kama yeye siwezi kumtumia kila wakati, ni lazima tumpumzishe kila wakati ili kuweza kupata kile tunachokitaka kutoka kwake," alisema Zahera.

**"Uwezo wa Tambwe ni mkubwa sana, nalifahamu hilo, lakini siwezi kumtumia mfululizo," aliongezea kusema Zahera.**

Aidha, alisema anatamani mchezaji huyo angekuwa na umri mdogo ili aweze kumtumia mara kwa mara.

Tambwe juzi akitokea benchi aliifungia timu hiyo bao moja katika mchezo wa hatua ya robo fainali ya mashindano ya SportPesa dhidi ya Kariobang Sharks ya Kenya, ambao wenyeji hao walifungwa mabao 3-2 na kutupwa nje ya michuano hiyo iliyofikia hatua ya nusu fainali sasa.

Mbali na mchezo huo, Tambwe amekuwa akionyesha uwezo mkubwa akitokea benchi katika michezo ya Ligi Kuu Bara na kuisaidia timu hiyo kuongoza katika msimamo wa ligi hiyo inayotoa mwakilishi wa nchi kwenye mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika.




Mshambuliaji wa Simba, Meddie Kagere (kulia), akijaribu kumtoka beki wa AFC Leopards, Kamura Robinson, katika mechi ya hatua ya robo fainali ya mashindano ya SportPesa Cup iliyochezwa kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam juzi. Simba ilishinda mabao 2-1 na kusonga mbele. **PICHA: HALIMA KAMBI**

# *Dodoma FC yajipanga kuimaliza Trans Camp*

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

KOCHA wa Dodoma FC, Jamhuri Kihwelo "Julio", amesema kuwa timu yake imejipanga kuondoka na ushindi dhidi ya Trans Camp katika mchezo wa Kombe la FA unaotarajiwa kuchezwa kesho kwenye Uwanja wa Jamhuri jijini hapa.

Mara ya mwisho timu hizo zilikutana wiki iliyopita katika mchezo wa Ligi Daraja la Kwanza na Dodoma Fc ilikubali kichapo cha bao 1-0 mchezo uliochezwa kwenye Uwanja wa Azam Complex jijini Dar es Salaam.

Akizungumza na gazeti hili jana, Julio, alisema kikosi chake kimejipanga kulipa kisasi kwa kuondoka na ushindi katika mchezo huo wa mtoano kwa sababu hawataki kuona wanafungwa kwa mara ya pili na maafande hao.

Julio alisema katika mchezo wa Ligi Daraja la Kwanza walipoteza mechi hiyo baada ya wachezaji wake kushindwa kutumia vyema nafasi walizozitengeneza na wapinzani wao kuondoka na pointi zote tatu.

"Hatutakubali tupoteze tena, tumejipanga kupata ushindi, maandalizi yetu yapo vizuri, wachezaji wapo vizuri, kikubwa ni tuombe Mungu tuweze kupata ushindi," alisema kocha huyo wa zamani wa Simba.

Kocha huyo aliwataka mashabiki wa soka wa jijini humo kujitokeza kwa wingi kuishangilia timu yake ili kuwaongezea hamasa wachezaji.

Michezo
Ijumaa Januari 25, 2019
Nipashe



Higuain atua rasmi Chelsea

HABARI UK. 30



Wachezaji wa Simba wakiwa katika mazoezi ya timu hiyo, kwenye Uwanja wa Boko Veterans jana asubuhi, ili kujiandaa na mechi ya hatua ya nusu fainali ya michuano ya SportPesa Cup dhidi ya Bandari FC ya Kenya itakayochezwa leo. **PICHA: SSC**

# Simba yajipanga kuitesa Bandari

## ●●● Lengo ni kutinga fainali na kulibakisha kombe Tanzania kwa mara...

**Na Somoe Ng'itu**

HAKUNA kulala! Kikosi cha mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba kinatarajia kuwakabili Bandari FC kutoka Kenya katika mechi ya hatua ya nusu fainali ya mashindano ya SportPesa Cup itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam.

**Simba, wawakilishi pekee wa Afrika Mashariki na Kati waliobakia katika mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika, imefika hatua hiyo baada ya kuwafunga Wakenya, AFC Leopards mabao 2-1 wakati Bandari iliwaondoa Singida United kwa kuwachapa goli 1-0.**

Kocha wa makipa wa Simba, Mwarami Mohamed, alisema jana kuwa, timu yao imejipanga kuendelea kuipa heshima Tanzania kwa kufanya vizuri katika mashindano hayo na hatimaye kutwaa ubingwa wa michuano hiyo kwa mara ya kwanza ikiwa na kikosi kamili.

Mwarami alisema kuwa, wamejiandaa kukutana na ushindani katika mechi hiyo na vile vile wanawaheshimu wapinzani wao, Bandari ambao wanafundishwa na mshambuliaji wa zamani wa Yanga, Ben Mwalala.



"Tunaangalia nini tunataka kufanya, kuhusu kikosi chetu yoyote anaweza kucheza, anaweza hata akaanza Ally (Salim), Dida (Deogratius Munishi), hiyo tutajua hapo kesho (leo)," alisema kipa huyo wa zamani wa Timu ya Tanzania (Taifa Stars).

Mwalala alisema kuwa Simba isitarajie mteremko katika mechi ya leo na tayari wameshawaangalia namna wanavyocheza.

"Tunajua wapi wana nguvu na wapi wana matatizo, naamini tutaingia kwa ajili ya kusaka ushindi na hatimaye kucheza fainali," alisema Mwalala ambaye alitamani zaidi kukutana na timu yake ya zamani.

**LAMINE KIMEELEWEKA**

Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), limesema kuwa mshambuliaji wa Simba, Lamine Moro (pichani) ni mchezaji halali wa timu hiyo kwa sababu alikamilisha taratibu za usajili.

Taarifa iliyotolewa jana na Kamati ya mashindano ya SportPesa ilisema kuwa mshambuliaji huyo raia wa Ghana ni mchezaji halali wa Simba ambaye alisajiliwa na TFF tangu Januari 15 mwaka huu na kupewa leseni ya muda yenye namba 002821M94.

Mechi nyingine ya hatua ya nusu fainali ya michuano hiyo inatarajiwa kuwakutanisha Mbao FC ya jijini Mwanza dhidi ya Kariobang Sharks ya Kenya.

# Yanga waanza kuitisha Biashara

**Na Faustine Feliciane**

BAADA ya kuondolewa mapema katika mashindano ya SportPesa Cup, Kocha wa Yanga, Mwinyi Zahera amesema hawatakuwa na huruma kwenye mchezo wao wa Kombe la FA dhidi ya Biashara United kutoka Mara utakaochezwa Jumatano kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam.

Akizungumza na gazeti hili jana, Zahera alisema hajafurahishwa na matokeo ya michezo yao miwili iliyopita dhidi ya Stand United na Kariobang Sharks) ambayo walipoteza, amepania kuirejesha timu yake katika matokeo ya ushindi.

Zahera alisema kuwa kama wataruhusu kupoteza mchezo huo dhidi ya Biashara watajiweka katika wakati mgumu na morali ya wachezaji itashuka huku wakijiweka kwenye nafasi ngumu ya kukata tiketi ya kushiriki mashindano ya kimataifa.

Wakati huo huo, habari njema kwa mashabiki wa Yanga ni kuanza kupona kwa wachezaji wake waliokuwa majeruhi kwa muda mrefu. Wakati viungo Papy Thshishimbi na Thaban Kamusoko ambao walikuwa majeruhi wameanza kucheza katika mchezo wa michuano ya Sportpesa dhidi ya Kariobang Sharks Jumanne iliyopita, kiungo mwingine wa timu hiyo, Raphael Daudi naye ameanza kujifua.

Mratibu wa timu hiyo, Hafidh Saleh, aliiambia gazeti hili kuwa Daudi ameanza mazoezi mepesi na amepewa programu maalum ambayo itamweka fiti na hatimaye kurejea uwanjani kuitumikia klabu yake.

"Kupona kwa wachezaji waliokuwa majeruhi ni jambo jema kwa sababu kunatoa wigo mpana kwa kocha (Zahera) kupanga kikosi chake kwa uhuru, Raphael ameanza mazoezi na anaendelea vizuri," alisema Saleh.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042